# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, GARSEN CONSTITUENCY HELD AT GARSEN METHODIST CHURCH

## ON

# FRIDAY 3RD MAY 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARING, GARSEN CONSTITUENCY, HELD AT GARSEN METHODIST CHURCH ON 3RD MAY 2002**

**PRESENT**

1. Com. Alice Yano
2. Com. Mutakha John Kangu
3. Com. Dr. Charles Maranga

**SECRETARIAT IN ATTENDANCE**

1. Hassan M. Mohammed - Programme Officer
2. Beatrice M. Gikonyo - Asst. Programme Officer
3. Irene Karei - Verbatim Recorder
4. Christine Ondicho - Sign Language interpreter

**Meeting started with Com. Alice Yano in the chair.**

**Omar Abdalla:** Basi wale ambao wako nje waingie ndani tungependa kuaza programme, tafadhali muingie tuanze. Commissioner Madam Alice, Commissioner Maranga, Commissioner Mutakha Kangu, Programme Officer Bwana Macharia, District Officer Kipini ambaye anashikilia kwa niaba ya D.O wa Garsen, Constituency Committee members, viongozi wa tabaka mbali mbali, viongozi wa kanisa, viongozi wa Kiislamu, ma-councillors, chiefs na wananchi kwa jumla hamjambo? Ningependa kuchukua nafasi hii mimi jina langu naitwa Omar Abdalla Zadho, ndiye coordinator wa Tume ya mageuzi ya Katiba wilayani Tana River. Ningependa kuchukua nafasi hii kuwakaribisha kwa mkutano huu wa leo wa kusikiza maoni ya wananchi kuhusu mageuzi ya Katiba, karibuni. Na naona Tumechelewa kidogo kwa hivyo singependa kuzungumza mambo mengi ili tuanze kazi ya leo. Ningependa kwanza Constituency Committee Members wajitayarishe ili nikiwaita mje mbele na kumwalika

Reverend Richard Yaro wa kanisa la Methodist ili aje atufungulie mkutano kwa maombi, kwa hivyo nikimaliza tu introduction utakuja kuomba ili tuanza mkutano rasmi. Constituency Committee Member mko tayari? Kama mko tayari Reverend njoo utuombee mkijitayarishe. Karibu Reverend. Uje uombe kwa kutumia hiki kifaa hapa.

**Reverend Richard Yaro:** Na wale walio na kofia tungetoa kwa heshima ya Mungu tupate kuomba. Majina yangu ni kama mlivyo ambiwa naitwa Reverend Richard Yaro Abiyo, nafanya na kanisa la Methodist sehemu hii ya Garsen lakini nakaa Ngao. Natusimame tupate kuomba tafadhali. Na tuombe kwa wale ambao mnaingia twafaa tuwasubiri tupate kuomba. Na tuombe, Baba tunakushukuru kwa ajili ya mapenzi yako na ulizi wako uliotulinda, tazama wengine tumetoka bali tumesafiri kwa kutumia vyombo vilivyo tengenezwa na mikono ya binadamu, lakini umetuwezesha tukaunganika pomoja hapa kanisa hili la Garsen Methodist Hall. Mungu tunapokaa kwa sababu ya Katiba na maoni tofauti tutakayokuwa nayo kwa sababu ya taifa letu la Kenya, tunaomba jinsi tunavyo anza ukapate kuanza pamoja nasi, ukabariki mazungumzo yetu, ukabiriki maoni yetu, ukabariki kuongea kwetu ili tukakuone wewe nasi tukaweze kukusifu na kukuabudu na kukutukuza kwa wema na fadhili zako zizilizo nyingi. Bariki wote watakao shughulika katika Bwana jambo lile ambalo limetufanya tukusanyike mahali hapa Mfalme. Bariki hata viongozi wetu Bwana. Bariki Makamishena ambao tumetajiwa ambao wako mbele yetu. Bariki co-ordinator, bariki committee yote inayo simamia mambo haya. Bariki wananchi wote waliongia kuleta maoni tofauti. Bariki Bwana wanasiasa, bariki Bwana makanisa, bariki Bwana hata makadhi walio kuja kwa ajili ya jambo hilo, na hata waliojitoa kwa communities. Mungu tunapoanza mkutano huu anza pamoja nasi ukatuongoze. Tuna kumbuka hata wengine ambao wako barabani kuelekea kuja kwa ajili ya mambo haya. Ukawabariki na kuwapa safari za uheri na zenye kulindwa na wewe. Tunaomba haya Mfalme tukiamini jinsi tunavyo anza utakuwa pamoja nasi na tutakapo maliza utamaliza pamoja nasi na tutajeresha sifa na utukufuku kwako. Tumeomba haya nikupitia kwa mwanao Yesu Kristo aliye Bwana na mkombozi wetu, tumeomba na kuamini. Amen.
Asanteni sana.

**Omar Abdalla Zado**: Asante sana Reverend kwa maombi. Harakisheni mkae ili tuendelee na programme, naona battery imekuja ili tupate kipasa sauti, kutusaidia kuwasiliana na kila mtu. Mtulie. Ningependa kuchukua nafasi hii kuwajulisha kamati ya Tume ya Mageuzi ya Katiba katika sehemu ya uwakilishi Bungeni ya Garsen. Kwa hivyo wale wanachama ambao wako hapa tafadhali msimame hapo mbele ili wananchi waweze kuwaona pamoja na Makamishena. Muangalie wananchi, simameni hapa. Hawa ambao wako mbele yenu ni wanachama wa kamati ya sehemu ya uwakilishi bungeni ya Garsen. Tukianzia upande huu wangu, tuko na councillor Erastus Buko, huyu mzee ni councillor Erastus Buko anawakilisha Tana River County Council. Anaye mfuata ni mama Stella Wanthe ambaye ni chairlady pia wa maendeleo ya wanawake wilayani Tana River. Hapo anayefuata ni Mohammed Zaffo, ni mwanachama wa kamati hii. Huko pia, anayemfuata ni Said Bowa, ambaye tumemchukua kuwakilisha sehemu za Chara, huyo mama ni Khadija Kefie naye tunamjua ametoka hapa Garsen, tuko na mama pia Khadija Buyo kutoka pande za Kipini. Tuko na Abdi Rahaman Gogu anawakilisha walemavu, tuko pia na Mohamed Galore pande za Tarasa naye ni mwana chama. Mimi mwenyewe co-ordinator ni mwana chama wa kamati hii, tuko pia na mheshimiwa Moru Shabaro ambaye naye ni mwana chama, tuko na mama Eunice Mungatana wa YWCA naye ni member wa kamati hii. Kwa

hivyo hawa watu kumi ndio ambao wanawakilisha Tume ya Katiba katika sehemu hii ya Garsen (inaudible) Basi sitaki kusimama hapa mda mrefu maana leo ni siku ya wananchi, nisichukue mda zaidi, ningependa sasa kumualika mkuu wa Tarafa ya Kipini ambaye anashilikilia mwenzake wa hapa Garsen, na leo ikiwa ni siku yake ya kwanza aje kabisa awazungumzie yeye anaitwa Macharia. Kwa hivyo karibu Mr. Macharia uwasalimie wananchi na utukaribishe maana tuko kwako.

**Mr. Macharia.** Asante sana. Kamishena Maranga, Kamishena Madam Alice, Kamishena Kangu, Programme co-ordinator, District Constitution Review co-ordinator, Kamati ya Constituency Constitution Review, viongozi wa tabaka mbali mbali waliofika hapa, mabibi na mabwana hamjambo? Mimi nafikiria tutakuwa mambo mawili peke yake ya kusema siku hii ya leo. Jambo la kwanza, ningependa kwanza kujijulisha kwenu na pia kwa Kamishena’s ambao wamefika siku hii ya leo. Mimi kwa jina naitwa Albert Macharia, niko newly posted D.O. wa Kipini division na kwa hivi sasa ndugu yangu D.O wa hapa Garsen anaenda kwa masomo kwa mda mdogo, kwa hivyo tunakuwa tunafanya kazi na nyinyi hadi wakati atakaporudi katika tarafa hii yake. Kwa hivyo ningemuomba tushirikiane na tuendelee na kazi ya kujenga Constituency hii nzima ya Garsen.

Jambo la pili, ningependa kuchukua fursa hii kuwaalika Kamishena’s ambao wamefika hapa katika hii shughuli ya Constituional Review, niwakaribishe rasmi katika Constituency hii yetu ya Garsen. Nitawaomba radhi kwa sababu hatukuweza kuonana nao wakati walipo kwenda katika tarafa ya Kipini jana. Lakini nilifanya bidii nikaona ya kwamba tutakutana katika hii tarafa ya Garsen. Kwa hivyo Kamishena’s mjisikie mko uhuru na mmekaribishwa rasmi katika Constituency hii.

La mwisho, ningependa kuwaomba wananchi wenzangu kwamba, hii siku ni yao. Kila mtu ako huru kutoa maoni yake bila kuogopa, bila uoga wala mapendeleo. Kwa hivyo kila mtu ajisikie ako huru awa mabwana wamefika hapa kwa minajili ya kisikiza maoni yenu. Asanteni.

**Omar Abdalla**: Basi nisingependelea kuchua mda zaidi na rudisha usukani kwa chairperson wa kikao cha leo, na anaweza kuendelea kuwatambulisha wenzake na pia awambie namna gani mtatoa maoni. Asante.

**Com. Yano:** Ni asante sana Bwana co-ordinator, viongozi wetu wote hapa, wazee, wamama na vinjana, kama mlivyo elezewa na bwana D.O leo ni siku yenu, ni siku yenu kutoa maoni kwa wana Tume ya Kurekebisha Katiba. Kabla hatujaanza kuwapatia nafasi hii muanze kutupatia maoni yenu, ya kwanza ni ya kuwa kuna utaratibu tunataka kufuata. Ukipatiwa nafasi tafadhali usichukue zaidi ya dakika tano. Tumeelewana hapo? Five minutes maximum. Halafu kama uko na written memorandum yako, tafadhali guzia tu yale maoni ungetaka pengine tuyasikie. Hayo yenye umeandika yote tutachukua kwa data analysis center yetu na tutayasome na kuangalia maneno yenu yote. Na pia pengine tuko na wale wenzetu ambao wako na shinda ya kusikia, where is aa -- Ndio, tuko na mwenye atawasaidia na ningetaka pengine kuulizia kama wako hapa wakaribie mahali fulani, pengine hapa hivi ili waweze kufuata hii kazi yenye tunafanya. Sasa iki ni kikao cha Tume na sasa tunataka kuanza kazi yetu. Tuko na orodha ya wale watu ambao wamejiandikisha hapa na tutaifuata hii orodha. Ya kwanza tuko na Councillor Bugo civic leader, tafadhali uje hapa mbele utupatie maoni yako.

**Councillor Stephen Bugo:** Mimi naitwa Councillor Stephen Bugo. Ward yangu ni ya Shirikishiro hapa jirani na hapa Garsen. Kitu cha kwanza nashukuru kwa kazi nzuri ya Tume ambao walikuja hapa kutuelimisha. Lakini kabla sijawashukuru nilikuwa nataka kuwalaumu kwa sababu sisi hatukujulishwa hivi vitabu tulipewa jana, hivi vitabu, kwa hivyo watu wengi hawatakuja kutoa views kwa sababu tuliaambiwa jana wengine hata hawana hivi vitabu viko kwa ma-chief, hawajajua watakuja ama la. Kwa hivyo hii ni kusema serikali haikutaka sisi tutoe views. Lakini wale wachache ambao watakua hapa tutatoa views inavyo takikana.

Ee, mimi views zangu nilikua nataka kuanza kuzungumza habari ya mamlaka ya serikali. President anauwezo mkubwa sana ambao sisi kama kabila ndogo kama sisi anatuvunja miguu. Kwa sababu sisi tulikuwa tunataka, mimi nataka kwa-views zangu ya kuwa serikali kama President akichaguliwa, hasiwe mwana siasa. President hasiwe mwana siasa wala asiwe na uwezo wa kuchagua moja kwa moja Ministers. Kwa sababu kama minister ni mtu ambaye anajukumu kubwa, akiwa na jukumu kubwa la nchi nzima. Kwa mfano minister wa ardhi, achaguliwe kwa sababu ya upendeleo wa siasa mtu ambaye hajui maana ya ardhi ni kitu gani, sasa huyo mtu atamaliza uchumi wetu. Kwa mfano kulikuwa na minister ambaye amechaguliwa ambaye hajui hata hii mambo ya public health. Ameweka minister for health, huyo mtu hata hajui syringe ni kitu gani. Sasa hiyo imetuchangua na hiyo ndiyo uleta uchumi wa serikali nyuma. Kwa hivyo, kwa sababu hiyo iwe minister anachaguliwa moja kwa moja anakwenda yeye anatoa views, mtu kama huyo anatumia cabinet, anatumia hii au wanasiasa. Analetwa mtu kama huyo anatukuwa scrutinized, anaangaliwa kama huyu mtu, je hicho kipaji cha kuwa minister wa hii anafaa ama hafai. Kuliko kumchagua mtu ambaye kwa sababu ya tamaa yake ya siasa nikimchagua huyu nitapata kura pahali fulani, sasa inatumaliza ndiyo mojawapo inachangia uchumi kudhoofika hapa Kenya. Kwa hivyo Ministers na President wasiwe ni wana siasa, hiyo iwe ni kazi mtu anaweza kufutwa kwa sababu ya kukosa kufanya kazi sawasawa.

Ingine, nilikuwa nasema uwezo wa kuchagua President awe kuna miaka fulani, akifika miaka fulani kwa vile mnajua, mtu akiwa mtu mdogo kadri anavyo kuwa mzee hata akili inaanza kuwa ya mtoto. Akiwa na miaka mingi zaidi atatutawala kinyama ambavyo hatajua anafanya kitu gani. Hiyo iwe hata kwa mwana siasa awe ana miaka fulani ambayo inatekelezwa kuwa huyu akifika miaka fulani hasigombee uchaguzi.

Vile vile, kwa upande ya wana siasa, iwe kuna umuhimu wa kuwa especially councillors, wana kiwango special, kama level ya form four iwe anaweza kufika achanguliwe. Iwe ndiyo qualification, kwa sababu, tuna shida kubwa especially area kama yetu ya Tana River, tuna shida ya kwamba, hii shida yote inatokea katika hizi ninii, zinachangia. Ukipeleka coucillor ambaye hajui kitu, inachangia ukabila maana hana cha kuzungumza, hana contradiction, halafu baadaye analeta shida, kwa hivyo tunataka councillor yeyote anakuja pale awe ana level ya education, ambayo hiyo ndiyo inaweza kumuwezesha achangie katika hali ya kuinua baraza.

Jambo lingine, tulikuwa tunataka ikiwezekana, chairman wa council awe anachaguliwa moja kwa moja na wananchi, kuliko

kuwacha watu wachache wanaweza kwenda kumchagua kule na kumbe huyo mtu hafai na raia hawana haja naye. Kwa hivyo chairman achaguliwe moja kwa moja na wananchi.

Jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kusema, ni kusema kwamba --- (interjection)

**Com. Kangu:** Nadhani umemaliza mda wako,

**Cllr. Stephen:** Asante sana. Ningalizungumza zaidi lakini kwa sababu time hakuna

**Com. Kangu:** (inaudible) Malizia lenye ulikuwa unasema.

**Cllr. Stephen:** jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kusema, nikuzungumza kwamba, kuhusu mambo ya ardhi, tunataka ikiwezekana, serikali isiwe na uwezo mkubwa sana, uwezo wa ardhi upewe councils ambazo ni local people ambao wanaweza kujua namna ya contribute, namna ya watu wao watakavyoweza kukaa.
Asanteni sana.

**Com. Yano:** Asante sana Bwana Bugo. Tafadhali nenda kule kuna kitabu tuna-sign hapa. Asante sana. Wapili ni Mr. Joel Ruhu.

**Joel Ruhu**: Asante sana wasimamizi ni wetu wa kusikia maoni yetu, wasimamizi wetu wa Katiba. Mimi kwa majina naitwa Joel Ruhu, ni mwenye kiti wa kitaifa wa chama cha KUSCO. Chama cha KUSCO ni chama kinacho simamia vyama vyote vya kuweka akiba na kukopa. Savings and Credits Co-operatives in this country. Kwa vile mda mliotupa mama kwenye kiti ni mdogo sana wa dakika tano kwa kila mtu, sikudhania ungetupatia mda huo tulirauka, tukakesha hapa kwa ajili ya kuwangojea nyinyi na kwa bahati mbaya sasa unakuja unatupa dakika tano. It is too unfortunate, lakini hata hivyo nitajaribu niwezavyo, nizungumze kwa mda wa dakika tano. Na ikiwa nitaacha mengine, basi wenzangu watanisaidia.

Jambo la kwanza ambalo ningependa kuzungumzia ni kuhusu hali ya ardhi. Land tenure system na policies zake. Mimi ningependa kutoa maoni yangu kwamba ingekua jambo la busara kwa serikali yetu ya Kenya kuhakikisha ya kwamba mipaka ya utawala, District boundaries and Provincial boundaries ziingizwe kwenye Katiba ili tuweze kujua ya kwamba Kenya iko na district ishirini na mbili, arobaini na mbili au kitu kama hicho. Lakini hatungepanda tuwe na ma-district ambayo yanakuwa created on political grounds. Kwa hivyo, ikiwa, Katiba itatengenezwa ili mipaka ya wilaya iwe iko katika Katiba hakutakuwa na mtu wa kuchezea mipaka ya wilaya zetu. Vile vile, katika wilaya ya Tana River we are being encroached, wilaya yetu inanyanganywa na wilaya zingine. Tunanyanganywa kama kwa mfano, ukitoka Malindi, Kilifi District kuja Tana River unakuta kutoka Sabaki mpaka wetu na Kilifi zamani ulikuwa ni Sabaki, ule mto wa Sabaki, but today mpaka wetu umeondolewa kutoka mto wa Sabaki mpaka ukaja Kurawa hapa na kwa sababu yule anaye uondoa hatujui ni nani, na uenda today mmekuja

hapa mnatusikiza maoni yetu mkiwa mko wilaya ya Tana River. Kesho Madam Kamishena na Kamishena's wako, mtakuja mtuone hapa hatuko wilaya ya Tana River na imekuwa ni wilaya nyingine tena. Kwa hivyo tungetaka mipaka yetu ilindwe. Hatutaki mtu wakutuingilia mipaka yetu, ili mipaka irudishwe. Vile vile na wilaya yetu ya Tana River mipaka yake ibaki vile vile. Wasiwasi wetu pia ni kwamba tuna wilaya ambazo there are still encroaching on us. Kama wilaya ya Ijara, wilaya ya Garissa they are claiming kwamba mpaka ubalishwe uwe the river bank. Tunataka kusisitiza hapa leo kwamba hatutaki kama watu wa Tana River mipaka yetu ibadilishwe. Tunataka mipaka ibaki ile ile, ni kweli si kweli wananchi?

(Clapping)

Mipaka ikibakia vile pia itasimamisha hali ya kutoelewana na watu kupigana. Shida zinazotokea za hata vita zinakuja kwa sababu ya watu ambao asili yao ni watu wa Tana River, na wakiingia hapa hawaishi kwa amani, kama vile watu wa Tana River walivyozoea kuishi kwa amani. Kwa hivyo, tungeomba ya kwamba mipaka idumishwe na iabki ile ile hatungetaka mipaka ya Tana River abadilishwe hata dakika moja. We do not want to shfting of boundaries.

Vile vile ningeomba kwamba ugawanyaji wa ardhi katika Tana River uendelee, na mbali na kuendelea iwe ni lazima ya kwamba kila mwanachi wa Kenya apewe kipande chake cha ardhi. Kila mwananchi wa Kenya apewe kipande chake cha miliki ardhi. Kwa sababu hiyo ni wajibu wa mwananchi na ikiwa mwananchi wa Kenya atakuwa treated kama squatter hatai akiwa Kenya hatakwenda nchi gani apewe ardhi. Kwa hivyo, ni jukumu la serikali ihakikishe ya kwamba kila mwananchi wa Kenya amepewa nafasi ya miliki ardhi. Kwani ugawanyaji wa ardhi ni muhimu na iwe ni sheria katika Katiba, it has to be clearly spelled out in the Constitution, that it is the right of every Kenyan to own land, na waki-own land, na ikingawanywa, yaani zile gharama za kugawanya hio ardhi na kupewa Title Deed zisiwe ni za gharama za mwananchi kulipa. Serikali iwagawanyie ardhi na gharama zile za kugawanya ardhi ziwe ni jukumu la serikali.

Pia ningependa kupendekeza ya kwamba, kwa sababu ya hali ya kutoelewana, vita za kila wakati kwa sababu ya ufugaji, ulishaji, ukulima, ningependekeza ya kwamba, tuwe na land laws au rules ambazo zitatufanya tulizingatie. Ikiwa mtu atatoka na ng'ombe zake North Eastern Province kuja Tana River kulisha ng'ombe zake awe anapewa ruhusa na wazee wa Tana River. Iwe ni wafugaji wa Tana River na wakulima wa Tana River, kuwe na vikao ambavyo nivya wazee na vinakubaliwe ki-Katiba, kuwezo kuwazuia. Watu wa nje kuingia freely na ku-graze ng'ombe au mifugo yao katika wilaya Tana River.

Jambo la pili nikitoka upande wa ardhi ningependa kuingilia upande wa Natural Resources na utumizi wake. Kama mnavyojua wilaya yetu ya Tana River sisi tumeitwa watu wa Tana River na mto wa Tana River kama mnavyojua umeanza kutoka Mt. Kenya uko. Ukaja Meru ukazunguka mpaka ukaja ukaishia Tana River. Najua dakika zimeisha, Madam asante sana. Najua mto huu ndio rasilimali yetu kubwa, it is the main natural resource of the Tana River people. Na tungependa matumizi ya mto huu yaangaliwe vikali sana, hivi sasa tunaanza kufa, tunaanza kukosa maji. Mto wa Tana River umeenza kukauka kwa sababu ya matumizi mabaya ya mto huu kutoka upande wa juu na tungependa matumizi ya mto huu yaangaliwe ki-Katiba, yaangaliwe kikamilivu ndani ya Katiba ili tusije tukaadhirika na uangamia sisi ambao tuko mwisho wa mto wa Tana River.

Nikienda kumalizia, Madam Chairlady, ningependa kupendekeza ya kwamba now on political governance: Ningependa kupendekeza ya kwamba nchi yetu ya Kenya itawaliwe au iongozwe na two political parties. Na iwe katika Katiba ya kwamba vyama vya upinzani katika Kenya viwe ni vyama viwili. Kama nchi zile zilizoendelea America, Britain, unakuta vyama vya siasa ni viwili peke yake, na ikiwa hivyo itaondoa ile hali ya kuwa na vyama vya ubakila, ni kweli si kweli wananchi? Vyama vya ukabila vitakuwa vimeondoka na tutakuwa tumebakia na vyama ambavyo wananchi wa Kenya watang'ang'ania bila kubagua huyu ni wa kabila gani au huyu ni wabila gani.

Na mwisho kabisa ningependa kuomba ya kwamba kama inawezekana ingiizwe katika Katiba ya kwamba mbunge akichanguliwa, na akiwa ha-perform, Katiba itoe uwezo wa wananchi kumuita Mbunge huyo na kuchagua mtu mwingine, bila kungojea wakati wake kuisha.

(Clappings)

Otherwise I have no quarell with time.

**Com. Yano:** Asante sana Bwana Ruhu. Tafadhali hata sisi tunauzunika kwa ajili tunawapatia tu dakika tano na pia nyinyi mnajionea kuwa mko wengi sana. Na tukisema ati tupatie mmoja wenu pengine dakika kumi hivi, hatutaweza kupata maoni kutoka nyinyi wote. Nafikiria tumeelewana hapo. Sasa wakati huu ni Bwana Nathaniel Amuma.

**Nathaniel Amuma:** Madam Chairlady ninakushukuru kwa kuwa siku ya leo umekuja hapa kuchukua maoni yetu. Mimi sina mengi ya kuzungumza mbali ambayo ningetaka kuzungumza yako kwenye karatasi hii. Sanduku hili ndilo linaonyesha au litamuonyesha yale ambayo kuwa ni maoni yangu ambayo ningependelea yafanyike.

Asante.

**Com. Yano:** Asante sana. Asante sana Bwana Nathaniel Amuma. Tuko na pia Bwana Magid Murua.

**Magid Marua**: Asante sana kupewa kwa nafasi hii kuongea mambo kidogo nafikiri mengi yashazungumziwa. Lakini mimi ningepitia tu yale ambayo pia nimeona hayajazungumziwa. Kwa mfano, uraia wa Kenya. Uraia wa Kenya upewe nafasi kwa wale watu ambao ni automatic yaani makabila arobaini na mawili, yale yalikuweko wakati wa kujitawalia uhuru wetu. Kwa sababu kuna makabila mengine ambayo yanachipuka kila siku, na hayo makabila kwanza yanaleta matatizo ya kung'ang'ania sehemu fulani. Kwa hivyo kitu cha kwanza ni kwamba makabila yabakie asili yale yale, na hao ndio wapewe uraia automatic. Yeyote ambaye hakuingia katika makundi hayo ambayo ni ya kikabila basi kuwe na sheria nyingine ya kumueka hapo.

Kuhusu jukumu la usalama au ilinzi wa nchi, ningependelea kuwa chochote kile ambacho kinahusu usalama au ulinzi wa nchi hii kiundiwe kamati maalam ya wananchi wote wa Kenya. Popote pale ambapo kutakuwa na matatizo hao wawe wanaweza kuchukua wajibu wa kushughulikia hilo jambo.

Kuhusu vyama au siasa ya nchi, mimi ningependelea kwamba siasa yetu ya majimbo. Kwa sababu hasa mkoa wa Pwani tumeadhirika zaidi. Mahakama za Kadhi nafikiri nilipitia kile kitabu, ningependea kwamba pia, makadhi wakuu au makadhi wa kawaida, wawe na visomo sawa na wale makadhi wengine. Isipokuwa tu, kwa kuongezea lazima wawe na stakabadhi maalum za taasisi za kiislamu.

Kuhusu swala la ardhi, ambapo liliongelewa na mwenzagu sitaki kurudia lakini kuna hatari kuu ambayo inatukabidhi hapa wilaya ya Tana River. Nafikiri mwenzangu aliongea kuhusu kwamba mpaka asili wa Tana River ulikuwa Sabaki. Lakini kulingana na sheria ya sasa ya kwamba, mwananchi wa kawaida anawakilishwa na council yake, kulikuwa na mapatano fulani ambayo siyo ya kawaida. Kati ya council yetu na wale wagiriama wadogo walioko huku, kwa hivyo walikuwa wakichukua nafasi hiyo yakutengeza sheria. Ukibeba kibao hicho na kukiweka hapo. Baada ya mda kidogo, wanakibeba wanakisongesha, kwa hivyo si ajabu baada ya nyinyi watatekeleza hapa Garsen.

Upande wa pili pia, kama mwenzangu alivyo ongea, wenzetu huko wamechukua nafasi ya kuanzisha wilaya mahali ambapo hapawezekani. Sasa kulingana na Katiba mpya, tunapendelea hivi, mipaka ya mkoa na wilaya ibakie ile ile ya asili wakati tulipopata uhuru. Kama kuna wilaya yoyote inataka kujigawanya basi ijigawanye kutokana ile mipaka ya asili yake. Isiingilie mpaka wa wilaya nyingine. Kwa hivyo, kwa hayo machache nafikiri, mengi niliandika hapa na ni mengi sana, lakini nitawaachia wenzangu nafasi, kile ambacho sikuongea wataendelea kukiongelea.

Asanteni.

**Com. Yano:** Asante sana Bwana Magid. Mwenye anafuata wakati huu ni Bwana Ali Barisa, Bwana ali Barisa na tafadhali unaanza kwa kujitambua majina yako yote.

**Ali Barisa**: Mimi kwa jina naitwa Ali Barisa. Natoka Mera location katika Garsen division. Nimeona mwenzangu mwingine alizingumza hapa, amezungumza yale ambayo ningeyazungumza, lakini nitaguzia kidogo upande wa mazingara na mali asili. Kulingamana na mali ya asili na mazingara yake, katika hii Tana delta yetu, kutoka Kibauni mpaka Kipini, kuna rasilimali ambazo zina milikiwa na serikali, sehemu ambapo wananchi ambao wamezaliwa pale pale mahali hawapati haki zao. Kwa hivyo, ni maoni yangu kwamba popote ambapo, kuna mazingara ambayo yana rasilimali ndani yake, yule mwananchi ambaye amekuwa pale, na imemkuta pale ile mali awe na yeye, atambuliwe na apate haki. Ikiwa ni 50% pamoja na serikali au 75% lakini ashirikishwe katika yale mazingara. Maanake tunaona kwamba, kuna maonevu fulani ambayo yanatokea upande huu.

Na pili, ni habari ya haki ya ardhi na mali. Kama wenzangu walivyo zungumza, habari ya ardhi yetu, ni kwamba Tana River tuna tishwa juu ya mipaka, na tungeomba ile ile mipaka ambayo mkoloni ameikabidhi nchi yetu Kenya mwaka wa sitini na tatu iwe ni ile ile. Hatukatai mtu kuja kufanya mendeleo katika wilaya yetu lakini, ikiwa atatambua kwamba hapa mahali ninapokaa ni mahali fulani, atapatana na yule mwenye ardhi au ploti wataelewana. Lakini mipaka iwe ni ile ile na pia umulikaji wa ardhi, kila mwananchi apate kibali chake, Tana River hakuna mtu yeyote ambaye anamiliki ardhi kialali. Kwa hivyo, tungeomba kila mtu apate kibali cha ardhi yake anayoishi. Asante sana.

**Com. Yano:** Asante sana, Bwana Ali Barisa. Mwenye anayefuata wakati huu ni Dickson Njiru.

**Dickson Njiru:** Mapendekezo yangu leo - jina langu ni Dickson Njiru na nataka kutoa mapendekezo ya kurekebisha Katiba kuhusu uongozi. Kuhusu uongozi, Katiba tuliyo nayo sasa, inawekea umuhimu wa elimu, lakini imeacha kuweka mahitaji ya kiuadilifu. Kwa hivyo, napendekeza kuwa, katika Katiba, tunayopendekeza uongozi uende na uadilifu. Napendekeza kuwa, mtu yeyote anayegombania kiti cha udiwani, ubunge na urais aitajike kuwa mwaminifu, kiwango cha kuwa asiwe na historia yoyote ya uhalifu. Kutokuwa na majili haya katika Katiba ya sasa kumechangia wezi kujazana katika mabaraza ya mawaziri, bungeni na hata katika ikulu. So, kurekebisha hali hiyo, pia napendekeza kuwa mtu yeyote ambaye ni kiongozi, wakati wowote akiwa katika huduma ya umma aishi ama awe juu ya laana ya ualifu. Hatutaki kuwa na viongozi ambao wako bungeni, na bado wako na case za uhalifu mahakamani.

Mapendekezo yangu mengine ni kuhusu ardhi: Kuhusu ardhi, napendekeza kuwa sheria ama Katiba, izungumzie kuwa raia ama wananchi asili, waliotajwa katika kifungu cha tisa cha Katiba ya sasa ni kina nani. Mapendekezo yangu ni kuwa katika Katiba tuliyo nayo wakati itakayorekebishwa, kifungu cha tisa kinachozungumzia ardhi, kiseme ya kuwa wananchi halisi ni wale ambao kutoka tarehe moja mwezi wa December mwaka wa ishirini na tatu walikuwa ni wakaaji wa hapo. Pia napendekeza kuwa, haki ya kumiliki ardhi itambuliwe kama haki ya kimsingi katika Katiba.

Pia napendekeza ya kuwa uwezo wa Rais wa kuunga Tume uwekwe chini ya idhini ya Bunge. Pia napendekeza ya kuwe kuwekwe sheria zitakazoongoza Tume kama hizo. Tume hizi, niza umma siyo za mtu binafsi na tunataka ripoti hizo zisiwekwe kwa bedroom ya mtu. Siyo kuwa leo kunakuwa hii Public Commission halafu ripoti inakuwa siri, mtu anaenda kuilalia. (intejection) (inaudible) Kwa hivyo, tunaomba ya kuwa kuwekwe sheria itakayo lazimu Tume yoyote itakayoundwa na Rais ama itakayo undwa na Bunge, ipewe mda wa siku zisizopungua sitini kutoka siku ya mwisho waliofanya kikao cha adhara, watoe ripoti yao kwa wananchi direct. Hakuna hii sheria inayowahitaji kupeana ripoti kwa Rais iondolewe. Ripoti iletwe kwa umma direct.

Asante.

**Com Yano**: Asante sana, na kama ulikuwa umeongea jana tafadhali, na leo uko na jambo yenye ungetaka kuongezea kidogo

umesema jana uachie watu wengine nafasi, uachie wale pengine hawajaongea wapate kupatiana maoni yao pia.

**Com. Kangu:** I suggest we don't break , instead those one's who have gone to the mosque and they were called but were not here, you just put an X, they will come after prayer, we will continue with the others.

**Com Yano:** Na wale wenzetu waislamu naelewe ya kuwa kukifika saa sita mngetakikana muende kusali, saa sita unusu. Ikifika wakati huo munaweza kuenda, tukiita majina yenu na hamko tutawangojea mpaka mrudi ili tuirudie hiyo orodha ya majina tuwaite halafu muendelee kutupa maoni yenu. Hiyo ni sawa sawa?

**Congregation**: Sawa.

**Com. Yano:** Ndiyo, tuendelee sasa, tuko na Pauline Komora, Mrs. Pauline Komora.

**Mary P. Komora:** Kwa jina naitwa Mary P. Komora. Kwanza naomba Tume iniongeze mda kwa sababu mimi nazungumzia wanawake wa Garsen North. Kwa hivyo, naongezea kuwa nazungumzia kutoka Garsen mpaka Mwina kule. Kwa hivyo, ninaomba Commission iniongezee mda wa kuzungumza. Kwanza nazungumzia mkuu wa Katiba. Wambunge wako na wakati wao ambao wanaupitisha mswada wao kwa asimia sitini na tano. Tunaomba, kubadilika Katiba iwe ni kazi ya wananchi, wahusishwe kurekebisha Katiba kwa kura ya maoni.

Mamlaka ya Rais, ile mamlaka ya kuwa ama kuchaguliwa kwa Rais kwa kura ishirini na tano kwa mikoa mitano, ibadilishwe. Iwe ni asimia hamsini na moja, kama hakuna mgombeaji ambaye alipata asimia hamsini na moja, iwe na duru ya pili kwa wale wawili waliopata kura nyingi.

Tunapendekeza msamaha wa Rais ambao anatoa upunguzwe. Kwa mfano, kutoa msamaha wa kiuchaguzi, kuvunja kwa Bunge wakati anataka yeye mwenyewe. Na Rais asiwe na uwezo wa kuteuwa wafanyi kazi mbali mbali, kwa mfano, mkuu wa sheria, makatibu wa kudumu na wakurugenzi. Uteuzi huo upewe Tume ya Utumishi wa Umma.

Rais hasiweze kutangaza vita wakati anafikiria mwenyewe.

Rais hasiwe na uwezo wa kuunda na kuvunja wizara za serikali.

Rais hasiwe na uwezo wa kuunda Tume mbali mbali. Kuunda Tume iwe ni idhini ya Bunge.

Serikali ya wilaya, tunapendekeza kiwango cha elimu cha madiwani kiongezwe. Ili awe mtu wa kidato cha nne.

Mapendekezo yetu kuhusu mfumo wa uchaguzi. Asilimia ishirini na tano kwa mikoa mitano itolewe. Wagombeaji kiti wa urais, ubunge na udiwani wawe wagombeaji huru, wasiwe wakisimamiwa na vyama.

Haki ya vikundi vya wanyonge. Katiba iweke maangizo maalum kuwawezesha vikundi kama kina mama, watoto na walemavu kupata haki zao za uongozi na kutoa maoni. Ikiwezekana vitu vyote maalumu katika Bunge na mabaraza ya miji na ya wilaya, vitengewe kina mama na walemavu. Kuwe na sheria kuwasaidia wanyonge kama kina mama, watoto na walemavu kupata misaada ili waweze kujiendeleza.

Haki ya kumiliki ardhi na mali: Kila mwananchi aweze kumiliki ardhi na mali, akiwa mwanaume, mwanamke, mtoto ama akiwa mlemavu. Ikiwezekana ardhi yote ---wanaongeza district kila wanapotaka wenyewe. Na hiyo inaleta mvurutano kati ya wananchi.

**Com. Yano:** Tafadhali Mary, naona ya kuwa umeandika Memorandum yako, ungeguzia juu, halafu utatupa Memorandum.

**Mary:** Haki ya kimila, kikabila na maeneo: Sheria za utamaduni zote za kimila tunapendekeza zipewe ulinzi na serikali. Sheria zote za kimila zinazo changia ubaguzi na unyanyasaji kwa kina mama na watoto na wasiojiweza lazima ziharamishwe na Katiba. Kwa mfano, ndoa ya lazima na kutahiriwa kwa wanawake.

Mapendekezo yetu juu ya Bunge: Uwezo wa Rais wa kupinga miswaada inayo pitishwa na Bunge uondolewe, kwani Bunge ndio sauti ya wananchi.

Tunapendekeza uchaguzi bila kuvunja Bunge.

Muundo na mfumo wa serikali: Serikali ya Majimbo, tunapendekeza serikali ya Majimbo kwa sababu serikali ya sasa imeshindwa kupatia kila mwananchi maendeleo. Kusiwe na malingano yoyote kati ya serikali na Bunge. Pia tunapendekeza kuwa serikali, Rais na mawaziri wasiwe na constituency zao. Wawe ni watu huru.

**Com. Yano**: Asante sana, Mary, unaweza kutupatia hiyo Memorandum yako. Mary tafadhali nenda kule u-sign records zetu. Tafadhali ukipatiana maoni, fikiria pia juu ya wenzako, ili pia wapate wakati wa kupatiana maoni yao. Stick to the time please. Sasa wakati huu, tuko na Bahati Komora, tafadhali njoo.

**Bahati Komora:** Kwanza kwa majina naitwa Bahati Omora, kutoka sehemu ya chini ya Garsen. Yangu ni machache, nina karatasi kubwa sana, lakini nataka kuguzia mambo muhimu ambayo hayajazungumzwa bado. Kwanza kupitia ile Katiba ya zamani, Katiba ya zamani ilikuwa haina utangulizi. Tumependekeza Katiba ya sasa inayoenda kuandikwa iwe na utangulizi.

Ukuu wa Katiba. Mamlaka ya Bunge yakubadilisha sehemu yeyote katika Katiba yaondelewe. Sababu wambunge wanakaa, bila kupitia kwa wananchi waliowachagua na wanaondoa sehemu fulani, ambayo huku chini inatunyanyasa. Wananchi wahusishwe katika kubadilisha kura za maoni, kupitia sehemu hizo Bunge wanazotaka kubadilisha.

Tukienda kwa vyama vya kisiasa. Mamlaka ya msajili wa vyama yapunguzwe ili idhini ya kuandikisha isitoke kwake.Tukienda sehemu nyingine, kuwe na idadi maalumu ya vyama visizidi vinne, kwa kupunguza ghasia na gharama. Hivi vyama vya kisiasa ambavyo viliingia vikawa vingi vinatuletea ghasia na kuleta gharama nyingi sana.

Jambo lingine, sheria ibadilishwe ili iruhusu mwananchi yeyote ambaye ni mwana chama wa chama kimoja, cha vyama vilivyo sajiliwa agombee udiwani, ubunge na urais kama mgombezi.

Tukienda kwa muundo wa serikali, tulisema kama wanawake tuendelee kuwa na Rais ambaye ni Mbunge, lakini mwenye kupigiwa kura moja kwa moja wapiga kura. Lazima Rais atakaye chaguliwa awe amepata zaidi ya nusu ya kura zilizopigwa.

Tumependekeza mfumo wa serikali ya Majimbo kama wanawake wa kule Garsen South. Tukienda sehemu za Bunge, sheria irekebishwe ili kila anayetaka kugombea kiti cha ubunge hasiwe na historia ya uhalifu. Wambunge wachangie mijadala na kupitisha sheria baada ya kuzingatia maoni ya wale waliowachagua.

Tumesema kuwe na muongozo maalum wa kuongezea wanawake bungeni. Bungeni hakuna wanawake wa kutosha, tumependekeza na sisi wanawake tuwekewe nafasi nyingi, ili tuweze kuingia bungeni.

Tumesema uwezo wa Rais wakuvunja Bunge uondolewe, sababu wabunge wanaenda kwa mikutano na mara unasikia katika radio Bunge limevunjwa, na wabunge wanaenda manyumbani wiki mbili, wiki tatu, hali huku wanalipwa mishahara elfu mia tano. Tumesema uwezo wa Rais wakuvunja Bunge uondolewe.

Tukienda kwa mamlaka ya serikali, Rais awe amechaguliwa na wingi wa kura zinazofikia asili mia hamsini na moja. Uwezo wa Rais wa kuunda wilaya nao tumependekeza uondolewe na upewe wabunge.

Tukienda mfumo wa uchaguzi ---(interjection)

**Com Yano:** wakati, wakati.

**Bahati Komora:** Nimemaliza, subiri kidogo tafadhali, mfumo wa wabunge na madiwani maalum ubaki lakini waliochaguliwa lazima wawe akina mama. Haki za kimsingi, kuwekwe sheria ya katiba ya kuwezesha raia kudai haki zao kikatiba.

Umilikaji wa ardhi: Tumependekeza Katiba itambue umilikaji wa ardhi kama haki ya kimsingi. Katiba iweke sheria zitakazosaidia wenyeji wa asili kumiliki ardhi yote itakayo tajwa chini ya kifungu cha tisa cha Katiba. Katiba itambue haki ya makabila yaliyokuwa yanaishi katika sehemu zilizotajwa, katika kifungu cha tisa cha Katiba mwaka wa sitini na tatu kama wakaaji asili.

Wanawake wawe na haki sawa na wanaume za kumiliki ardhi. Neno ardhi ya serikali itolewe katika Katiba na ardhi yote iwe chini ya usimamizi wa mabaraza ya wilaya na miji. Kuwekwe kiwango cha kumiliki ardhi.

Tumeenda mbele tukasema serikali haitambui haki za watoto, walemavu, wajane na kadhalika. Sababu tunaona watoto wanaranda randa, hawana elimu na serikali haitambui elimu kwa watoto. Watoto wanasoma serikali haiwapatii makazi, na sisi kama wanawake tumependekeza serikali wanapounda Katiba yao mpya, wachukue hatua kuonyesha kwamba watoto wetu hawafai warande rande na kazi zipatikane.

Asanteni.

**Com. Yano:** Asante sana mama Bahati tunashukuru kwa yale uliyosema. Danson Mungatana.

**Danson Mungatana**: Nitajaribu kusema kwa uchache sana, Madam Chairlady wa Commission. Jina langu naitwa Danson Mungatana. Kuna kitu kimoja ambacho kimetuweka sisi watu wa Tana River nyuma sana. Na hiyo ni kukosa pesa za kiserikali, kuletwa kwa miradi ya kiserikali hapa mjini Tana River. Ninataka kuzungumzia jambo la Public Finance. Katika Katiba ambayo tuko nayo sasa, inasema ya kwamba waziri wa finance ndiye peke yake anapewa mamlaka ya kuleta zile budget kwa kila mwaka kwa serikali, kwa Parliament, na Parliament wanazungumzia, na Parliament wanapitisha ni pesa gani zitaenda kwa miradi gani. Sisi watu wa Tana River tunaona kwamba mfumo wa namna hii, umetuacha sisi nyuma sana, kwa hivyo tunapendekeza ya kwamba katika Katiba mpya itakayo kuja. Waziri huyu wa finance aambiwe kabisa yakwamba ni lazima akiwa anapanga mipango ya kutumia zile pesa za wananchi wa Kenya nzima hapa kwetu Tana River na sisi tuwe na percentage fulani au sivyo wananchi?

(Clappings.)

Na sisi tuwekewe miradi ambayo serikali itakuwa ina-sponser na pesa zake na waziri wa finance akiwa anasimama atakuwa akisoma mpaka Katiba akisema kuwa Tana River District watapeleka pesa fulani, kwa ajili ya mipangilio fulani, na sisi pia tule matunda ya uhuru, au sivyo?

**Audience:** ndio.

Jambo la pili, nimesema nitasema mambo kidogo maanake nimeandika mengi. Katika Katiba hii yetu ambayo tuko nayo. Kifungu cha mia moja na kumi na tano, kinazungumzia kwa urefu sana, mambo ya trust land. Sisi watu wa Tana River na Garsen haswa, tunaomba ya kwamba, mamlaka ya kugawa ardhi yasiwe Nairobi, yasiwe mahali popote. Katiba mpya iseme kwamba, mamlaka ya kungawanyia wananchi iwe kwa wale wazee na watu wa county council, au sivyo? Maanake ni sisi ndio tunajua hii nchi mwenyewe ni nani, na mwenyewe si nani. Tunataka Katiba mpya ipatie mamlaka hii kwa wale wananchi.

Na nikiwa ninazungumzia urithi wa Tana River District. Katika Minerals and Oils ambazo, tunaweza zikawa zinapatikana hapa, hapa kwetu Tana River kuna mineral moja inaitwa Gypsum, lakini hakuna mwananchi wa Tana River yeyote ambaye amepata pesa kutokana na hiyo mineral wakati huu, sote tu masikini na mineral hii ni yetu hapa hapa, Tana River, inafaidi watu wa nje. Sisi tunaomba katika Katiba mpya, iseme kabisa wananchi wenyewe watatawala zile minerals ambazo zitapatikana katika nchi ambayo Mungu ametupatia, kweli si kweli?

Kwa sasa Katiba inasema ya kwamba una haki ya kuwa na trust land, section 15 subsection 1, lakini huna haki ya kusimamia minerals zako. Kwa hivyo, bila kuchukua wakati mwingi tunaomba katika Katiba mpya, sisi watu wa Tana River, nchi yetu bado haijafanyiwa exploration yoyote. Pengine hapa tunasimama, tumesimama katika mahali kuna mafuta, hatujui. Haya mafuta yakipatikana, sisi watu wa Garsen basi hatuna haki hata kidogo. Lazima tuko nayo au sio? Kwa hivyo tunaomba katika Katiba mpya ya kwamba wananchi, zile minerals ambazo ziko kwao na wao wapewe mamlaka ya kufaidi na sisi pia tupate utajiri.

Asanteni sana.

**Com. Yano:** Asante sana, Bwana Mungatano. Kwani (inaudible) kuna na wakili, wakili wapenda kuongea sana. Lakini asante tumeshukuru. Mwenye anafuata ni Councillor Yusuf Godana.

**Yusuf Godana**: Commissioners na wananchi nyote, hamjambo? Mimi ni mwana Majimbo, napendekeza kwamba mfumo wa serikali wa Katiba hii mpya uwe wa Majimbo.

**Com. Yano:** Majina tafadhali.

**Yusuf Godana**: Mimi naitwa Councillor Yusuf Hussein Godana, nominated. Napendekeza kwa dhati kwamba mfumo wa Katiba mpya ya Kenya uwe wa Majimbo, na kwa hivyo basi, katika pendekezo hilo, napendekeza pia, kwamba jina la jamhuri ya Kenya libadilike kidogo iitwe People Federal Republic of Kenya, badala ya Republic of Kenya, iitwe People Federal Republic of Kenya. Na serikali isiitwe Government of Kenya pekee, iitwe Peoples Federal Government of Kenya. Na muundo wa serikali uwe katika vinyanda tatu, central government kule Nairobi, regional government, majimbo na local authorities, yaani serikali za mitaa kama hizi za wilaya na za miji. Central government itakuwa na Parliament yake kule Nairobi na itakuwa na wawakilishi ambao watukuwa wakichaguliwa na wananchi moja kwa moja kutoka katika kila constituency na

walipwe mishahara yao na marupu rupu yao kutoka kwa Central Consolidated Fund ya serikali kuu.

Napendekeza pia, kwamba kuwe na Rais, Ceremonial President. Kiongozi ambaye ni wakisherehe tu, ambaye atakuwa ni kiongozi wa nchi, ambaye atapigiwa kura na wananchi wote nchini lakini hasiwe chini ya umri wa miaka arobaini. Na awe na elimu isiyopungua angalau degree kutoka chuo kikuu kinacho tambuliwa. Ingawaje ni lazima awe amedhaminiwa na chama fulani cha kisiasa kilicho andikishwa, lazima awe si mjumbe wa Bunge anayewakilisha sehemu yoyote ya ubunge. Awe ni mtu amechaguliwa na wanakenya wote kuhudumia wanakenya wote bila kujali kuwa mimi ni mbunge wa Baringo Central, ni mbunge wa Garsen ni mbunge wa wapi.

Hali kadhalika kuwe na waziri mkuu, ambaye hatachaguliwa na Rais, atachaguliwa na wabunge katika Bunge. Waziri mkuu atakuwa ndiye mwenye serikali, ndiye kiongozi wa serikali, wakati Rais ni kiongozi wa nchi, waziri mkuu atakuwa ni kiongozi wa serikali. Na wote watakaa katika ofisi kwa mda wa miaka mitano, labda theluthi mbili ya wabunge wapige kura ya kukosa imani na wao, na wawatoe kulingana na sheria.

Waziri mkuu, kutokana na watu ambao siwabunge, watu experts kutoka nje ya Bunge. Kwa mfano, Yusuf Godana ni expert wa pahali fulani, wa kitu fulani, awachagua mawaziri kutoka nje ya Bunge ili wale wabunge wabaki na ubunge tu, isije ikawa oh Rais amenipa kazi nyingi kule Nairobi.

Na hao watakaa kwa mda wa miaka mitano, labda watolewe na vote of no confidence ya two third majority vote ya wabunge. Wabunge wa federal Parliament lazima wawe angalau na diplom, wawe na elimu ya angalau diploma kutoka chuo kinachotambuliwa cha elimu au cha kitaaluma. Na wawe wanachama wa vyama vilivyo andikishwa na serikali, na wachaguliwe na wananchi moja kwa moja kwa mda huu wa miaka mitano. Na mmoja akitoka chama chake kilicho mchagua, saa hiyo speaker amtangaze kuwa yeye si mbunge tena ana kiti kiwe wazi.

Tukienda kwa mabaraza ya regional assemblies, kila administrative division katika jimbo lolote, na ninaposema jimbo na-refer kwa hii mikoa tuliyo nayo. Nikisema jimbo la Pwani ni huu mkoa wa Pwani, nataka mnielewe. Kila administrative division iweze kuchagua muwakilishi katika Bunge la jimbo moja kwa moja. Kura ya mtu kwa mtu. Nikiendelea nafikiri sijamaliza.

**Com. Yano**: umemaliza wakati wako, endelea.

**Cllr. Yusuf Godana:** Okay wacha nikusomeshe kidogo, an kila Assembly pamoja na ma-local authorities yawe na speakers. Na ma-chairmen wa county coumcils, town councils, municipal councils, wawe wakichaguliwa na wananchi wa maeneo hayo moja kwa moja na wananchi wenyewe. Isipokuwa deputy mayors, deputy chairmen wa county councils na ma-chairmen wa ma-committee wachaguliwe na wale ma-councillors au wabunge wa mkoa.

Nikiguzia kidogo, nasema ya kwamba wale ambao wanafanya kazi nzuri sana na wanadharauliwa na kazi nzuri wanao fanya kama ma-headmen, kama hawa KPR, serikali iwahurumie KPR (Kenya Police Service.) Serikali iwahurumie, iwaweke katika pay roll angalau job group A, ili wawe wakipata chochote, wanapoteza wakati wao mwingi, wanapoteza usingizi wao, wanapoteza mambo yao, kutuhudumia sisi. Wanafanya kazi nzuri hata kuliko ma-chief na ma-sub-chief. Na hao walipwe from the regional consolidated funds. Walipwe mishahara yao from the regional consolidated fund, siyo national ni regional consolidated fund. Na kwamba 85% themanini na tano kwa mia ya mapato ya kila jimbo, yabaki kwa jimbo hilo kwa mambo yake. Mishahara, maendeleo na kila kitu, kumi na tano kwa mia iende Nairobi kwa serikali kuu. Na wafanyi kazi wa umma, themanini na tano kwa mia, Katiba ihakikishe ya kwamba ni lazima wawe ni wenyeji wa jimbo hilo, isipokuwa kumi na tano kwa mia, pengine, nimetunia neno pengine ikiwa ni lazima kumi na tano kwa mia wachukuliwe kutoka sehemu zingine za nchi, lakini themanini na tano iwe mandatory kwamba lazima watoke katika jimbo hilo, kwa sababu tayari themanini na tano kwa mia ya pesa za jimbo hilo zinabaki katika jimbo hilo.

Tuna watoto ambao wanakosa masomo kwa sababu ya uhaba wa mapato ya wazazi wao. Tunataka Katiba itunge, iweke vipengele ya kwamba watoto hawa wa secondary na college wawe wakielimishwa, halafu hata kama ni kudaiwa baada ya kuelimishwa wapewe kazi. Serikali ihakikishe imewapa kazi ili walipe pole pole pesa hizo kutokana na mishahara yao. Na hali kadhalika kwa wagonjwa ambao hawajajimdu, ogonjwa si kitu cha kualika, kwa hivyo wale wagonjwa pia wawe wakihurumiwa ipasavyo ili kwamba wawe wakitibiwa haswa na hospitali za umma ili waendelee kulijenga taifa hili.

Tunaazimia kwamba, ili kuendeleza elimu katika nchi nzima, kila mkoa at least uwe na university college moja, chuo kikuu kimoja. Badala ya vyuo vikuu vyote kurundikana pahali fulani, kila mkoa uwe na chuo kikuu kimoja, kila Jimbo for this matter, kila jimbo liwe na chuo kikuu kimoja. Tuna Mombasa polytechnic pale. Ile imetosha chuo na kubaki. Tayari kabisa hata hakuna haja ya marekebisho. That one qualifies to be a university; Mombasa polytechnic qualifies by itself hata bila marekebisho yoyote. Kwa hivyo, kwa haya machache naona pengine nimewaudhi sana Commissioners, wenzangu wataendelea.

Asante.

**Com. Yano:** tafadhali kuna swali tungetaka kukuuliza.

**Com. Maranga**: Nataka sijui kama umefikiria utueleze, ikiwa Rais ndiye anachaguliwa na watu directly, naye Prime Minister anachaguliwa na wabunge, ni sababu gani Rais awe ceremonial naye Prime Minister ndiye anakuwa na nguvu za serikali?

**Cllr. Godana:** Tunataka Rais awe ceremonial, awe kama baba wa mji, awe baba wa family, akae atoa mawaidha, sio kuongoza, waziri mkuu achukue pale pahali pa sasa ambapo panaitwa head of public service. Aendeleshe serikali, Rais akiona kosa anamuita kando, anamuambia hapa unaenda kombo, unaenda kombo Katiba kama hizi tunazo pahali pengi hapa katika

Bara la Africa na ambazo zimeridhisha. Na hata mawaziri, mawaziri wasitokane wa wabunge. Mbunge akichaguliwa abaki mbunge wa wale watu waliomchagua peke yake. Mawaziri watoke kwa huyu anajua sheria, haya mkuu wa sheria, ule anajua ukulima, waziri wa ukulima. Watu kutoka nje ya Bunge.

**Com. Yano:** Tafadhali kuna swali lingine, tafadhali Bwana Godana kuna swali lingine kutoka hapa. Swali lingine.

**Com. Kangu:** Mimi ningetaka kujua ni nguvu kiasi gani ungetaka kuipatia ile serikali ambayo ni ya majimbo ama ya regional ama serikali ya jimbo. Itakuwa na nguvu gani na ile ya serikali ambayo tunaita central government? Na wale wa local authorities watakuwa wanafanya nini? umefikiria hayo maneno pengine.?

**Cllr. Godana:** nguvu ambazo ningetaka kuachia serikali kuu, ni kama Judiciary iwe chini ya serikali kuu, Defense iwe chini ya serikali kuu, Public Service Commission iwe chini ya serikali kuu, lakini hayo mengine ya elimu, Social Services, Agriculture, Veterinary yabaki kwa Majimbo.

**Com. Yano**: Asante sana, inaonekana nyinyi watu wa Garsen mumechemka kabisa, mnaelewa hayo maneno kabisa. Tuendelee tafadhali. Mwenye anayefuata ni Tom Ali Bwora. Na tafadhali tunakupatia dakika tano tu.

**Tom Bwora:** Mimi kwa majina yangu naitwa Tom Bwora, na nimeokoka. Bwana Yesu asifiwe?

Congregation: (Amen)

Sisi ni the Professional Arm of the Church NCCK, kwa hivyo tunawakilisha mawazo ya kanisa. Kuna mambo ambayo nimengi ambayo tumeandika kama kanisa, lakini nitapitia tu, yale ambayo mngeweza kuyasikia. Kitu cha kwanza kuhusu vyama vya kisiasa, tungetaka kuwe na vyama vitano in order of merits i.e the number of M.Ps it has in Parliament. Vile vyama vitano vya kwanza, hivyo viwe funded, vipate usaidizi kutoka kwa serikali.

Kitu cha pili, kihusu uongozi au system of government, kama kanisa tunapendekeza tuwe na Rais na pia kuwe na waziri mkuu. Pia tuwe na ugawanyi wa madaraka kati ya Rais na huyu waziri mkuu. Lakini, waziri mkuu awe anahusika na day today running of the government. Na pia ahusike na utekelezaji wa maongozi ya serikali. Na pia tuweze kuwa na combination ya both President na Prime Minister na pia tuweze kuwa na mfumo wa serikali kuu. Tunasema hivi kwa sababu, tumeona tunaingia kwa misisimko, na serikali kuwa na serikali kuu si vibaya. Kwa sababu ile iliyoko, inatarajiwa kutekelezwa na kufanyiwa marekebisho hapa na pale. Lakini kuwe na serikali moja iliyo kuu (inaudible) hayo si makosa. Kwa hivyo kama kanisa tunasema tuwe na federal government, kwa sababu ikiwa tayari central government kuna mambo mengine ambayo hatuyaoni, je tukiwa na serikali ya hapa Mombasa, kutakuwa na mambo ambayo sisi wananchi yatakuja kutuudhi zaidi na zaidi. Kwa hivyo tunasema ile iliyoko irekebishwe, ili ikaweze kufanya kazi kwa kila mmoja.

Jambo lingine tunalolitaka, ni kuwa Bunge likaweze kuwa na mamlaka ya ku-summon na ku-sensor to summon and sensor Ministers. Kitu kingine tunataka wabunge wetu wafanye kazi, wasiwe idle. Kwa sababu tunaona kama mtu yuko idle anapata nafasi ya kuchochea hapa, anapata nafasi ya kufanya hivi, anapata nafasi ya kufanya hivi. Kwa hivyo, wabunge wetu siku hii ya leo kama kanisa tunasema wambunge hawafanyi kazi, tunawalipa mishahara ya bure, kwa hivyo tunataka Katiba yetu, wabunge waweze kufanya kazi kwa siku tano. Huwezi kulipa mtu nusu million kisha anafanya kazi kwa mchezo.

Kitu kingine, tunataka watu waweze kupewa uwezo wa kuwaitisha wabunge wao ambao hawafanyi kazi. Wabunge ambao wamewapotelea wananchi waliomchagua, ameenda Nairobi akapotelea huko. Tunataka Katiba yetu itupatie mamlaka ya kum-summon na kum-recall na ikiwezekana tumtoe.

Tafadhali ninapoenda kumaliza nitazungumza kuhusu freedom of worship, kanisa linataka hivi, zile societies ambazo zinakuwa registered kama makanisa, ziwe scrutinized kwa sababu zingine zinahusiana na mambo yanayo husiana na kishetani.

Ya pili, makanisa yapewe uwezo wa kutengeneza curricum au syllabus katika ma-shule.

Kitu cha tatu, makanisa na taasisi za elimu ambazo zilikuwa ziko chini ya makanisa, tunaitaji zilirudishwe kwa makanisa.

Kitu cha nne. Makanisa yaweze au mpango wa Pastoral Programme katika shule zetu, ziweze kusimamiwa vizuri na ziweze kutiliwa mkazo.

Kitu cha mwisho, ninapoenda kumaliza, tunasema kama kanisa, 8-4-4 system imetuaibisha, kwa hivyo tunataka mfumo ule wa zamani wa 7-4-2 uweze kurudishwa.

Kitu cha tatu, tunataka Parliamentary Committee on education iundwe katika Bunge ili liweze, ku-over see au kuonelea, kuona kuhusu mambo ya elimu na malipo ya waalimu. Maanake walimu hawalipwi kitu.

Kitu cha mwisho, tumesema hivi kama kanisa, wale walimu ambao ni non-graduates, hawa ndio ambao wanataka kulipwa zaidi. Wale ambao ni non-graduates, government, serikali iweze kuwapatia a scheme of service.

Asanteni sana.

**Com. Yano:** Asante sana, Bwana Tom. Mwenye anamfuata ni Buye Bonaya

**Buye Bonaya**: Kwa majina naitwa Buye Godana. Mimi nikiongozi wa vijana wa Taraza. Hii Memorandum nimeandika kwa

kizungu lakini nasikitika kwa wale ambao hawajui pengine kizungu hawataelewa, kutakuwa na watu ambao wakuwa wana-translate kwao. Na mimi nitaisoma moja kwa moja.

Defense and National Security: The Armed forces should be different from the political wing. The President should not be the Commander In Chief of the Armed forces. Parliament should not be involved in declaring war. The Constitution should empower armed forces to extra- ordinary powers in emergency situations like war, national disaster and break down of public order.

Tuje katika upande wa political parties: Only two political parties to be registered that is the ruling party and the opposition party, and should be equally financed by public funds. Political parties should not be financed by individuals on condition that each party should have a bank account to be monitored by the Central bank, this will ensure transparency. The opposition must have a shadow cabinet to work closely with the said cabinet.

Tuje kwa Structure and System of Government: The present system of government should be maintained and Parliamentary system of government in which a Prime Minister is appointed from the opposition side.

The President should not be above the law.

The President should be the appointing authority on condition that all appointments are based on professional career through the approval of Parliament.

Appointments should be based on national outlook, kwa sababu tunaona saa hii, unaona kabila moja peke yake ndiyo inarundikana katika ofisi nyingi za Nairobi. Ukiangalia unaona ni kabila moja au kabila mbili na yale makabila mengine pengine yamesahauliwa. Sasa, wakati huu tunataka kila kabila liakilishwe katika zile ofisi za Nairobi pia. Nitaenda tu pole pole.

**Com. Yano**: Nafikiri pengine nitakukata.

**Buye Bonaya:** Sasa kwa Legislature; Being an MP should be by part time. Minimum educational qualification for MPs and President should be set. A person to contest should have at least a first degree. A person contesting for Presidency should at least serve as a governor for five years.

Moral and Ethical qualification for Presidential and Parliamentary on the candidate should be introduced. People should have a right to call for the attention

**Com. Yano:** tafadhalini tumpe mda aongee, pia nyinyi tutawapa nafasi yenu.

**Buye Bonaya:** People should have a right to re-call their MP, a half of the people in the constituencies can write to the Speaker of the National Assembly giving their complains and demand on petition in the High Court. MPs should act on instructions from their constituency. An independent Parliamentary Service Commission should determine the salary and benefits of the MP and it should have a wide representation.

**Com. Kangu:** Maliza kwanza.

**Buya Bonaya:** Seats for nominated MPs should be divided to disabled, women, trade unions, (inaudible) youth, civil servants, NGOs and religious groups. There should be two chambers of Parliament, house of representative and senate to care of regional, provincial, (inaudible) and checks on the decision passed by the Legislative and Executive. We should structure election for Parliament by having elections for MPs and Senate held at different times while Presidential and Senate elections should be held differently from that of MPs and Councillors.

**Com. Yano**: Asante sana Bwana Buye Bonaya, mwenye anayemfuata ni Samuel Bonaya.

**Samuel Bonaya:** Kwa jina naitwa Samuel Bonaya. Nitazungumza kingereza, but just before I present my views it is important to note that, every thing runs according to principle, the universe, the laws governing the universe and everything runs according to principles. Similarly, the Constitution should run according to principles of democracy. In deed the word democracy comes from two words, demos-cracy. Demos mean people, cracy-government by the people. So the Constitution is very important in regulating the activities of the various organs and the systems of a country. A Constitution with good regulatory mechanism should provide an environment that enhances political stability, financial soundness and social soundness. Such a Constitution should have organs, systems and mechanisms that provide positive counteractive activities to stop the negative activites that poison the ideal environment for the thriving of the economy. Hence, there is need of putting regulatory mechanisms in the Institutions of Presidecy,

the Judiciary and National Assemblies, so that the combined effects of the activities of this institutions can create an ideal environment for optimum economic growth, social soundness, peace, stability, prosperity. A good Constitution will enhance the rights of the citizens. Enhancing the rights of the citizen's means giving a chance to exercise their democratic rights in participating in government, e.g the word democracy comes from the rootword demos and cracy. Demos means people, cracy means government that is government by the people. The regional government system brings the people closer and the government closer to the people. It enables the people in the regions to fomulate laws that will protect the rights of the people and region e.g when the region has properly instituted land laws. There will be proper laid guidelines on transactions involving land.

Regionalism also affords the people of the region to plan the development of their resources for the good of those who are in

the region, or those who come to stay in the region, so that task of resources is distributed between the region and the central government. We suggest a Constitution of Presidential system with a President, a deputy President and 8 Vice Presidents from the regions. We suggest the President or a member of the cabinet should not be a parlimentarian. We suggest that the President should be voted directly by the people. We suggest that the duties of the Parliamentarian should strictly be in Parliament. The Parliamentary committee should be formed in line with Constitutional Government Ministries. That each Parliamentary Committee be involved in formulating policy guidelines for the ministry and its overseer. Sorry.

Parlianmetary Committee to approve or reject Presidential appointment of secretary, minister incharge of ministry, Parliamentary committees to serve as the watch dog of the people. To see to it that the ministry is serving the people efficiently. Parliamentary committee to have a system of conducting both financial and technical audit operations on ministries and its charge. For technical audit of work, the Parliamentary committee to get technical advice and clearly defined procedures of conducting such audit. Parliametarians to be involved in Parliamentary business on everyday prices because they roles are equal. Tafadhali nipatie dakika tano.

A successful regional Parliamentarian will have region committees on miniature model frame. We suggest regional Parliaments that will have regional committees on miniature model similar to National Parliament. We suggest the President should be obligated by the Constitution to ensure the following inperformance of his duties, to ensure all governement ministries are running efficiently without corruption, to safeguard the democratic right of every Kenyan. To perform its duties ethically according to the requirements of the Constituion. To ensure that government officers are performing their duties without corruption, efficiently and with dedication. To ensure that citizens get their rights at the right time without being molested. Duty to ensure police officers, judges and government officials don't get involved in corruption. Duties to know that he as President, is under the Constitution, not above it.

We suggest that the activities of all ministires including Judiciary, defense and internal security, actually should be regulated by the appropriate Parliamentary Committee.

Finally on religious worship: Freedom of religious worship I would like to take note, that in taking the decision of the NCCK or whatever other movement, it is important to take the historical basis of the existing culture of 325 AD, where may be the catholic system was based on Trinitarian basis of worship. Anybody according to the ethics, it may be important to go to that according to the ethics of the Audosers. The Audosers after concept is everybody who is not a Trinitarian every church assembly that is not an Trinitarian in basis has not right of being called a church or a hieracy, so it is important (intejection) let me, please, one minute please. It is important and it will start the Audossers that caused the massacres of very many people and it brought into a census a system of religion --- (interjection)

**Com. Yano**: Are those part of your views?

**Samuel Bonaya:** Yes, views yes, part of my views because it is important that _____

**Com. Yano:** what do you want over religion?

**Samuel Bonaya:** yes religion as much as possible to have freedom of worship, to practice as long as one is within the combines of the Constitution.

**Com. Yano:** Thank you very much Samuel, I think I said very clearly. Huu ni wakati wa kupatiana maoni tafadhali don't go into the history of everything, kazi yako ni kama umeandika maoni yako, guzia zile sehemu ungefikiria wewe mwenyewe ungetaka tujue tukiwa hapa. Mkisha tupatia ripoti yenu ama Memorandum yenu, kazi yetu kama wana Tume ni kwenda kuketi natutaisoma na tuifanyie kazi vyenye tunatakikana kuifanyia kazi vilivyo. So tafadhalini ukikuja hapa chukua mda mfupi. Jaribu ili upatie pia mwenzako apate kupatiana maoni yake. Tunaelewana hapo? Na uguzia yake maneno, hapana patiana maneno mengi, kama ni maoni sema ni haya, na haya, na haya. Mwenye anayemfuata ni Ghuyo Biesa. Yuko hapa?

**Ghuyo Biesa:** Asante sana bibi mwenye kiti. Kama mlivyo sikia naitwa Ghuyo Biesa. Nimekuja hapa kwa point mbili tu, ambazo ni fupi, nazo zimehusiana na haki ya mtu. Niko na point ambayo najaribu kuisikia ya kama mtu ambaye kwamba amekamatwa, atapelekwa kotini kwa kesi, mtu kama huyo ilikuwa ni maoni yetu ya kwamba lazima aandike statement. Ile statement mtu kama huyo angeruhusiwa kuiandika mwenyewe binafsi au maanake wakenya wengi sasa washapata katika hali yakuweza kujiandikia, ikiwa hayuko katika nafasi ya kuweza kujiandia, mtu kama huyo angeruhusiwa kuchagua yule ambaye atakaye muandikia statement kama hiyo. Kwa sababu tumechoka na yale mambo ya polisi ya kuandikiwa, halafu baada ya kuandikiwa unaambiwa tia sign hapa, hujui unatia sign kitu gani. Kumbe ni mamba ya kuenda kukuzamisha, kwa hivyo inastahili mtu ajiandikie mwenyewe, na ikiwa hawezi kuandika mwenyewe achague yule atakayemuandikia kwa sababu atakuwa na uhakika kwamba anaandikiwa kitu gani.

Point ya pili, hali ya makesi vile vile, kuna hizi form ambazo wanaziita P3's. Ilikuwa ni maoni yetu kwamba form kama hizo, zingepelekwa huko hospitali. Zikakaa kule ma-hospitalini kwa sababu kule kukaa kwake polisi, zinatuletea matatizo ya kwamba hao polisi wenyewe wamekuwa ndio wanaotupiga na kutuumiza, na wakati unapoenda kule, ni sawa sawa na kesi kuichukua kwa tumbili uende ukaishtaki kwa nyani, huwezi kutoka hapo, huwezi kupata haki. Unakuta zile forms zinafichwa, unazitafuta huzipati, unaambiwa zimekwisha kidogo, nenda hospitali daktari aka-recommend. Ukienda hospitali daktari ana kuuliza forms ziko wapi, polisi huzipati, kule hospitali haziwekwi. Kwa hivyo unajikuta una yamba yamba hapa katikati mwisho ile hali ya kuenda ku-claim, kijitafutia haki yako unaikosa. Lakini kama zile forms zinakaa hospitali ukisha kuumizwa huku hata ikiwa ni polisi amekuumiza, ukimbilie kule hospitali, unakuta daktari, anakuhudumia, unajaza zile forms halafu unazipewa sasa inakuwa ni kuchukua ile hatua. Maoni yangu ni hayo tu.

Asante sana.

**Com. Yano**: Asante sana Bwana Ghuyo, yule anayemfuata ni David Gilo.

**David Gilo**: Asanteni sana. Nafikiri yangu si mengi kwa vile yameshazungumzwa na watu wengi hapa. Lakini nilikuwa nataka kuguzia kitu kingine kidogo, kama huu mpango wa ma-land. Mpango wa ma-land ni kwamba kuna watu wengi sana ambao wakiwa wamekubaliwa kukaa mahali, wana-change hata majina ya pale mahali. Wanaondoa jina la zamani wanaweka jina lao na baadaye wanalifanya kuwa hapo mahali ni pao na hawawezi kuondoka tena, na hatimaye fujo inatokea kukawa na clashes.

Kuna sehemu ingine, jambo la pili ni kwamba, kuna hii habari ya kutembea hapa na pale katika areas ambazo kwamba hizo zina wenyewe kabisa, yaani ni owners of the place. Lakini watu wengine wana-abuse wapenda kukanyaga kanyaga na hawafikirii kwamba ile area ni ya ancestors ambao kwamba ndio walikuwa wenyewe wa hayo mashamba.

Jambo la tatu. Kuna huu mpango wa health, watu wa afya. Watu wa afya wanaaminiwa na serikali kwamba wao ni watu wa kuchunga afya ya wananchi. Na hali wanapochunga hali wananchi nashangaa sana kwa jambo lile ambalo lilikuwa limetoa ama lilitolewa kama amri. Lakini si sheira ni amri kwamba hii pombe ya kienyeji haina ruhusa ya kutumika, lakini ifanywe amri si sheria. Lakini yasemekana pombe ya kienyeji isitumike. Ilisemekana ni pombe haramu, polisi waliandika kama pombe haramu. Wakiandika pombe haramu hatujui ni pombe gani ambayo Mungu amehalalisha, na Mungu haalalishi pombe yoyote. Kwa hivyo hili jambo la pombe haramu liondolewe. Lakini kwa ufupi nitanyamazia hapo, maanake mengi nimeyaandika. Asante.

**Com. Yano:** Asante sana Bwana Gilo. Yule anayemfuata ni Reverend Richard Yalo Abio.

**Reverend Richard Yalo Abio**: Majina yangu ni Reverend Richard Yalo Abio. Nafanya kazi na Methodist Church in Kenya. Yale mengi nimeandika yameongewa na ninatiaka kuongea machache. Kusajiliwa kwa makanisa. Ningependekeza kwamba makanisa yasajiliwe ku-avoid cult and devil worshipping kwa kutumia ratiba ya ku-fall under the doctrine of Trinity.

Jambo lingine, nataka kuongea kuhusu ufisadi. Kenya tunayo mali nyingi sana, nchi tajiri kama hii sijaiona lakini kwa sababu ya ufisadi hatuendelei. Na wengi wanaofanya ufisadi wengine wao ni viongozi maarufu wa serikali.

Pia ningeomba ofisi ya Judiciary ipewe mamlaka kukamata watu wa ufisadi kama hao.

Jambo lingine, ningependa kuongea ni kuhusu uchaguzi, election. Kuwa ethmetical leaders wawe involved katika hali ya uchaguzi kwa sababu ya kuepuka kutumia nguvu kupitisha wengine ambao wanataka wenyewe, so ningeombe ethimetical leaders wawe considered the elections. Hayo tu ndio niko nayo yale mengine yote yako hapa nimeyaandika. Asanteni.

**Com. Yano**: Asante sana Reverend Richard Abio, mwenye anamfuata ni Abaloni Racha Abaloni, Abaloni Racha Abaloni. Abaroba Barisa Abakoba, Maria Kopesa. Kama ulikuwa umeongea tafadhali hatutakuhurusu uongee, tafadhali patia mda mwenzako. Kama ni ku-submit Memorandum submit it.

Asante.

Omara Abaye Karasinga.

**Omara Abaye Karasinga**: Madam chairperson. Mimi naitwa Omara Abaye Karasinga na la kwanza nataka kuondoa kisha nijalize yale mapendekezo yanayohusiana na serikali ya majimbo. Kwanza katika serikali ya Majimbo, tunapendekeza ya kwamba President atachaguliwa na chama lakini atakuwa na running mate, na hakutakuwa na Prime Minister kulingana na serikali yetu ya majimbo. Wizara katika regional government zitakuwa nane. Wizara kule central government ambazo zitakuwa pamoja na President zitakuwa Foreign Affairs na Judiciary ambayo ni under the Attorney General plus defense. Hayo ni mabadiliko kidogo na tutakuwa na bi-cameral Parliament. Senate ambayo ni upper house na house of representative. Katika hapa ngazi ya regional government, tutakuwa na regional members of Parliament ambao watachaguliwa kulingana na zile taratibu. Na vile vile ningetaka kuongeza ya kwamba ikiwa hii system itakubalika, tunataka kuongeza majimbo kama Rift Valley itagawanywa mara mbili, maanake ni kubwa mno.

Number two, kuhusiana na vyama vya kisiasa. Madam Chairlady, Kenya bado haija-involve philosophy au ideology, bado kuna vyama arubaini na vinane ambavyo havina mpangilio, bado havina philosophy. Kwa hivyo nime-recommend hapa vyama vitano, kulingana na zile trends tuko nazo katika Kenya wakati huu. Kwanza labour party, kulingana na strong labour movement ambayo ilikuwa Kenya, hawa akina (inaudible).

Pili, Democratic Party, wale ambao wanaamini wao ya kwamba wanataka democracy in Kenya.

Tatu, wale kama sisi ambao tunajiita federal, ambao tunazingatia mifumo ya majimbo.

Nne, wale New KANU, wale wanajiita New KANU hao ni those ambao wamekuwa convinced of the Unitary System of Governance.

Tano, Ni wale ambao wanafikiria jinsi ya mazingara yao yatakuwa vipi. The green movement. The green, green,green kwa hivyo nimezigawanya vyama vya kisiasa namna hio na ningetaka vihifadhiliwe na serikali kuu. Vile vile ningetaka visajiliwe, viwekwe katika Electoral Commission. Kuwe na Director of Elections under the Electoral Commission, ili aweze kuangalia adabu, na mipangilio na vyama visivunjwe ovyo ovyo maanake tabia ilioko Kenya ukipiga makelele unafutwa siku ya pili. Mambo kama hayo serikali na vyama viwe ni vitu tofauti.

Ningetaka vile vile kuguzia maneno ambayo hayajaguzwa hapa. Hatukua na mkataba Kenya, sijakumbuka popote niliposoma kwamba tulikuwa na mkataba wowote stadi, kuhusu mwambao wa Pwani na serikali tuliyoridhi, maanake mwamba wa Pwani ulikuwa ni tofauti, na serikali ya Kenya ilikuwa ni tofauti. Namna vilivyo unganishwa mpaka leo ni tatanishi kubwa sana, Katiba ijitokeze wazi wazi. Itambue wale waliokuweko katika mwamba huu wa Kenya wakati ule, ya kwamba ndio wenye ardhi wakati huo. Maanake ardhi ilikuwa na Title Deed wakati huo, kila kitu kilipangwa namna yake wakati huo na leo tunaona watu tu kiolela wanaenda kuchua ardhi za white land bila madhumuni yoyote, mara utausikia hii ploti ni ardhi ya serikali, mambo yanakwenda namna hio. Kwa hivyo Madam Chairperson tunapendekeza, kwamba ikiwa kulikuwa na mkataba wowote sisi hatujautambua na hatuujui na hujulikani na wale ambao wako mwambao huu wa Pwani. Na tungetaka awe-revisited na ardhi iwe trust land belonging to the people of that area.

Number tatu, mazingara yamekuwa tishio kubwa. Mungu ameweka mazingara kwa sababu zake, ili kumlisha mwanadamu kwa njia tofauti tofauti. Lakini kinachoendelea Kenya leo na Katiba iliyoko hivi sasa haija taja kikamilifu kuhusiana na namna ya mazingara yatakavyo kuwa. Moja, nimezungumzia tu trust land tena kitu kidogo mle ndani.

Pili, pengine nitaguzia juu ya wild life, basi. Lakini haikuguzia maneno ya mito, leo mto wa Uasonyiro unakauka, mto wa Tana River unakauka kwa ajili ya watu wanakata misitu kiholela kila pahali, hakuna chochote kilichoko kwenye Katiba. Tunataka mazingara yawemo kwenya Katiba, kwa mfano, hapa tunasema tunataka kuwe na River Basin, Tana River Basin Authority ianzie Mt. Kenya ishuke hapa, iko-control huu mto peke yake. Kama vile mwaka wa 1926 River Nile ilikuwa na River Nile treaty with Kenya, kwa nini hatuwezi kuwa na treaty maanake watu wa Mt. Kenya wanaharibu mito wanavyotaka, watu wa Embu wanafanya wanavyo taka, wanaweka ma-dam ya electricity na huku hata spark hatuna na huku mto unakauka hatuna samaki, hatuna mpunga hatuna nini, watu wafugaji na wakulima wanapigana.

Madam Chairlady, bahari yetu, hakujakuwa na sheria kikamilifu kuhusiana an mambo ya bahari, na tungetaka Katiba hii iangalie uharibifu unaoendelea katika bahari. Reefs, samaki maanake ni source kubwa ya chakula ya watu wa Pwani, na ikiachiliwa kiholela maisha ya watu wa Pwani yataangamia.

Tungetaka vile vile, hali tunaangalia maneno ya hizo sheria ambazo zinahusiana na maneno ya bahari pamoja na mali rasmi. Mwenzangu alikuja hapa akaguzia maneno ya Gypsum kwa mfano, leo tuna titanium na kuna habari kamilifu
Kwamba Tana Delta kuna na gas, natural gas, that is automatic and it has already been established. Na tunaambiwa katika Katiba foot sita chini ya ardhi ndio mali yako wewe mwananchi, zaidi ya hapo huna chako ni mali ya serikali. Serikali ni nini? Tunataka Katiba ieleze serikali ni kitu gani? Maanake ikiwa serikali hakuna mtu hakuna serikali. Serikali ni wale, watu maanake bila watu hakuna serikali, tungetaka ile mali rasmi hata ikiwa nchi au foot mia moja iwe, hata ikiwa ilikuwa mali ya serikali lakini ni nusu kwa nusu, kati ya ile serikali na yule mwananchi. Asanteni.

**Com. Yano:** Kuna swali hapa tafadhali.

**Com. Kangu:** Bwana Karasinga umeguzia mali ikifika kiwango fulani chini inakuwa ya serikali na unauliza serikali ni nani, ikiwa tunatengeneza Katiba yakusema sasa tumeweka utaratibu wa kuhakikisha serikali ni watu wenyewe, kutakuwa na makosa gani kusema hiyo mali ni ya serikali, ikiwa nyinyi wenyewe ndio serikali?

La pili, umesema tuwe na Senate na house of representatives. Sijui kama umefikiria Senate itakuwa na wabunge wangapi na watachaguliwa kwa njia gani, wana-represent sehemu gani? La pili, hiyo Senate kikao chake kitakua wapi? Kwa sababu saa hii tunazungumza vitu vyote vimewekwa Nairobi, tena tuanze Senate tuweke Nairobi ama tuweke hiyo Mombasa?

**Karasinga:** inatokana na Mbunge mmoja kwa kila district. Senate ni wabunge wazee wazee, ambao wanakaa kuangalia kwamba yale yanayofanywa na house of representative ni sawa. Wanayatambua kisha wanaregesha, kwa hivyo, senate itakaa pale ambapo, inaweza ku-move, mara hii itakuwa Pwani, mara hii itakuwa wapi, si lazima iwe pahali pamoja. Lakini house of representatives ni hawa hawa members of parliament, ni haya haya maeneo ambayo yako katika Katiba wakati huu. Hao watakaa kule kule Nairobi. Na Regional Assemblies ni hao watakao chaguliwa kulingana pengine na division, ndio watakao kuwa katika regional assemblies na kutakuwa governor, ndiye atakaye wasimamia hao members of regional assemblies. Hii imetokana na hali ambayo mali rasmi ya nchi hii haijagawanywa ki sawa.

Number tw, kulingana na hiyo mali rasmi, mapendekezo ni kwamba tutambue ni nani serikali. Ikiwa tumeshatambua katika Katiba kwamba serikali ni mwananchi, basi huyo mwananchi asimamie mali yake rasmi.

**Com. Yano:** bado kuna swali hapa tafadhali.

**Com. Maranga**: Bwana Karasinga, umesema tuwe na vyama vitano, kulingana na miongozo ya vile watu wanavyosema, kwa mfano, wafanyi kazi, labour party, democratic party namna hio, sasa mimi nakuuliza Bwana Omara Karasinga, wewe ni mwana Kenya ambaye umepigania kabisa watu wawe na uhuru, wakushiriki katika mambo yao vile wanavyotaka. Sasa ukiwekea watu mpaka wa vyama vitano, si nikunyima wengine ile haki ya kushirikiana vile wanavyotaka Hilo ni swali moja.

La pili, huwezi ukapeana uhuru kwa kushiriki katika mambo mbali mbali halafu tena unaweka mipaka. Huoni hapo unaitilafiana na Katiba. Kitu cha pili, ningekuuliza kuhusu haya maneno ya agreement kati ya serikali kuu ama central government na unavyo sema hakukua na mkataba wowote kati ya mkoa wa Pwani na ile serikali ya Nairobi tuseme. Sasa tunauliza je, wewe kama Omara Karasinga unafikiria umoja wa kitaifa? Je, unajisikia watu wa Pwani ni watu wa Kenya ama ni nchi gani?

**Omara Karasinga**: La kwanza, kuhusiana na vyama hakuna nchi, sijajua katika nchi ambazo zinaendelea kama ziko na vyama vingi kama Kenya. Maanake ukienda Germany ni SDP, sijui ni kama vyama vitatu hivi. Ukienda Ulaya America utasikia ni

vyama viwili, na zile ndizo democracies ambazo zinatushinda sisi. Kulingana na ninii, chama ni philosofia chama ni maadili na wanakenya sasa ingawa walipewa uhuru wa kuanzisha hivyo vyama vyote, leo unasikia merger. Hiyo siasa sasa inakuja, kesho unasikia Alliance inameza vyama fulani, kesho kutwa utasikia mmm na hiyo ni kawaida katika historia ya development of political parties hizi ni stages. Tunaanza na wingi, tunashuka mpaka mwisho tunabakia na vyama vichache, viwili, titatu, vinne, siyo kwamba watu wamenyimwa lakini ningependa ku-suggest ya kwamba, watu waongozwe. Kukubaliana na aina fulani fulani ya falsafa na hizi ambazo nimezitaja hapa ndizo falsafa ambazo sasa zimejitokeza katika Kenya. Kuna wale ambao ni merger, the merger politics ambao wanaamini kwamba wao dhati, unitary system of govenment, kuna wale kama sisi ambao tumeamini ni majimbo na nikisema mimi ni majimbo kukujibu lile swala lako lingine, mimi ni mwana Kenya ninayeishi Pwani, kwa hivyo nimeamini kwamba mali yangu rasmi iliyoko Pwani, haijatumika kikamilifu kunifanya, kuniwezesha mimi kuwa mtu. Ni kwa sababu hiyo, tunasema ya kwamba tukipata serikali yetu ya majimbo wale ambao wako hapa hivi sasa wataamua either watakuwa Pwani, watakuwa na vitambulisho vyao vya Pwani ama watakuwa somewhere else. Maana yake ni kwamba, watu uingia hapa kwa masilahi yao na kutoka. Kwa hivyo katika historia hii ambao Pwani ina historia ndefu zaidi, kushinda mkoa wowote, nadhani tumekubaliana hilo. Because of our history, because of our origin, we have never been respected the way we are, hatuna National Schools, hatuna university, hatuna chochote, na ni kwa ajili hio tunasema ya kwamba, serikali sasa iwe ya majimbo ili na sisi tuanze university yetu, kulingana na mali rasmi yetu. Ili na sisi tuanzishe college zetu, zile colleges sisi tutazianzisha ni tofauti na zile zingine, tertiary colleges ni lazima ziambatane na mali rasmi yetu. Sio kuanzisha polytechnic, ni kuanzisha a fishering college ambayo ita-train watu juu ya nyafu na juu ya kumshika samaki. Those are the kind of rudimentally, technical colleges za kumpatia nguvu mbili yule mwanachi anaye elewa hapa ili aondoe umasikini wake. Na ni kwa ajili hio ni rahisi zaidi sisi kuji-manage katika regional aspects. Na ndio maana nika-suggest, na mimi niko strong and a I have vowed federalist. Nimeamini huku kwamba Cental Province, sisemi wakikuyu wanaoishi Central Province sio wakikuyu peke yake, North Eastern Province ina mali rasmi wanaweza kutegemea. Yule atakaye ajiriwa hapa, watu wa hapa wataamua mshahara wao, hakutakua na matatizo kama hapa KUT demanding so much money, no, kila jimbo litaamua mshahara wao kulingana na mali yao. North Eastern wataamua mshahara wao, kulingana na mali yao. Kila watu wataamua mshahara wao hata ikiwa ni shilingi mia mbili, mia tatu.

**Com. Yano:** Asante sana, Bwana Karasinga. Tafadhali enda ujiandikishe na pia utupatie hiyo Memorandum yako. Sasa tuko na Bashora Gathu.

**Bashora Gathu**: Madam Chairlady, Makamishena’s, wakenya wenzangu, hamjamboni? Kwa majina naitwa Omar Bashora Gathu, napeana mchango wangu kama ifuatavyo. Niko na sehemu tatu, sehemu ya kwanza ni kuhusu marekebisho, huu mswaada wenyewe tayari nimeona uko na kasoro.

Sehemu ya pili, muongozo ambao umependekezwa na Tume ya Marekebisho ya Katiba tayari ina sehemu ya kurekebishwa. Halafu tatu nipeane kama nafasi itaniruhusu ule mchango wangu. Mswaada unasema marekebisho juu ya Katiba, lakini mimi nasema si sawa. Sawa ingekuwa matayarisho rasmi ya Katiba ya Kenya, kwa sababu ya kwamba hutukuweko na Katiba

ambayo wakenya tuliitayarisha wenyewe kutoka kwa ngazi za mashinani, hatukuielewa, haikuweza kushughulikia masilahi kadhaa ya kiuchumi ya kiusalama, pamoja na kuusisha jamii zote za wanyonge wale wachache, nikipeana mfano kuna watu tunawaita Wata, hao ni watu wa Tana River, wanakaa Biliza hata assistant chief hawana, hawana hospitali, hawana shule. Kwa hivyo, tunaweza kusema kwamba ile Katiba ilikuweko haikuwa Katiba rasmi yetu ya Kenya. Ilikuwa Katiba ambayo imeombwa, imekuwa-borrowed, au imeibwa, hatuijui, kwa sababu hiyo hatujui, hatuwezi kurekebisha kitu ambacho hatujui.

Sababu ya pili yakusema kwa nini tusiweze kujadili mambo ya kurekebisha Katiba ni kuwa hatuku ___. (end of tape)

Jambo la tatu ambalo nimesema hatungeweza kuzungumzia mswaada wa kurekebisha Katiba mbali matayarisho ya Katiba rasmi ya Kenya ni kuwa ni mda mrefu sana umepita kutoka tulipopata uhuru, bila kuwa hatujui wala hatukushiriki katika Katiba hio. Kiasi cha kwamba saa hizi mambo mengi, yamepita sasa tunaona wakenya tunakabiliwa na matatizo na Katiba iliyoko haiwezi kutusaidia. Kwa sababu hiyo ndio nimesema ya kwamba mswaada uwe matayarisho rasmi ya Katiba ya Kenya. Ndipo baadaye Katiba hii ya sasa ambayo tutaweza kuitayarisha, mda utakaopita tuna haki ya kuirekebisha kwa sababu tumeitengeneza wenyewe.

Sehemu ya pili ambayo nimeona ina umuhimu pia vile vile, yataka pia vile vile kurekebishwa, ni muongozo ambao umepeanwa na Tume ya Marekebisho ya Katiba. Ukipewa kijitabu hiki, katika sehemu ya saba, wametaja taratibu maalumu ambazo wamezifuatia. Baada ya maoni yote kupokelewa katika ngazi zote, kutakuweko na mkutano wa kitaifa. Ambao wenye kujadilia maoni yote nikimaanisha kwamba wao wataweza kuwa wamepokea maoni, wametayarisha kila kitu, na wakaja na mapendekezo ya maoni vile yamekuweko. Kwa hivyo watu wataenda kujadili. Wakaweka taratibu kwamba kutakuweko na watu watatu wa kila wilaya, mimi nasema hiyo ni very unfair kwa sababu kama vile mnavyoona kuna wilaya zingine ambazo ni kubwa sana. Kuna wilaya zingine ambazo zimegawanyishwa karibu mara tatu, mara nne, na Tana River hasa katika mkoa wa Pwani ndiyo wilaya kubwa zaidi. Ikiwa tutapewa watu watatu tumeonewa. Kwa hivyo nimeona hapo panahitaji marekebisho, mimi ningeona kwamba at lease watu wangechaguliwa kulingana na wilaya ilivyo. Watu wa Tana River tupewe zaidi ya nafasi tatu mpaka kumi napendekeza mimi au mwasema aje?

Halafu, kitu kingine waliotaja hapa, kuna watu ambao Tume imejipa uwezo wa kuwachagua. Watu wakiweko ni mashirika yasiokuwa ya serikali, viongozi wa dini, mimi nasema sivyo hapana. Uwezo wa kuwachagua watu wengine ambao wangeweza kuenda kuhudhuria mkutano wa kitaifa uwachiwe wananchi, kwa sababu gani? Tume hiyo yenyewe sisi wenyewe wananchi hatukuweza kuichagua katika ngazi ya mashinani. Hiyo ni Tume ambayo imechaguliwa na walio ichagua kwa masilahi pengine ambao wanajua wao. Kwa sababu hiyo haitaweza kutuchagulia mtu ambaye sisi wenyewe tuna imani kuwa pengine uenda akawasilisha au akajadili yale maoni ambayo tumepeana. Kwa hivyo, baadhi ya maoni yangu ambayo yako hapa nikuhusiana na - - mengi yamejadiliwa nitagusia tu.

Natural Resources: Wameongea ya kutosha isipokua kwamba mimi ningependelea kusema kwamba zile sheria ambazo

zinahusu baadhi ya mashirika ambayo yanasimamia uhifadhi wa mazingira kama National Parks, National Reserves, ziko na ma-resources, mali rasmi ya wananchi. Tunasema kwamba sheria, policies, Katiba hii ibadilishe kwamba zimpe uwezo na nguvu mwananchi pale alipo apate kutumia na kunufaika sehemu zile. Kwa sababu sehemu ya sasa policy mwananchi katika reserve au katika park, hawezi kuingia ijapokuwa aweke hata mzinga wa kuchukua asali. Na hawezi kuumiza yale mazingira ambayo yako pale, kwa hivyo nafikiri yale mengine nitaweza kuwasilisha baadaye na maombi naomba kwenu, tafadhali nitawapatia anwani mnitumie rasmi baadhi ya maelezo yote kuhusiana na taratibu zenu, vitabu vingine nimezipata. Nataka kuakilisha rasmi, constructively, a written document katika mswaada huu wa kutayarisha marekebisho ya Katiba. Asante.

**Com. Yano:** Asante sana isipokuwa kuna swali mwenzangu angetaka kukuuliza.

**Com. Kangu**: Kuna mambo umeguzia kuhusu utaratibu wa kurekebisha Katiba, ingawaje mswaada unasema tunarekebisha Katiba iliyoko, kwa upande wetu hatuoni hilo jambo kama linatuzuia sisi wakenya kuandikisha Katiba mpya bila kusema tunarekebisha ile.

Jambo la pili, umeguzia vile mkutano wa kitaifa utatengenezwa na wale watakuwa huko, hayo sisi hatuna la kufanya kwa sababu ni vile yalipitishwa na Bunge, ikasema kila wilaya itakua na watu watatu, kwa hivyo hatuwezi kurekebisha hilo sisi wenyewe hilo ni Bunge iliamua, lakini tutajaribu kutafuta mbinu za kuhakikisha watu wenyewe wanahusishwa kwa kuangalia ni watu gani wanaenda huko. Lakini ningependelea kukueleza kwamba tumekuwa tukisikiza watu wengi na sisi tuko kati kati ya maneno, itakua kazi yetu kuamua mambo magumu kabisa, kwa sababu vile unasema mkoa wenu ni mkubwa sana ama wilaya yenu ni kubwa, kuna kwingine tumeambiwa hata mambo ya Bunge yawe yanaangalia watu, yasiangalie size ya wilaya. Wengine wetu tukasema hatuwezi kufanya hivyo kwa sababu kwingine mtu anaweza akapate kura ya watu elfu kumi kwa siku moja kwa sababu wako mahali pamoja, lakini hapa kwenu itachukua siku kadhaa ndio upate pengine hata kura elfu moja. Kwa sababu kufikia watu ni ngumu, so tuko kati kati ya maneno magumu, si rahisi vile unavyofikiria, kwa sababu saa hii kila mtu nasikia anatuambia tunataka serikali ya mfumo wa Majimbo. Na kuna kwingine tunaambiwa hatutaki hiyo hata kidogo. Siunaona tuko na kazi ngumu, lakini wakati wakuamua. Si ni kweli?

**Audience:** ndio.

**Com. Kangu:** sawa sawa.

**Com. Yano**: Asante sana, wakati huu si wakati wa maswali, ni wakati wa kuchukua maoni yenu. Mwenye anayefuata ni Ismael G. Dalla.

**Ismael Godana Dalla:** Kwa jina naitwa Ismael Godana Dalla, na mimi nimetoka katika jamii ya wafugaji. Kabla sijawapatia maoni yangu, ningelipenda kuuliza Commissioners watufafanulie, kwamba baada ya kuchukua wale watu watatu ambao

watakuwa kwa conference, tuliambiwa kwamba watakuja kuchukua tene sijui 25% ya wale watu ambao tayari wamekua appointed, kwenda kufanya conference huko. Kisha walisema hiyo 25% itakuwa ni representatives wa watu ambao kwamba either watakuwa marginalized ama hawakuweza kuwakilishwa kwa sababu ya uchache wao katika wale watu watatu, ambao kuwa wamekuwa appointed, waenda kule kwa conference. Tafadhali kama nikimaliza muweze kutufafanulia na pengine mtafuatia criteria gani, mtaweza kufikia wale ambao kwamba pengine hawajaweza kufikiwa a wakati wale watatu wakutoka kwa kila district wamechaguliwa.

Mchango wangu ni hivi, kwanza nitaanza na utangulizi: Ningelipenda Katiba ya Kenya ikuwe na utangulizi, kwa sababu ikiwa hakuna utangulizi ni kama mnyama mwenye hana kichwa. Itatambuliwa kwamba hii Katiba ina utangulizi na huu utangulizi umeongea juu ya kiti gani.

Upande ambao mimi nitazungumzia ni Legislature, wambunge, Kitu cha kwanza mbunge ni lazima akuwe ni mtu ambaye kwamba anaheshimika katika jamii. Katiba itupatie nafasi hiyo ya kwamba, mtu ambaye hana heshima yake, uaminifu wake, yaani ule utiifu wake kwa kusimamia mambo ya society ama mambo ya jamii hana, Katiba isimruhusu mtu kama huyo ama kumpatia mandate ya kugombania kiti cha ubunge.

Ya pili, Mbunge ni lazima awe amesoma na at least awe ako na diploma. Kwa sababu mtu kama hajasoma na anakuwa kiongozi, mimi nachukulia kama huyu mtu ni mchungaji kipofu, a blind herder ambaye hata hajui mifungo yake atapeleka upande gani.

Ya tatu, mshahara na ile benefit ya wabunge, wananchi wapewe nguvu ya kuweza kusema watawalipa kiasi gani kwa sababu hawa wabunge sisi ndio tumewaandika kazi. Na sioni kuwa ni heshima wao baada ya sisi kuwaandika kazi waende Bunge wazungumze vile wanataka, kisha wajipatie mshahara vile wanavyotaka wao wenyewe.

Ya pili, tunataka Katiba ipatie mwananchi nguvu aweze kumfuta kazi ikiwa mbunge hatatekeleza ile kazi aliyochaguliwa juu yake.

Na ya nne, kuhusu huyo mbunge, tunataka Katiba impatie mbunge nafasi ya kuweka ground level akikuja huku kwa wananchi kama kuna bill yoyote katika Parliament, kabla hajaiunga mkono mbunge wowote Katiba impatie nguvu ya kuja kuuliziana na raia au wananchi wake, kwamba ataenda kuunga mkono hiyo bill, au mswaada ulioko Parliament ama hataenda kuunga mkono huo mswaada. Lakini sasa utakuta kwamba wabunge wetu wakichaguliwa tu, basi hakuchaguliwa na wananchi. Anaona kwamba amepotelea Nairobi na uamuzi anaweza kufanya vile anavyotaka. Akiwa anakaa kwamba yeye ni mtu tu, mjumbe pia mtu amepewa salamu tu za wananchi apeleke, laniki hana nafasi ya kuuliza hao wananchi baada ya kuchaguliwa kuwa wanataka vipi.

Nikija kwa upande wa Nation and Citizenship. Nationality and citizenship, kwanza -- - (interjection)

**Com. Yano**: Bwana Ismael tafadhali tutakupa wakati ufaao. Tutakupatia one minute extra. Malizia, your time is up, si uko na Memorandum tafadhali, tutachukua iyo Memorandum tukaisome.

**Ismael**: tafadhali wacha nimalize basi, tunasema hivi, rights zetu sisi wananchi wa Tana River zinakuwa yaani ni kama hazifikiwi, wale viongozi tunaoletewa, askari, ma-D.Os na wale walio hapa, baadala ya kuja hapa kama watumishi wetu, wanakuja hapa kama masters wetu. Wao wameletwa ili watutumikie, lakini utakuta mwananchi anasukumwa sukumwa, yaani bila hata hatia wakati mwingine inakuwa ni kule kushukiwa kwamba amefanya kitu fulani. Lakini hatapewa ile nafasi ya kusema kwamba mimi nimekosea kitu gani, kwa hivyo tunaomba Katiba itupatie nguvu sisi wananchi iwezekanavyo na ilete sheria ya kuwa hawa watu waweze kuwa na njia ya heshima ya kuweza kutu-approach wakati kunatokea kitu chochote.

**Com. Yano:** Asante sana Bwana Dalla kwa kutupatia Memorandum yako. Mwenye anamfuata wakati huu ni Abdulahi Haji Gudo.

**Abdulahi Haji Gudo**: Salaam Aleykum. Kwa majina naitwa Abdulahi Haji Gudo, ninawakilisha baraza la ma-Imam, ambapo sisi waislamu tumeona tupange mipangilio yetu na tupeane kwa Tume ya Kurekebisha Katiba. Mipango mingi nimeiandika katika Memorandum yangu lakini nimeona niangalie yale ya muhimu, kwa vile mengine yashazungumziwa tayari. Nitaanza na mahakama ya kazi. Tunaomba ama tumependekeza kwamba mahakama ya kazi igawanywe mara mbili. Kuwe na Kadhi sub-ordinate court yaani Kadhi ndogo na kuwe na Kadhi's High Court. Kadhi wa mahakama ndogo awe kama daraja ya Chief Magistrate, tunapendekeza. Kisha na kuwe na mahakama ya Kadhi yenye kupokea rufani, yaani Kadhi's High Court of Appeal, yaani Kadhi's Court of Appeal.

Pia tunaomba katika uandikishaji wa ma-Kadhi, kuwe na kamati ya kitaifa ya kuchagua ma-Kadhi. Kamati inayowajumuisha ma-Sheikh, ma-ulama, na hao ndio watakaowachagua ma-Kadhi wadogo. Na Chief Kadhi awe na madaraka kama yale aliyo nayo judge mkuu wa Kenya, Chief Justice. Pia cheo chao kiwe kimoja na malipo yawe sawa.

Nikiingilia sheria ya mahakama ya Kadhi, tukiangalia mipangilio ya sasa, mahakama ya Kadhi haina mipangilio ya kisawa. Ukienda katika Kadhi fulani mipangilio yake huukumu kivingine kwa vile (inaudible) na mengine hukumu kivingine kwa vile (inaudible) tunaomba au tunapendekeza kwamba kuwe na Tume ambayo itabuni sheria ya ma-Kadhi wote, na itapendekeza hiyo sheria ipelekwe kwa wabunge na ipitishwe wawe ma-Kadhi wakiitumia hiyo sheria, mahali popote sheria moja itumiwe kwa pamoja.

Nikipendekeza tunaangalia uhuru wa dini. Katika Katiba ya kwanza kuna uhuru wa kuabudu, ambapo ni kinyume au ni tofauti na uhuru wa dini. Uhuru wa dini ni kuwa na uhuru wa dini katika makazi yako, katika kuchukua passport, katika kuchukua

vitambulisho, ambapo tunaamini kwamba mtu anavyo fanya hivyo hawezi kuangaliwa imani ya dini yake. Ndipo tunaomba sasa kuwe na uhuru wa dini. Kisha kuna wafu,wafu ni pesa ambazo waislamu uzitoa kusaidia nchi za kiislamu, mayatima, masikini na wengineo. Pia tunaomba kwa hii wafu iwe itawekwa mpango, iwasaidie mayatima hao na mipango mingine ya kiislamu kama kujenga madrasa na misikiti, na hawa wabuniwe Tume ambayo itasimamia shughuli hiyo.

Pia kuna zakaa, nikimalizia kuna zakaa ya kiislamu ambapo tunahitaji kuwe kutabuniwa. Tume ambayo itasimamia zakaa kwa kila mwaka, ambapo itakuwa ikitoa mfano kwa asili mia mbili nukta tano watoe na iwe anagawanywa kwa waislamu kwa mwaka ikiwasaidia kwa shughuli zao za misikiti na kusaidia mayatima na wengineo, na mengine nitayapeleka kwa Memorandum yangu kwa vile wakati hauniruhusu.

Asanteni.

**Com. Yano:** Asante sana Bwana Abdullahi, mwenye anayefuata ni Hussein Fayo. Kama huyo hayuko Sukri Dahir Fota. Na tafadhali nikianza kugoga goga hivi ujue namaanisha wakati umekwisha.

**Sukri Dahir:** Asante mwenye kiti. Kwa jina naitwa Sukri Dahir, mimi nawakilisha Group. ambayo kwa jina inaitwa TPF Tana Pastoralist Forum. Mimi natoka kwa kabila la wafugaji na ningependa kupendekeza mambo kuhusiana na watu wafugaji. Hasa kabila ambalo kwa jina linaitwa Wadehi. Wazo la kwanza nataka kupendekeza kwamba, serikali imetuwekea vikwazo, yaani obstacles ambazo zinafanya kabila hili la Adehi lisipate kitambulisho. Vikwazo hivi ni nini? Somali screen card. Jambo la pili grand parent birthcertificate. Hili wazo la Somali screen card linafanya asilimia tisaini na tano ya kabila la Wadehi wakose vitambulisho. Na vile vile unaweza kuona mtu amesoma sana mpaka akafika college level, lakini anaambiwa he has to produce grandparents birth certificate. Naona kwamba hatupati haki yetu.

Jambo la pili. Kuna mambo ambayo tunaita veting. Divisional veting. Naoelea sasa ya kwamba -

**Com. Yano:** tafadhalini mtulie, tumsilikize akisema yenye anayotuambia. Tafadhalini.

**Sukri Dahir**: Naonelea ya kwamba hii divisional veting ifanywe kwa sub-location level. Kwa sababu tunaona ya kwamba committee, divisional committee hawa watambui watu wakutoka sehemu tofauti tofauti katika division hii. Tuseme mimi ni baina ya hao divisional committee lakini siwezi mjua mtu wa kutoka Ngao, hata kama ni kabila yangu pengine siwezi nikamjua, na nitasema ya kwamba huyu simjui na hatakosa kitambulisho.

Pia ningependa kusema the government should recognize, yaani serikali itambue kabisa hii kabila ya wadehi kama wakenya wengine, kwa sababu gani? they have to be given the code number, wapewe code number kama wakenya wengine.

Jambo la pili, ni kwamba wanakuwa discriminated, hawapewi haki yao kikazi, kama ni interview ya college hawapewi nafasi ya kuingia college. They have the qualification lakini hawapewi iyo nafasi ya kuingia college. They are totally discriminated kwa hivyo iyo ni haki yao kuingia waende wakasome, na vile vile katika recruitment, mtu anaingia police ako na all the qualifications lakini anatolewa. Simply because he is being discriminated and is not recognized.

Jambo lingine ambalo ningependa kupitia ni kwamba the land adjudication, ugawaji wa ardhi. Ugawaji wa ardhi naonelea uwe suspended ufanywe miaka hamsini ijayo, si saa hii, kwa sababu gani? ---

**Com. Yano**: kuna nini tulia hayo ni maoni yake kama mtu wa Garsen, amekubaliwa kutoa maoni yake vilivyo, tungetaka mnyamaze ili ikiwa ni wakati wa kutoa maoni tukusikie tafadhalini tunyamaze.

**Sukri Dahir:** Ni kwa sababu gani? Hao wafugaji bado ni ignorant, hawakusoma kabisa, they are still illiterate kwa hivyo naonelea wapate nafasi ya kusomesha watoto wao na vile pia wajue faida ya land ajudication. Wajue faida ya ugawaji wa ardhi.

**Com. Yano:** Sukri tumekushukuru kwa hayo maoni yako, utatupatia Memorandum yako wakati wako umekwisha. Sasa wakati huu ni wakati wa Mohammed Geli. Mohammed Geli, Councillor Said Sadik, Said Sadik. Khadija Shediye, na nitarudia yale nilikuwa nimesema hapo mbeleni tafadhali, kila mtu ako entitled kutoa maoni yake. Mtu akiongea tulia, wakati wako ukifika kama unataka kupinga upinge, lakini kila mtu anakubaliwa atoe maoni yake vilivyo.

Asanteni. O.k. Khadija, karibu.

**Khadija Shediye**: Mimi naitwa Khadija Shediye na ninawakilisha Oral women Group ndani ya Garsen. Kwa hivyo mimi naongea kwa niaba ya wamama kuhusu upande wa urithi na upande wa sheria ya ndoa ya kiislam. Sisi sheria zetu za kiislamu za kisasa zinatuangamiza sana kimaendeleo, akina mama na watoto uzao wote. Kwa sababu baba akikuoa na akijua kwamba wakati wako umepita na umezaa watoto wengi, yeye yuko tayari kukutupa na hao watoto, wengine ni walemavu na wengine ni vipofu wanaotaka usaidizi wa hali ya juu ambao mama hana uwezo wa kujisaidia kwa njia yoyote. Sasa sisi wamama ingekuwa ni kwamba wakati bwana ametosheka na wewe na anamaanisha kwamba anaweza kukuacha kindoa, anasema kuwa anaondoka na mali ile mlibuni pamoja na anamuacha mama kwa hali mbaya ya kusikitisha kabisa. Katika maisha ya mama na vijana na watoto weingine ambao in yatima wako tiyari kurithiwa mali yao na baba mdogo au baba mkubwa kutoka kwa ndugu ya baba yao. Na akianza kurithi anaanza kunyanyasa watoto waliobakia hapo nyumbani na kuwagadamia mambo ya mali. Kwa hivyo sisi tunataka katika sheria zetu za undoa upande wa ukristo na upande wa islamu wawe wanatukuzwa wamama na walemavu na wanyonge wote wapewe haki yao kwa njia ya sawa na njia alisi na masikini wote wawe wanajulikana kuwa wanaweza kujiendelesha kimaisha. Tafadhali sana ninataka katika sheria zetu za Kadhi, Kadhi apate nguvu kutokana na sheria ya serikali na awe na Kadhi appeal, anaweza kua na copy yake ya Kadhi na anaweza kuhukumu. Na sheria ya dini ya islamu inapatia heko na serikali iwe inapongeza sheria chini ya serikali. Na iwe wamama wana-feel free na wanaweza kwenda sheria

sambamba na wanaweza kujigambia haki zao. Kwa sababu tunaona watoto wengi wababa wamewatupa na wababa wenyewe wana mali na wana nguvu.

Na upande wa ardhi: Upande wa ardhi wakati umiliki wa ardhi umetokea, ninataka wamama wote pia wawe wanapewa haki zao upande wa ardhi. Sio wababa tu ndio wanapewa title deed ambapo sasa akiamua ku-divorce wewe anajua hiyo ardhi ni yake na anakufukuza kama mbwa na ali umezaa watoto nayeye wako huko nao, watoto wengine ni walemavu hawawezi kuhudumiwa na wamama ambao si mama zao, ni lazima yule mvumilivu awe mama yako, ikiwa wewe ni mwizi, ikiwa wewe ni kiwete, ikiwa wewe ni kipofu, mama hana njia yoyote anaweza kukutupa. Anaweza kufa na wewe kwa maisha yoyote hata kama ni maisha ya kuomba. Awe anakaa anaomba siku zote kwa ajili yako, kwa sababu sasa sisi, elimu pia wanawake tunaambiwa wanawake wanapewa scholarship wakienda kwa masomo ya juu. Hata sisi waislamu, tunaambiwa kwamba wasichana wakienda shuleni wanakuwa wabaya ndio sababu, kwa hivyo tunataka wababa wapewe mkazo na kuchukuliwa hatua kwenye sheria ya serikali ili wamama wapate nguvu ya kujivunia elimu. Tafadhalini sana tunataka ugawaji wa ardhi ukitokea kwa namna yoyote ijulikana mama kama ana bwana anapewa title deed kwa majina mawili. Either mama awe na yake kivyake au wawe pamoja akipewa hiyo title deed yao, iwe na majina mawili ya mama na ya baba. Asiwe baba peke yake anaenda kujigambia kwa sababu anaweza kuchukua title deed yake peke yake na siku ambayo anatosheka na huyo mama anafukuza mama na watoto na hiyo ardhi ana enda kumiliki na kuuza kivyake kwa starehe zake. Na sisi hatutaki hio forever na njia ya Kadhi, tunataka Kadhi akuwe na Appeal Court, ambayo wakati Kadhi wowote akituhukumu nje raia wanaenda na pesa zao kuchukua koti kivyao, wasiwe wanaruhusiwa kabisa. Tuwe sisi tunayo njia yoyote ya kujigambia haki na ualali wowote, na masikini wawe wanaweza kijigambia maisha yao. Kwa hivyo tunataka uajiri wa kazi ukitokea mlemavu pia awe ana haki ya kiajiriwa kazi.

Na upande wa elimu: Tunataka vipofu wawe na kikundi cha vipofu cha kipofu na walemavu wote wawe wana vikundi vyao. Hasa upande wa maendeleo haya ambayo sasa yametokea kutokea mwaka juzi. Tunataka wale watu walemavu wawe na vikundi vyao na tunachagua kiongozi kwa njia yoyote ili kusaidiana na serikali. Ikiwa mimi ni mama wa maendeleo naninapendelea sana watu walemavu pia, wakuwe na groups zao na wawe wanaweza kujisaidia kwa njia yoyote.

Na hivi ninataka upande wa health pia. Watu wa health, tunataka wasaidie sana kwa mambo ya maendeleo kwa njia yoyote ili wakiletewa ripoti wawe wanachukulia kwamba ni kitu ambacho kinafaa na kinastahili kusaidia wamama kwa njia ya afya na uzazi na mambo mengi. Kwa sababu, sisi ni walemavu.

Asante.

**Com. Yano:** Asante sana mama, nafikiria, inaonekana umeongea kabisa naona ni wazee ndio wanapiga makofi hata zaidi kushinda wamama. Mwenye anayefuata Khadija ni Yaya Ali.

**Yaya Ali**: Mimi nawakilisha jamii ya wafugaji ya Wardehi hapa Tana River, Garsen constituency. Sasa naomba mnipe nafasi ili niweza kueleza.

**Com: Yano:** Tafadhali tumekupatia katika tano, endelea, anza.

**Yaya Ali**: Sasa, jamii ya Wardehi kusema kweli Tana River wanabaguliwa. Na hii inatokana na historia yao. Historia karne ya kumi na sita Waoroma na Wasomali walipigana, ambapo Waoroma walishindwa vita. Maelfu na maelfu wa Waoroma walipekwa North Eastern na Somalia. Hawa watu ambao walipekwa, walipekwa na mifugo, watoto, wanawake na wote wakapelekwa North Eastern, na hawa watu walikuwa wanatumiwa vibaya kama watumwa. Watu hawa walikuwa wamedhulumiwa vibaya sana kiasi cha karne mbili na nusu, baadaye hawa watu around 1950's Wardehi walianzisha vita ya kudai haki na usawa na wasomali. Ambapo wardehi waliweza kushinda vita na wasomali ambapo walipata haki sawa na wasomali wakawa wanaishi kati ya North Eastern wakiwa wardehi wenye haki sawa na wasomali. Lakini wardehi hawa walikuwa wameshabadilisha lugha, utamaduni, itikadi na kila aina. Lakini kuanzia 1950s wardehi walianza kuvuka kwa uchache, 1950s wardehi walikua wanalipa nusu ya ng'ombe zao kwa wasomali, ufalme wa kisomali. Walikuwa wamekubaliana kulipa half of your livestocks kwa wasomali. 1950s kiumbe cha kwanza ambapo kilikuwa na ma-Sheikh na ma-haji watu wenye mali walitoa nusu ya ng'ombe zao wakavuka Tana River. Baadaye 1965 wakati wa Kenyatta government, wakati wa uhuru kulitokea shida huko North Eastern province ambapo kulikuwa na harakati za wasomali, wanataka North Eastern itengwe na iwe part ya Somalia. Wakati huo serikali ya Mzee Kenyatta ilionelea hawa watu wanaweza wakaangamizwa na wardehi wakaruhusiwa kuvuka na wakati huo wanajaza form, kuna form fulani watu wanajaza wakuja hapa Tana River. Hata wardehi walianza kuvuka kwa wingi kuanzia 1960 mpaka 1970, lakini inatufundisha ya kwamba sisi wardehi bado hapa Tana River tunaambiwa sisi ni wageni, hatuna haki kabisa, kwa mfano, mpaka leo lazima Mwardehi akipata kitambulisho Somali screening card. Hii screening card ilitolewa 1999 ni karatasi nyepesi nyekundu. Hio karatasi imeisha sisi ni pastoralists hatuwezi kuweka karatasi kama hizo. Karatasi imeisha na hakuna ofisi unaweza present hio karatasi, lakini unaambiwa leta karatasi ya screen card. Leta birth certificate ya babu yako na nyanya yako, mpaka sisi wenyewe hatuna birth certificates za nyanya zetu na babu wetu. Na hiyo tunaona haki yetu ya citizenship bado tunanyang' anywa. Maelfu na maelfu ya vijana wetu mwaka huu hawata-vote kwa sababu ya hiyo screening card na birth cerficate. Hata ukienda Garsen registration office, Garsen division, Moyale division, forms zetu za application zimekataliwa na zimejaa maofisi ni huko.

Jambo lingine ni wakati wa uchaguzi, wakati wa kazi, ukienda kwa interview pale useme wewe Mwardehi automatically unakuwa disqualified.

Na jambo lingine ni committee, District committees, AIDS committee, Census committee, hizo committee zote za ki-district level sisi hatuko. Hata NGOs wakija Tana River sisi hatuusishwi, NGO wanakuja wanatembelea vijiji vingine, hivi vijiji vyetu vya kiwardehi hawafiki. Na tukiangalia upande wa gender bado kuna mambo ya female, wasichana hawapelekwi shule na

kuwa dhuluma wanawake wanafanyiwa. Lakini kwa vile hatuna viongozi, hakuna mtu ambaye ana advocate rights za women and children fo the society.

Kwa hivyo na upande wa land adjudication, ilipofika ardhi ya Tana River tulikuja tunasikika Wardehi wengine warudishwe kule walikotoka. Saa hakuna Waredehi in North Eastern Province, na tutaenda aje na sisi walio kuja hapa ni wazee wetu na sio sisi. Wale walio zaliwa hapa, tuko na wasi wasi sana ambapo hatujui, kwa hivyo land adjudication tuliambiwa hao ni wageni hawana ardhi.

**Com. Yano**: we give you only one extra minute to wind up.

Kwa hivyo land adjudication in Garsen division, ambapo maelfu na malfu ya watu wamekuwa replaced, watu wameuliwa, kazi zimeharibika, mali imeharibika, kwa sababu ya land adjudication, halafu serikali ililetwa kwa lazima wakuzaji hapa Tana River hawataki ardhi igawanywe, kwa sababu kuna a lot of issues, kuna land issue, kuna land dispute, tayari huku juu kuna a lot of land cases. Ukiangalia huku chini kuna Tana Delta Irrigation Scheme ambayo iko na five thousand acres. Sasa wafugaji hawana mahali. Government haija solve land dispute inajaribu kuleta land adjudication by force. Na wakati land adjudication ilikuwa iaanze Ngao nafikiri tarehe 7th March, vita ilitokea kwa sababu ya land adjudication. Saa hiyo ndio land adjudication ikawa suspended. Kwa hivyo kwa maoni yangu nasema land adjudication iwe suspended untill further notice. Before the government solves that issue, wafugaji wawe na ardhi, sehemu ya juu, wakati wa malisho, wakati wa rainny seasons, ng'ombe ziwe zinaenda juu. Tukuwe tuna enough land, kuwe na a very big land ambapo watu wafugaji wa ---. Na huku za Kipini ambapo wakati wa ukame tunalisha ng'ombe zetu tunataka land.

Na upande mwengine ni mambo ya Kadhi. Kadhi, sisi Wardehi tuna dhulumiwa. Kwa hivyo sasa Wardehi recommendations zetu ni kuwa; Wardehi wawe recognized as a Kenyan ethinic community with participation in development issues.

Second, Constitution should protect the community against any serious intimidation and discrimination, kwa sababu hata wakati wa uchaguzi ukifika sisi tuna wasi wasi tunajigawanya tunasena village fulani ipigie candidate fulani, tuna wasi wasi, uenda tukipigia mtu mmoja wale wengine wakituvamia watuambie turudi makwetu. Sasa tuna wasi wasi, kuna-fear, hatuwezi tuka-exercise our democratic rights.

Na lingine, tunasema our community should be considered as a Kenyan tribe and should be given a code a number. The most important ni code number, some very small commmunties wana code numbers, sisi ni 40% ya watu wa Tana River ni Wardehi lakini hawana hata code number. Mwingine anaandikwa other Kenyans yaani 81, mwingine anakuwa Somali (inaudible) (interjection)

**Com. Yano:** Asante sana, Ali naona uko na Memorandum tafadhali tupatie Memorandum yako, tunaenda kusoma tukirudi

tafadhali Ali tupatie Memorandum yako. Asante sana. Mwenye anayemfuata ni councillor Hassan Omar Guro, Abdi Gile.

**Abdi Gile Suleiman:** Kwa majina naitwa Abdi Gile Suleiman, na ningependa kuzungumzia kwa uchache mambo ya land. Ingawaje Memorandum yangu nimeandika kwa lugha ya kingereza lakini nitaeleza kwa lugha ya kiswahili. Tumependelea serikali isiwe na uwezo wa kumiliki ardhi ya trust land au kupeana sector yoyote ya kibinafsi, kwa sababu hii inaweza kuleta shida kwa wanaoishi katika hiyo ardhi.

Pia tumependelea serikali iwe ikichunguza movements, yaani kuondoka kwa ufugaji kutoka wilaya hadi wilaya ingine, hii inasaidia kwa kupunguza mambo ya tribal clashes, diseases na robbery.

Pia, tumependelea serikali uwajengee shule za boarding hawa wafugaji, kwa sababu wao ni watu ambao wanahama kutoka ardhi, kutoka sehemu moja hadi sehemu nyingine kutafuta green pastures.

Pia, tunaonelea elimu iwe niya bure na ya lazima kwa wakenya wote kuanzia primary hadi secondary. Pia kwa upande wa Bunge, tumeonelea wabunge wawe na ofisi zao binafsi katika constituency ambazo wamechaguliwa, wawe waki-visit, wakija kila mwezi.

Na pia, tungependelea wabunge ambapo watakosa kuzuru makao yao kwa mda wa vikao vitatu mfululizo waondolewe hayo mamlaka. Hali kadhalika tumeonelea wabunge ambapo watashindwa kupeleka malalamishi ya wananchi kwa Bunge mishahara yao ipunguzwe kwa asilimia hamsini na hayo mishahara ikipunguzwa iletwe kwa constituency kwa sehemu walio chaguliwa kwa kuendelesha miradi mbali mbali.

Pia, tumeonelea mishahara ya wabunge iwe-controlled na wale waliowachagua, yaani watu walio wachagua wao.

**Com. Yano**: Bwana Abdi naona uko na memeorandum tafadhali guzia yale ya muhimu hatuna wakati. Utatupatia Memorandum yako.

**Abdi Gile**: Pia tumeonelea katika Tana River tuwe na equal job opportunities kati ya makabila yote yanayoishi hapa.
Pia, tumeonelea katika Tana River, waislamu wanafunzi, pamoja na civil servants wapewe amri ya kuwa na dressing ya Islamic kind. Ku-dress Kiislamu katika shule na mahali pa kazi pia.

Hali kadhalika tumeonelea waislamu, students pamoja na civil servants wapewe nafasi ya wakati on Friday, wakati wa Ijumaa kuanzia saa tano unusu hadi saa nane hali kadhalika wawe wakipewa siku free, siku za sikukuu za kislamu kama Idi day na Mladul-Al-Nadin.

Hali kadhalika tumeonelea, Chief Kadhi achaguliwe na Imam pamoja na Sheikh kulingana na elimu ya kiislamu, kiwango cha elimu ya kiislamu.

Hali kadhalika –(interjection)

**Com. Yano:** Bwana Gile, tafadhali utupatie Memorandum yako tutaenda kuisoma. Mwenye anayemfuata ni Ismail Bogu. Kama huyo hayuko Abdi Robule Bogu.

**Abdi Robule Bogu:** Mimi ninaitwa Abdi Robule Bogu, mimi ni mfugaji na Mwardehi. Nafikiri maneno mengi yametajwa mbele yangu, lakini kwa ajili ya kufafanua vile ilivyo semekana Mwardehi kutoka Kora mpaka Kipini, hakuna idadi ya watu ambayo wamewashinda, lakini wamenyimwa kila makazi yote, wanashinda wakifanya kazi sio kwa ajili ya dini kwa ajili ya screening card iliyotajwa. Tunataka huo mkazo wale waliyoleta ni watu North Eastern, wameondolewa na sisi hatujaondolewa, hiyo hatutaki, kusia jina hilo nyinyi watu ambao mlitumwa kwa niaba ya watu wa Tana River sisi tunawambia hatutaki hayo mambo.

Ya pili, Somali wamepita mipaka yao, siku za ukoloni ilikuwa ni maili tisa kutoka sehemu yote hii. Sio upande wa Garissa lakini Tana River, sehemu hii ilikuwa ni maili tisa. Lakini wametukaza sijui ni fursa gani wamepata ndio wamekuja mpaka maili thirty. Maili thirty wamepita sasa hata maili moja hatufiki wameingia Tana River, kwa hivyo tunataka mahali Msomali wamepita kutoka siku ya ukoloni maili sita, aende hatutaki, aende. Kila mtu apate haki yake, tunataka haki zetu

Jambo la tatu, vijana hawapati kazi shauri amekwisha ambiwa nyinyi ni wageni na kila mtu ametoka sehemu ingine. Hakuna mtu ambaye atakuja hapa, kila mtu amekuja na wale vile walikuja hata sisi tulikuja, ni sisi watu wa Tana River. Hakuna haja ya kuambia sisi ni wageni. Mtu ambaye alitaka kutuambia sisi ni wageni hapa mahali hatutatoka, aende.

Serikali, ilinde haki za makabila yote hata kama ni kabila ndogo, mahala pote, myaya, wata, wote wako na haki lakini sawa sawa na sisi. Hakuna haki anayopata, tupate haki zetu.

Kwa kufupisha sijaandika Memorandum kubwa kwa hivyo. Serikali ---

**Com. Yano:** Mama Leah,

**Leah Kenga:** Jina langu naitwa Leah Kenga na mimi ni mzaliwa wa hapa Tana River na isitoshe hapa ndipo mimi ni mzee wa miaka mingi sana. Nina miaka sabini na moja, kwa hivyo langu ni moja tu. Langu ni kutetea ardhi. Ardhi tumeambiwa udongo ndio mama wa Kenya. Mtu akikukataza udongo akikukataza kulima, hata ukifanya kazi zote za juu lakini chakula chetu kinatoka katika ardhi. Leo tukikatazwa kufanya kazi, tukikatazwa kulima, je tutakula nini? Si tutakufa na njaa? ingawa kuna

jambo la jua na mvua hakuna lakini tunazo sehemu ambazo tunaweza tukalima na tukavumbua vyakula. Sehemu zetu ikiwa nchi imekauka, tunakimbilia maziwani, lakini kwa upande wetu sisi maziwani hakuna nafasi, ukienda kulima maziwani watoto wetu wanamalizwa. Ingawa sote tu wanakenya lakini je, kukitokea watu ambao wanakukataza, mtu yeyote akikukataza kufanya kazi, akikukataza kulima, natumeambiwa katika huu udongo ndiye mama yetu ambaye anatupatia chakula, anatupatia mavazi, anatuptia kila kitu. Mimi hapa nilipo ni mzee, na siwezi kulima lakini ninao wa nyuma yangu ambao wanaweza wakafanya kazi. Shamba ninalo tangu jadi, lakini sasa hilo shamba lije lichukuliwe na mtu ambaye ametoka huko ameingia sasa hivi, je, nitakubali? Kwa hivyo kitu ninacho omba ni hiki, Katiba iangalie masilahi ya wananchi, sio ya wageni peke yake. Wageni wakae nyuma kwanza tuangalie masilahi ya wale ambao wanaishi hapa. Kisha baadaye, ikiwa wamefanya hivyo, baadaye kile kitakacho baki wale wageni nao watapatiwa.

Asanteni.

**Com. Yano:** Asante sana mama Leah Kenga. Mwenye anayemfuata ni Paunde Asako, yuko? Paunde Asako, kama huyo hayuko, Faith Bakero. Councillor Robert Ghuyo.

**Cllr. Robert Ghuyo Suleiman:** Kwa majina naitwa Robert Ghuyo Suleiman, mimi ni Councillor kutoka Mwina. Sina mengi ya kuzungumza maanake hayo yote niliyoyaandika hapa yameshazungumza. Lakini ni machache tu mawili, matatu ambayo nita jaribu kuguzia.

La kwanza, kuna hii ministry ya game, kama ingewezekana ipunguze uwezo wake, haina kazi inayofanya kwa upande wetu, watu wanaliwa na mamba kila siku, wao ni kuzunguka tu, hawana chochote wanachofanya.

Cha pili, tusiwe na koti ya kupeleka watu wanaoshikwa na bunduki. Mtu akishikwa na bunduki ni auwawe, bila msamaha. Kusiwa na koti ya watu wa mabunduki kushikwa, leo anashikwa na bunduki anapelekwa, siku ya pili unamuona ndio huyu kwa kuwa ana pesa, kwa hivyo tusiwe na mahali pa kupeleka watu wa mabunduki, watu wa mabunduki wakishikwa ni kifo tu. Kwa hivyo, nasema hayo yangu yote yameshazungumzwa nitatoa pale, itanibidi tena kuyazungumza, sina mengi ya kuzungumza maanake nitawachosha na bado kuna wengine ambao wanataka kuzungumza.

Asanteni.

**Com. Yano**: Asante sana Bwana Ghuyo kwa kazi nzuri yakuwa unajua unatetea wenzako. Levi Bahati. Yuko? Tafadhali harakisha, na mwenye atakayefuata ni Patrick Boso, karibia tafadhali.

**Levi Bahati:** Mimi naitwa Levi Bahati kutoka Lazima. Mimi maoni yangu nazungumzia habari ya urithi, urithi wa wanawake, wanawake hawana urithi, hawana urithi Tana River, wanawake kwa upande wa urithi, utaambatana na utamaduni wa mtu wa

jamii, wa jamii yao, urithi wa wanawake, wanawake bila Kibokoni hana urithi. Mila Kibokoni mwanamke hana urithi. Tunazungumzia habari ya kuhusu ardhi, ardhi inazungumziwa kwa urefu sana, lakini mimi sina mengi ya kuzungumza kuhusu ardhi. Ardhi inamilikiwa na jamii ya kiasili ya mahali pale, wale jamii ambao walikutwa pale, ndio jamii ambao wanamiliki ardhi ile, ni wao kwanza wapate halafu wale ambao wako nyuma yao nao wapate.

Asanteni sana.

**Com. Yano:** Asante sana kwa wakati wako. Simon Amuma, Simon Amuma, ulikua umeongea?

**Simon Amuma**: Madam Chairlady na wote waliofika hapa amani iwe kwenu. Nilikuwa na machache kidogo ya kuzungumza, Ninaitwa Simon Amuma. Ninaitwa Simon Benjamin Amuma, kwa hivyo nilikuwa na machache ya kuzungumza, la kwanza, tunatatizika kidogo. Sisi tuliishi na mayonda vizuri sana bila shida yoyote, na tulipatana na wale wanyama, na tuliishi vizuri na wanyama wote wa wild life walikuwa tunaiishi vizuri mpaka mwisho ikawa sasa, hawa watu wa wild life walipokuja ndio wanyama wanapungua. Na leo iwe kwamba ati kunadhaminiwa yule mnyama, yule mwenye ile ardhi, binadamu awe yeye ni kifukuzwa. Tunatatizika hapo. Nimezungumza kwa ufupi.

Cha pili ni kwamba, tunashangaa sana, kuna dhambi inayotokea ambayo it is being noticed. Lakini hakuna watu wanaozungumzia hilo jambo. Kuna mzee mmoja alifanya kazi mpaka mwisho akafa, anadai pesa zake za retire mpaka leo hajalipwa. Ni kwa nini yule mtu unamuandika shamba boy nyumbani kwako iwe yakwamba ati unamjua tu wakati yeye anakufanyia kazi, wakati ukimfuta ile kazi, ama ameenda zake retire, wewe huwezi kumpa pesa zake, kwa nini? Na ni kwa nini hawezi kulipwa the last day of his work days, siku ile ya mwisho anamaliza kazi umpatie haki yake aende zake. Kwa hivyo nilipendelea Madam Chairlady ya kwamba wale watu kama wale wanapoenda retire, pesa zao ziandikwe ile siku yake ya kuacha ile kazi azipewe zote.

Cha tatu ni kwamba, kuna watu wengine ambao wanakua nominated, kama Councillors ama MPs. Wale watu kule kwao wamekataliwa, they are rejected in their own home areas, halafu kwa kuwa anategemea Kizito, anamu-nominate, tusiyemtaka wewe unamu-nominate vipi? Hatutaki. Just one point left. Kwa hivyo hatutaki hawa nominees ambao wao wamesimamia kura, wakakosa, halafu wanakua nominated. We don’t like that one. Just another point.

Kulikuwa kuna mtu mmoja ambaye alizungumzia habari, kuna wenzetu aliyezunguzumzia habari ya freedom of worship. Freedom of worship is, mimi kidogo imetilia kasoro kidogo. Freedom of worship hii imefanywa mpaka mwisho Kenya tunakuwa devil worshippers. Kwa nini hii freedom of worshp itokee namna hiyo, tunapata laana hii nchi kwa ajili ya freedom of worship ambayo mpaka mwisho tunakuwa devil worshippers. Ni lazima worship iwe --- hizi dini ziwe identified ya kuwa dini ipi iliyo ya alali ama ina kasoro.

Cha mwisho ni kwamba. Hii tabia ya wanawake, mambo ya kutupeleka makotini na kusema ati sisi tunawa-rape hatutaki, bibi ni wangu. Nimemaliza sasa.

**Com. Yano:** Asante sana. Simon Amuma tumeshukuru sana na pia wamama wamesikia hayo, niwajibu wao kujibu hilo. Sasa tuko na Ababia Dogo. Kama huyo hayuko tuko na Mohammed Said Bashora, Mohammed said Bashora.

**Salim Nyogu Ababia Dogo**: Mimi nitasema kwa niaba ya wafugaji. Mimi nitazunguza tena kwa niaba ya mkulima. Mimi nazungumza juu ya mifugo. Mifugo hana haki Kenya. Mifugo, kila mimea mpaka maua inaenda nje, mifugo dhamani yake ni maziwa, nyama , pesa nyingi lakini hana hazina ya kuenda nje, na ndani ya Kenya hazina market. Iko KMC iliyokuwa inaendeleshwa na serikali, wao tena wanarudi wanaimaliza. (Inaudible) mishahara yote inatokana na mfugaji, wote tena wanamaliza na mshahara kuliko kufanya miradi ya wananchi. Game inafanywa kwa ajili ya wananchi, hakuna huduma yoyote inafanyiwa wananchi, kusoma kwa miradi yoyote. Garana game inafanywa kwa ardhi ya wananchi, haina huduma yoyote kwa wananchi. TARDA iko kwa ardhi ya wananchi, hakuna huduma yoyote ya wananchi. Mfugaji hana haki yoyote ya keunda nje kutafuta market, na nyama haiendi nje, sisi mifugo yetu haina pesa, tunafuga, haina kazi inaweza kutusaida sisi lakini hazina market. (inaudible) iko pesa mara tatu wao wanachukua, grazing fee, auction, export. Ile pesa kama nusu yake hata grazing ya nyasi watawacha, inaweza kusaidia mfugaji, mlimaji, wote na tutaweza kusomesha watoto,. Sisi tunaomba Katiba, (inaudible), pesa ile wanapora, wanakula inalipa watu wa mshahara peke yake, hawafanyi huduma yoyote wala difu, wala jumba, wala kusomesha wote wanachukua wanakula wao wenyewe, afadhali atupunguzie grazing fees shilingi mia moja kwa kila kichwa cha ng’ombe, sisi tutasomesha a watoto wetu, tutakua na machine, mto uko hapa, tutaweza kulima, kufufua uchumi wetu. Sasa pesa zote zinachukuliwa, ufisadi tupu kwa ofisi za serikali. Serikali kila mwaka inahakikisha pesa za miradi inapanga. pesa zinakuja kwa ofisi ya D.C wa Hora, pesa zote zinaenda kwa tumbo za wale wanakaa maofisini. Wanasema wanafanya miradi fulani lakini hakuna miradi yoyote inayoendelea Tana River. (Interjection inaudible) Hata samaki wote wamekufa wote. Kwa hivyo kama nyinyi wana Katiba jaribuni kuangalia haki yetu --- (interjection)

**Com. Yano:** Asante sana Bwana Salim sasatumpate Ali Mohammed. Yuko? Harakisha.

**Ali Mohammed:** Mimi nilikua nataka kuongea kabisa juu ya haya mambo ya kipande system. Hiyo kipande system naona kwa wakenya wengine iondolewe kabisa. Kwa maana ina sharti ambayo imekuwaapplied kwa wengine na wengine haikuaapplied, na hiyo inaleta discrimination. Maanake wanasema all the districts lazima kama wanachukua vitambulisho wawe na vetting, na hiyo vetting unaona kama district zingine hazina, kwa hivyo kama mkenya wa kawaida naona tayari hiyo ni discrimination na haifai kwa wengine. Na pia, nimeona hiyo inamaliza pesa za wananchi, kwa maana tuko kwa economic crisis, serikali inasema hakuna pesa, tuna shida ya pesa, wananchi wanahangaika kutafuta pesa na kutengeneza maisha yao. Lakini wako wengine wana-spent ama wanatoa pesa juu ya hicho kitambulisho kwa ajili ya kunaitwa vetting, kwa hivyo kwa maoni yangu mimi naonelea kipande system iwe out kabisa, serikali ilete kitu kingine lakini sio vitambulisho.

Asanteni.

**Com. Yano:** Asante sana Bwana Mohammed. Mohammed K. Said Bashora, halafu afuatiwe na Cyrus Wairo.

**Mohammed Said Bashora**: Mimi naitwa Mohammed Said Bashora kutoka Nyaro location, na mimi ni mzee wa Gaza. Na wagaza kule wamekaa wameandika Memorandum yao, wamenikabidhi nilete hapa. Sina haja ya kuyazungumza yale ambayo wenyewe waliyoyazungumza mimi kazi yangu ni kupeana na hawa Kamishena wataenda kuikagua huko. Lakini nitaguzia kidogo mambo mengine ambayo yananihusu kama kamati ya usalama, Ndere location, husiano sisi na ndugu zetu Wardehi na Wapokot, wakulima. Kule tunatatizika kwa sababu wardehi ndugu zetu, walikuja tukawakaribisha kukaa, lakini wanakaa ndani ya mashamba yetu, na tukijaribu kulima haiwezikani. Walijenga maboma ya ng'ombe katika yale mashamba. Sasa watu kama hao ni wandugu zetu lakini wanatutatiza. Kwa maoni yangu mimi kama chairman wa kamati ya usalama, nilijaribu kurekebisha na kuenda mbio usiku mchana lakini mpaka dakika hii hatujafanikiwa. Lakini Mwenyezi Mungu ametusaidia kidogo mambo yamepoa. Na kamati hiyo tumeungana wao wardehi na sisi, wao watu sita na sisi pokomo watu tisa tukawa watu kumi na tano, tunashughulikia habari hiyo. Kwa hivyo, sisi tunaiomba hii Tume ya Kurekebisha Katiba ijaribu kutia amani, yaani mfugaji na mkulima hawakai mahali moja. Mimi nalima, nalinda mchana kutwa ng'ombe na usiku ninalinda ng'ombe ambaye Pwani kulinda nyati, na ngurue na kiboko imekuwa usiku mimi ni kulinda ng'ombe. Mchana ni ng'ombe usiku ndovu. Kwa hivyo tunaomba Tume ya Katiba, ikiwa Katiba haijabadilika watu kama hao watengewe, watolewe nje ya mashamba yale wakawekwe kando kama zamani wazee wengi tuliowaona. Wanakaa bara halafu siku za ukame wanakuja kutafuta maji wakinywa wanatoka wanaenda lakini hawakukaa ndani ya mashamba. Kwa hivyo sisi hatutaki yalikuwa ati wananchi wasikae la, mahali serikali wamekubali, lakini watengewe, watolewe katika mashamba yetu tupate uhuru wa kulima maana hili tatizo limetutia njaa kweli kweli Ndera location haina chochote . Kwa hivyo mimi malalamiko yangu ni hayo, basi.

**Com. Yano**: Asante sana mzee, sasa enda ujiandikishe. Cyrus Wairo, halafu afuatiwe na Mohammed Goro.

**Cyrus Wairo**: Habari zenu kwanza, haya, maneno yangu ni mawili tu. Neno langu ambalo nilikuwa nataka kuongea ni kwamba mwanadamu uongea. Unaongea na mtu akiwa mzima au utaongea na mtu akifa? Akiwa mzima. Sasa mimi nauliza katika Katiba, neno langu ni kwamba mimi ningeomba maanake saa hii hospitali, hizi hospitali, bila shilingi hupati dawa hata Asprin. Mwisho unaambiwa pale hakuna dawa enda chemist, ukiende chemist ni maelfu ya pesa upate dawa ya mtoto wako. Kwa hivyo tunaona, serikali inaongeza wanadamu lakini ikiwa dawa hupati, dawa hupati, unaenda dawa hakuna kwa chemist. Ukinda kule unagongwa, ukirudi kule unagongwa, ukipita kule unagongwa, sasa kweli hawa watoto wa Kenya leo au Kenya kesho nani atabaki? Lakini wale wakenya kesho je, wakifariki, Kenya itakuwa na nani? Sasa ningeomba katika Katiba serikali ione ya kwamba dawa ziwe bure. Ili kwamba tujenge Kenya ya kesho.

Ya pili, kuna like moja, ni irithi. Mungu mwenyewe aliumba watu wawili Adam na Hawa. Kisha akasema zaeni muongezeke mjaze dunia. Leo hii family inatoka wapi? Family planning inatoka wapi? Mungu ametupa watoto wawili, je mkiwa saba

mnatafuta dawa za family planning , je kanisa litabaki na nini? Au serikali inafanya nini? Mungu akatupa watoto wawili sawa lakini na hizo dawa zimetoka wapi? na Mungu amesema zaeni muongezeke ili mjaze dunia. Hiyo family planning ya kuua watoto imetoka wapi? Kwa hivyo mimi hiyo hatukubaliani, Katiba itaje hizo hiyo dawa ziondoke kabisa, na tunazilaani katika jina Yesu.

**Com. Yano:** Asante sana Bwana Wario, Mohammed.

**Mohammed Goro:** Mimi naitwa Mohammed Goro, natoa mapendekezo yangu, maoni yangu mimi ni haya, Madiwani walipwe na serikali kuu kwa sababu hao wako na kazi nyingi hapa kwa location na sub-location. Hii ni vile huyo mwenzangu alisema (inaudible) yangu, mimi nafanya na council, vile yeye anasema madiwani kuwa pesa zote inalipwa na haifanyi kazi ya maendeleo ya wananchi, nafikiri madiwani wakilipwa na serikali, hiyo senti ya kutoka kwa wananchi, tunaweza kufanya maendeleo, ya wananchi. Ndio mimi napendekeza, hawa madiwani walipwe na serikali kuu, kama wabunge office walipwe na of the President.

Na ya pili, Mambo ya ardhi: Ardhi pressure yake ni nyingi sana na tukiwa hapa Tana River, tutaambiwa tu, oh, ardhi itakuja kungawanywa na watu wa Nairobi, watu huwa na wasi wasi mwingi, sasa mimi nimeonelea maoni yangu, hiyo ardhi mamlaka ipatiwe, kutoka sub-location hadi kwa wazee.

Tatu, mtu yeyote ambaye anataka ardhi ya Tana River ama mashirika yoyote ya kutoka juu, lazima apitie kwa wananchi aje huku awaombe ndio apatiwe.

Ya nne, bibi na bwana wa kiislamu wakikosona huwa wanaenda kwa mahakama. Lakini sasa mimi naonelea, hii koti Kadhi court ya Tana River iko Hola peke yake. Kadhi court moja tu ndio iko Tana River, sasa mimi nimeonelea serikali iwafanye juhudi waweke kila division, mambo ya bibi na bwana wakiislamu wakikosana, huo ugomvi uende koti ya kiislamu, siyo ile koti ingine.

Ya tano, wafugaji na wakulim: Ardhi ikigawanywa kila mtu atengewe sehemu yake. Ya wakulima kando, kwa sababu Katiba ya mbele ya ukoloni nafikiri. Ugawaji kwa wafugaji hakuna, kwa hivyo sasa iwekwe upande wa wafugaji pia itengwe na upande wa ukulima pia itengwe.

Ya sita nikimaliza, mambo ya hawa wananchi ambao hawana kazi, wengine hawana kitu, wanakaa tu nyumbani. Sasa mimi nimeonelea serikali iwe ikifanya budget yao, watengewe pesa fulani wananchi ambao hawana kitu, hapo nyumbani fungu fulani apewe kila mwezi asaidie, chakula nyumbani kidogo. Halafu ----(interjection)

**Com. Yano:** Asante sana Bwana Goro. Mwenya atakayemfuata ni Zalado Okola, halafu afuatiwe na Buya Gilimani.

**Zalado Okola**: Mimi ni Zalado Okola na kabila langu ni Wata. Kwa hivi mimi nakuja kutoa maoni yangu hapa kwa Tume na tena maoni mimi nakuja kutoa, na mimi ni mtu wa Tana River. Basi tu, hii Tana River ni watu kabila sita, hao ni Hola mpaka Kipini. Kwa hivyo, hii kabila yetu huwa ni ndogo sana, katika hawa watu na wameonewa, na wamedhulumiwa Kenya nzima hawatambuliki. Hata kama ni kazi, kuajiriwa hakuna, hatambuliki, atambuliwe vipi? Kama sisi tuko hapa na Tana River iko na haki. Na Tana River, kabila sita, hizi kabila sita asili ya Tana River ni Wata, na hakusema Tana River ni yetu ndugu zetu wakubwa ndio wanatulalia sisi hatutambuliki sisi. Kwa hivyo kutoka Hola mpaka Kipini sisi tuko Tana River ndani, na haki nyingi tumekosa. Pande za Kola tuko on the extreme tuseme tumekosa shamba wasomali wametunyanganya, tumekimbilia mpaka hapa. Na hivi leo Waoroma na Wapokomo vile hao wanapigana kwa ajili ya njaa tu, walikuwa wanatembea mpaka hola huko. Sasa wote wako hapa hapa tu, ni njaa tu ndio inagombanisha watu. Kola sasa kuna Wasomali tupu, mpaka pahali --. Tana River hii, North Eastern yote wamekwishavuka, wako ng'ambo hii. Waoroma hawanana nafasi ya kwenda ndio wametawanyika hapa, ndio watu wanakuja kupigana, kwa hivi sasa Tana River tumekosa mashamba yetu, kutoka kola mpaka (inaudible) hakuna shamba watu wa Gabo na kwa miezi sita ndio watu wa Tana River, sasa hakuna, hakuna mahali tumekusanyika hapo, sisi wandugu ndio tunapigana sasa, haki zetu zitambulike, haki zetu warudishe, shamba letu, hawa watu wa North Eastern wapelekwe mbali na sisi.

**Com. Yano:** Asante sana Bwana Okola: Buye Ilibani, halafu mwenye atakayemfuata ni Mathew Gapo.

**Buye Ilibani:** Mimi majina yangu Buye Ilibani, kile ambacho nataka kuzungumzia sina mengi ni machache, lakini ningependa kuzungumza hivi. Kuna uwezo wa ma-chief, miaka ile ya zamani kidogo katika Katiba ya zamani chief alikuwa na uwezo na watu wake wale anaokaa nao. Leo uwezo wa chief umepunguzwa kiwango ambacho hakitaeleweka, kwa sababu hata watu wakipigana wakipelekwa kwa chief, chief anashindwa jinsi ya kuamua. Kwa hivyo mimi naomba kwa Katiba hii mpya ambayo tunatengeneza ma-chief warudishiwe uwezo wao, moja.

Pil, nimeona hatari ile ambayo inakuja wakati huu, kwa sababu zamani ma-chief walikuwa wana uwezo wakujua ni akina nani wanaingia kwao nani akina nani wanatoka. Leo ma-chief hawana uwezo, that is why unakuta watu wamejazana hapa Garsen na chief hawajui majina na hawajui wametoka wapi, ni watu tu. Kwa hivyo ma-chief warudishiwe uwezo wao.

Jambo la pili, ambalo nataka kuwaambia ni kuhusu Hanging Act. Hanging Act, hii ilizungumzwa katika bibilia, kuwa mtu akiua mtu auwawe. Hii ilizungumzwa katika Korani, ukiua mtu uwawe, ukiwa umemuua kwa mshale, uwawe kwa mshale. Ukimuua mtu kwa kisu uwawe kwa kisu, kwa hivyo katika Katiba iwekwe mtu akiua mtu auwawe.

Tukiangalia mambo ya natural resource: Binadamu ni mali gamfi katika ulimwengu huu. Binadamu ni natural resource, kwa hivyo ikiwa binadamu ni natural resource ni lazima aifadhiwe kwa zile njia zinazofaa. Huyu binadamu aliumbwa na Mungu, akamuweka shambani kule Eden, kwa nini hakumuweka juu ya akiwa miti? alimuweka shambani na leo mashamba tunayo sawa

na yale ambayo yalikuweko zama zile za nabii Adam. Hatukuambiwa kwamba kwa sababu mtu ni mfugaji, kwa hivyo mwenye shamba aondoke amuachie aweke ng'ombe zake. Katika Katiba hii mpya tunaomba wafugaji walikuwa wakikaa kule (inaudible), kule juu sehemu za Gaza, Wazena, Kipiri, Wayu, Waresorea, Walestokot and Bilbil huko juu, warudi kule kule, waache nafasi kwa mtu ambaye ni mkulima hapa chini. Tunajua wakati wa shida hawa watu walikuwa wakija tunawapatia chakula, tunawapatia nyasi, tunaishi nao vizuri, sasa wamekuwa threat. Hawa watu wamekuwa threat maanake watu hawaishi kwa amani.

Lastly, Land adjudicatio:. Tuna ---kila wakati watu wanazungumzia land adjudication. Land adjudication ni natural resource tuliyoachiwa na. Mungu aliwagawanya hawa watu, kila mtu na kazi yake. Land adjudication utajiri wa Kenya ni ardhi maanake ni mali gamfi, hakuna development yoyote itafanyika, ikiwa ardhi haitagawanywa. Ardhi ikigawanywa umasikini utaondoka, saa hii wewe huna security, huwezi kupata bank loan, huwezi ukapata mkopo kwa banki yoyote Kenya ikiwa wewe huna security. Watu wa Tana River tumelaliwa kutokea ukoloni. Katika Katiba mpya tunataka, tu-stress ya kwamba watu wa Tana River na ardhi igawanywe mara moja, ili tuweze kujipatia mikopo kutoka kwa banki, mikopo kutoka kwa other inistitutions tuweza kufanya development.

**Com. Yano:** Asante sana Bwana Buye, tumeshukuru kwa hayo maoni yako. Kwa wakati huu tumuite Mathew Gabo.

**Mathew Gabo**: Kwa majina yangu naitwa Mathew Gabo na nina jambo moja tu ambalo kwamba nataka kuongea, maana mengi wenzangu wameshaongea. Kwa hivyo, sitaki kupoteza wakati. Jambo ambalo nilikuwa nataka kuongea ni kwamba katika mfumo huu wa serikali wa sasa, mfanyi kazi waserikali amefinyiliwa kwa sababu wanaangalia upande mmoja tu, wa elimu ili mfanyi kazi apitie kutoka kiwango hadi kiwango. Wanaangalia akiwa na diploma, wanampandisha cheo, akiwa pengine ana degree wanamuweka juu, lakini hawaangalii wale ambao wana bidii ya kazi. Kwa hivyo katika mfumo huu wa sasa, katika Katiba mfanyi kazi wa serikali pia ambaye anafanya bidii, aangaliwe ili awekwe katika kiwango cha juu na yeye afurahie matunda ya uhuru. Mimi ni hilo tu ambalo nilikua nataka kuongea yale mengi wenzangu wameshaongea.

Asanteni.

**Com. Yano:** Asante sana Bwana Mathew, kila mtu akiongea namna hivyo tutakuwa tumefanya kazi nyingi sana. Councillor Adam Guruka..

**Cllr. Adam Guruka:** Salam Aleykum. Yangu ni machache nafikiri mengi yamezungumzwa. Mimi naitwa Councillor Adam Guruka. Maoni yangu kwanza tunazungumza mambo ya wild life. Mambo ya wild life, serikali yetu ya sasa inadhamini wanyama kuliko wanadamu. Kwa sababu, kila wakati, kila usiku na machana, watu wetu wanauliwa na mamba na nyati, lakini

tunatatizo kubwa sana, ukipiga ripoti hakuna hatua. Na imesemekana kuna malipo, tunaomba Katiba ya sasa, tunaomba mtu yeyote, mtu akiliwa na wanyama, akijaza form, baada ya wiki moja ridhaa yake ilipwe bila kuenda Nairobi. Ilipwe kwa ofisi ya D.C bila kupelekwa hapa na pale.

Jambo la pili, mambo ya elimu, serikali inatusimamia elimu vizuri hatukatai. Wakati uliyopita ilikuwa mambo ya elimu inasimamiwa na serikali, lakini mda wa miaka kumi iliyopita huwa tunajitegemea sisi wananchi, elimu na afya. Watu wote si sawa lakini tunaomba Katiba ya sasa malipo ya hospitali na walimu, serikali itusimamie kama zamani. Kuanzia nursery hadi secondary. Walimu wa islam, serikali huwa inalipa elimu upande mmoja, imetuwacha sisi waislamu nje. Walimu wa islam pia serikali isimamie kama walimu wa shule zile zingine waislamu pia ni wakenya, sio ambao wanatoka sehemu fulani, sisi wote ni wakenya, akiwa ni mwalimu wa shule, akiwa ni mwalimu wa dini, serikali ichukue jukumu hilo iwe yote ni sawa.

Jambo la tatu, mambo ya hii retire, ambayo imetokea juzi juzi hata mtu ambaye ameandikwa kazi hajamaliza miezi tatu anapewa retire, hii iondolewe. Wale ambao wanafaa kupewa retire waangaliwe wale ambao file zao si nzuri kwa kazi zao badala ya kuachisha watu ambao wako na miaka kumi na nane, hata hawajafikisha miaka ishirini. Naomba kidogo.

Jambo lingine, sisi Watana River mimi ni mfugaji na mkulima. Sisi kusema ukweli Tana River hatuna maendeleo kwa sababu mapato yetu ama mifugo, na mapato yetu ya kilimo hatuna pahali pa kuenda kuuzia, hatuna soko. Serikali itusimamie ili mpaka sisi tupate masoko kutoka sehemu za nje tupeleke mifugo yetu, ikiwa ni mazao ya shamba ili serikali itupatie factory yetu katika wilaya yetu ya Tana River.

Asanteni.

**Com. Yano:** Asante sana Councillor Adam Guruka, anayemfuata ni Councillor Abdulahi Bile, halafu afuatiwe na Haji Z. Godana.

**Cllr. Abdulahi Bile**: Salam Aleykum. Kwa jina mimi naitwa Abdulahi Bile Moru na nimechukua nafasi hii kurekebisha Katiba. Katiba yenyewe nafikiri imekuja kwa kimakosa kurekebishwa kwake. Kwa sababu nasema hivi, saa hii ndio tumegawanyiwa vitabu ndani ya hii hall tunaonyeshwa picha ambapo tutaongea ama tunasikiza yale maoni ya watu wengine, kwa sababu saa hii district tulikuwa na co-ordinator wetu ambaye alikuwa anasimamia CKRC. Lakini hakuna kitu ambacho tulijulishwa, committee ilichaguliwa nje na ndio saa tunaambiwa muhudhurie na mtoe maoni yenu. Maoni gani tutaongea twajua.

Nikianza na yale maoni yangu kwa serikali, wafugaji wamesahuliwa. Nikisema wafugaji ni kwa sababu, saa hii hatuna huduma yoyote ya serikali. Kama ni chanjo, zamani tulikua tunapata chanjo kutoka kwa serikali za ng'ombe, tulikuwa tunapata dip kutoka kwa serikali saa, hii yote mfugaji ndiye amepatiwa hilo jukumu na hali wakulima, kila mwaka wanaletewa mbegu, kila

mwaka wanapatiwa ile soko mpya, ndio watapatiwa sisi hatuna soko ya nje, kwa hivyo tunataka hii Katiba ya sasa wafugaji wawe wanasimamiwa kama wale wakulima.

Upande wa sheria: Mimi ndio mhalifu, mimi ndiye nakosea, lakini sheria ya Kenya sijui ni mahali gani mimi nitaelekea, kwa sababu police officer ako na saa hiki kitabu ambacho mimi atanifunga nacho. Makosa yangu yale nimefanya sijui, nakimuambia wajua sheria ya Kenya iko mahali moja peke yake, kitabu kimoja peke yake, tunataka kuwa Katiba ya sasa mwananchi lazima ajue mahali gani, sheria, haki yake ni nini.

Upande wa masikini, serikali ilianza vizuri zamani. Lakini saa hii imefika mahali ambapo masikini hana haki, kwa sababu nikisema hivi, hospitali saa hii ukienda tajiri na masikini wanaenda hospitali moja. Ile dawa wameitishwa kama moja, ile tajari anajidungia, yule masikini ambayo anajidunga ni hiyo hiyo moja. Sasa masikini baba yake ni nani? Kama ni shule karo ya shule yule tajiri, umesikia nikisema kama Rais ama mtoto wa waziri, ile shule anaenda ndio yule masikini anatakiwa, hasipolipa hiyo ada haendi shule, kwa hivyo tunataka serikali vile ilivyokuwa hapo zamani iendelee, ki vipi? Zamani mtoto wa primary vitabu kila kitu kilikuwa kinasimamiwa mpaka college na wanalipa (inaudible) kwa wale ambao wanaenda college. Saa hii hata nursery mpaka ulipe kitu kidogo kwanza kwa kutafuta nafasi yenyewe. Kwa hivyo, tunataka kuwa kama ni masikini inatakikana iwekwe haki yake tunataka serikali imulazimishe mzazi kwanza awe atahukumiwa kama hajapeleka mtoto shule. Na serikali ile ingine, isimamie.

Upande wa national reserve:. National reserves ni za serikali lakini saa hii, ile nafasi saa hii Tana River sisi nafasi yote serikali imechukua na tunataka kugawanywa kwa ardhi. Ardhi gani itagawanywa, na serikali ndiyo imechukua? Isitoshe ugawaji wa ardhi, saa hii tunaweza kusema kuwa mkubwa fulani, ako na acre zaidi ya kiasi fulani, je, masikini atapata wapi ardhi? atajitengenezea, ama ataiba? Kwa hayo machache mimi nasema kuwa serikali iwe inasimamia wananchi.

Asanteni.

**Com. Yano:** Asante sana Bwana Adbullahi Gile. Mwenye anayemfuata ni Abdi Dede Godana.

**Abdi Dede Godana:** Mimi sijasoma naweza sema kwa Kiswahili lakini Kiswahili yangu ni ngumu. Kiswahili naweza kuongea. Mimi naitwa Abdi Dede Godana ni headman wa (inaudible) village. Sisi ni kabila linaitwa Wada. Basi mimi sina mengi ya kuongea ni kuuliza kama shida yangu naweza kuongea inakubaliwa? shida yangu ni sisi niwatu masikini kwanza hatuna ng’ombe, hatuna mbuzi, hatuna chochote. Na watu wetu hakuna mmoja ako na kazi, ni watu washa funikwa. Hii(inaudible) mtu basi anayeokenana hapa area hii ndio sisi. Hawa watu wanajaa hapa wanakuja tu nyuma yetu lakini wametufunika, sasa sisi hakuna mtu tunajua. Kama kuna kitu kinatokea hakuna mtu anatujulisha sisi, wanafanya vile wao wanataka, sisi tunafichwa tu.

Kwa wanawake group ya maendele, kuna wanawake wa maendeleo, kila mtu anasemekana maendeleo wanawake wafanye. Sasa kila kabila wamepatiwa machine wanalima shamba, wanapata maji kwa sababu ya machine hiyo. Sisi wanawake wetu hakuna mtu anawapatia machine ya maji, hawalimi, wanakaa tu bure na inasemekana wako na maendeleo. Na maendeleo hayo yako nyuma, sasa shida yangu ni hiyo. Upande wa shamba sisi hatuna shamba, hatuna ng'ombe, kazi yetu ni kulima. Tukilima nchi yetu inasemekana ni nchi ya ng'ombe mtu aondoke aende kando, hapa ng'ombe zitalishwa, tunahama huko, sasa hatuna nafasi ya kulima upande wa shamba.

Na upande wa homeguard. Siku moja wanaandikwa homeguard, watoto wetu pamoja na mimi sisi watu watatu, tulikuja hapa ofisini tukasema tunataka bunduki kama homeguards. Ikasemekana bunduki ziko Kipini tuende huko, tukaenda Kipini. Mimi Abdi Dede popoto wa Badija tukaenda Kipini. Watu wanafundishwa hapa, wanapelekwa huko, wanapatiwa bunduki, sisi tunakuja tunaulizwa nyinyi ni kabila gani? ni Wada, hakuna bunduki, muende muuliza D.O wa Garsen awapatie karatasi. Tumekuja kuulizwa karatasi, hatukupewa wametunyanganya karatasi. Basi sisi hatuna chief, hatuna homeguard, hatuna headmen maalumu. Ndio watu wametulalia sisi hata agent wa serikali akikuja wanabeba peke yao sisi hatupati, tunapatiwa kiasi kidogo na wale wengine wanapewa tunapatiwa na jamaa zao, sisi tunapatiwa mji mzima gunia kumi, kumi na mbili, kumi na tano, ishirini, kama zinazidi ni thelathini, watu wanapata themanini. Basi sina mengi ya kuongea, kama ningejua kuzungumza zaidi ningeshukuru serikali ingebadilisha Tume yake.

**Com. Yano**: Asante sana enda ujiandikishe. Ibrahim Moru, Councillor Jacob Biro, tafadhalini na tutulie, heshimu maoni ya watu wengine ili pia wakati wako ukifika wao wakusikilize.

**Ibrahim Debe Moru:** Mimi naitwa Ibrahim Dupe Moru, na hivi sasa niko na nywele nyeupe, nafikiri mnaweza kuniona kama mimi ni mzee sana. Nafikiri kikao hiki ambacho tumekaa hapa nikijuwa hii yote ilikua ni jangwa hakukuwa mji na watu hapa. Nikikumbuka kabisa mimi nikiwa mtoto hii yote ilikuwa ni jangwa, kwa hivyo sasa kwa vile wingi wa watu walioingia hii nchi ya Tana River kutoka Garissa, kutoka Malindi, kutoka Kisumu hata wengine nakuta wako hapa, wengine wanatoka Marereni sehemu za Malindi, nafikiri wako watu wengi sasa tuko na jamii nyingi na tumepanuka sasa tumekuwa tunajenga, tuna shule, tuna chief, tuko na ofisi, ilikuwa hayo yote hakuna hii ilikuwa ni jangwa tu hapa. Nikikumbuka kama nilipokuwa mtoto mdogo, lakini wakati ule ninaanza kuzungumza sasa vile nimejitambulisha mimi hapa mbele yenu, na hivi sasa naanza kuzungumzia zile shida ambazo zimetukumba sisi. Kwa hivyo, wakati huu sisi, hatuwezi kutambuliwa kwa sababu sisi ni kabila ndogo, sasa wapokomo wamepata elimu wametukalia. Hakuna mtu anatujua, Muoroma alikuwa ni mtu anayefuata mkia wa ng'ombe aliona sasa amepata elimu, amekuwa chief, mbunge, D.C, D.O sasa wametufunika, hakuna mtu anayetujua, lakini kwa ukweli sisi tunajulikana kutoka ukoloni, wacha wakati Kenya ilipata uhuru. Kutoka ukoloni tunajulikana kama sisi ni wananchi wa Tana River hii. Hapa mahali mnao kaa hii yote ilikuwa, tuseme ni kama kambi ya babu yangu. Hapa ni kambi ya babu yangu na nazi ya Maziwa ni kambi ya babu yangu, na hapo maziwa inaitwa Daraba sio maziwa, inaitwa Daraba. Kabole, unasikia sasa hapo panaitwa Sera, sio sera pana inatwa Kabole, huko kote ni makambi yetu. Unasikia Ida Baganda huko Wardehi wamejazana tele huko, huko kote ni kambi yetu, ni kambi za babu wetu tukiwa tumefungua macho tunatembea na wazee wetu huko, tunalala

huko, ni nyika tu hakuna chochote. Lakini kwa vile sasa Mungu ameleta njia wale waliopotea ama waliochukuliwa na nguvu siku zile za vita walirudi, na hatukuona vibaya vile waporudi, hatukuona vibaya, lakini tu kitu kimoja kinatushinda sisi hapa. Hatulimi, sisi tumefunikwa, Wada tumefunikwa hatulimi, hatuna shamba na kutoka mbele sisi si watu wa kulima, hatulimi, kutoka mbele hatulimi, lakini baada ya hiyo tuko na jembe letu serikali imekuja inatunyanganya jembe letu. Sisi ni watu wa kula nyama peke yake, sio watu wakulima, na watoto wetu tunawalisha tunauza nyama, hatuna nyama ingine ni pembe, tunauza pembe, halafu tunapata nguo za watoto, kwa hivyo sasa hayo yote tumefungiwa, tafadhalini sana.

Laughter.

**Com. Yano:** Karibu Councillor Jacob Bhuyo.

**Cllr. Jacob Bhuyo:** Mimi jina langu ni Councillor Jacob Bhuyo na leo ninashukurani kubwa sana kukutana na hii Tume. Hii Tume nafikiri imeona maneno vile yako, wanachambua mambo mengi sana, wale walikuwa wanalialia hapa, mengi yamefunikwa leo, hii Tume imekuja kufufua hawa watu. Leo unaona wengine wanalalamika, wengine wanakasirika, hakuna haja ya kukasirika, hii leo, Tume inasikiliza maneno, na inachua maneno ya watu, na inaenda nayo na itaenda ili ijulikane hawa watu walikuwa kabila ndogo na imesahauliwa.

Kwanza. Jambo la kwanza, mimi nimesema mimi natoka katika community ya Wada. Huyo mzee alikua amesimama kuongea, sisi ni watu asili wa hapa, hata hatukutoka popote tumekutwa hapa, yule anakuja anatukuta hapa Tana River. Sisi katika Tana River district tuko kabila ya Wada elfu tatu na mia sita na sitini, kabila nzima ya watu. Na hawa watu kabila hii wamepoteza haki yao kabisa hawatambuliwi kabisa, kabisa, kabisa na leo tumetoa kwa Tume ya Katiba ili watambue chini ya Katiba hii mpya, tafadhalini sana, tutambulike hii kabila ya Wada wako katika Tana River district.

Tena nikiikingilia maneno mengine ya mambo ya utawal, tuwe na utawala tugawanye kwa haki sawa, kwa sababu kama kiti cha Rais akue katika province yake atoke. Kama anataka province ingine wakati mwingine aende kwa province ingine, kwa sababu hiyo ni muhimu sana ni jambo ambalo linashirikishwa kikamilifu kwa hali ya utawala.

Jambo lingine, sisi kama watu wa Tana River, hapa tuko na taabu kubwa sana na lazima tueleze leo kwa ajili ya kuandika Katiba mpya. Sisi Tumepata taabu kabisa watu wa Tana River, hata Tana center. Kwa hawa watu wa kampuni ya stima wanatoa Kindaruma, wametuletea taabu nyingi sana, tumekosa chakula, mto unakauka, hatupati chochote, tumeadhirika, mambo ya mikopo, mambo ya wanyama kumaliza binadamu inatokana na hiyo stima inayotolewa huko, na imefunga mto Tana. Ikiwezekana sisi watu wa Tana River tulipwe ridhaa bwana, sababu tumepata taabu sana, vitu nyingi hatukupata, maafa mengi yametuingia sana.

Jambo lngine, mimi natoa maoni yangu ya kwamba district ya Tana River ni kubwa sana. Ujaribu kugawanya mara mbili ili

tulete huduma karibu na wananchi watambulike katika Katiba kwa jina mpya.

Jambo lingine, ikiwezekana chini ya Katiba mpya hii, wananchi wa Tana River wale walipoteza maisha yao kwa wanyama wa misituni, tafadhali walipwe kwa ridhaa, wale walipoteza watu wao, iwekwe katika Katiba mpya. Tena sisi tumepata taabu sana wananchi wa Tana River, stima yenyewe inatumika Kenya nzima, inatoka kwetu lakini hatupati stima yoyote, ndani ya Tana River district tunakaa na giza ile taa inaitwa koroboi ile ya kuakisha usiku. Na shirika yoyote hatupingi maendeleo, maendeleo ni kitu muhimu chini ya Katiba mpya lazima watambue ya kwamba wananchi walioko Tana River, wakubali maoni ya wananchi, mimi nimetoa haya maoni yangu kwa hii Katiba mpya. Na habari iko hapa nimeandika katika Memorandum yangu, katika sisi waislamu, siku ya sikukuu ya Idi, tunataka tutambuliwe kabisa kirasmi ya kwamba iwe siku ya mapuziko taifa nzima. Hii ni kama public holiday, kama mkristo ambaye anasherekea siku ya Pasaka au sikukuu ile ingine ya watu wanapewa mapumziko hata sisi tupate chini ya Katiba ikubalie waislamu tuwe, tupate siku ya mapumziko vizuri kwa siku zote mbili. Mimi bado katika Memorandum yangu nimeandika maneno mengi mengine na ambaye sitaki kusoma yote na mimi nataka nyinyi msome.

**Com. Yano**: Asante sana Bhuyo, tumeshukuru sana kwa hayo maneno, utatupatia Memorandum yako na u-sign register yetu. mwenya anayefuata ni Nathaniel Kiunga.

**Nathaniel Kiunga**: Asante Madam chairlady kama hiki kitabu tungekipata kutoka jana pengine tungejifunza mengi, lakini tumekipata hivi karibuni. Lakini yangu ni machache, kwanza natarajia katika ule wadhifa wa urais -- Jina langu naitwa Nathaniel Kiunga. Wadhifa wa urais, Rais awe akipatiwa mamlaka ikiwezekana mara mbili peke yake. Hasije akaingia mara ya tatu, pia mbunge, kila mbunge aliye chaguliwa aweke ofisi yake katika tarafa yake ili kwamba wananchi wawe wakimuendea pale. Hiyo hakuna mbunge tumchague hapa anakaa Nairobi, ikiwa hana ofisi mwanachi awe na uwezo wa kumuita na kumtoa maanake hatumtambui. Na iwapo amevuka sakafu bila kuambia wananchi kile kiti cha ubunge kiwe wazi, apende asipende, mwanachi achague mwingine.

Mamlaka ya nchi. Ma-chief waweze kuchaguliwa na wananchi wenyewe, si kuchaguliwa na serikali kwa kutumia ubaguzi, maanake ma-chief wengi ukichunguza, chief pengine amefanya kazi ya u-askari, chief amefanya kazi ya ujeshi na mwananchi hampendi. Kwa hivyo inaonekana hapa hapa, kwa hivyo Katiba iwape nguvu wananchi wachague chief wao.

Na ya tatu, mhalifu iwapo amewekwa korokoroni, isiwe akipigwa akiteswa, mbali awe na uwezo wa kujiandikia kile kinacho takikana, lakini si polisi kumusurutisha. Na pia awe katika kizuizi kwa mda wa masaa, ishirini, ishirini na nne ndio apelekwe kotini.

Upande wa kuajiri kazi: Hapa Tana River tumekaliwa sana upande wa kazi, ikiwa serikali wametangaza kazi tuseme kama ya u-askari, ama kazi ya walimu kama hivi juzi, kuna letwa watu kutoka nje wanapewa interview, wale vijana wetu ambao wamekwenda training wanaachwa, kwa hivyo Katiba ionyeshe kwamba wale ambao wametoka katika Tana River ama district

ile iwe wameandikwa. Hivi sasa walimu hao walioandikwa hivyo ukitafuta Tana River huwezi kuwapata wamerudi kule ma-kwao. Kwa hivyo Katiba iweke mkazo kwa upande huo. Kwa upande wa elimu iwe lazima watoto kutoka miaka saba wapate elimu ya bure, lakini hivi sasa ukitembea hapa Garsen utakuta watoto wengi wanauza mikate kwa sababu elimu imekuwa ukipeleka mtoto bila kulipa elfu moja mtoto hatasoma, na wewe ni masikini chakula unatafuta. Sisi mtoto atakuwa masikini hawezi kuingia shule. Kwa hivyo, Katiba ikaze na serikali iweke mkazo na mpangilio maalum. Pia upande wa ufisadi, ufisadi umezidi kwa sababu katika hii bara bara hii unaona ikiwa wewe unataka kazi mpaka kwanza umuonge yule mkubwa ndio upate kazi. Na hapo hapo unatafutiwa makosa kama umeandikwa kama watchman, unafungwa, kwa hivyo Katiba ikiwezekana pale palipotoka ule mpango wa kuandikisha kazi, wenyeji wa pale wapate kazi. Lakini si kuchukua watu kutoka nje. Kwa hayo mafupi nimemaliza. Asante.

**Com. Yano:** Asante sana Bwana Kiunga. Anaye fuata ni Jeremiah Higwo, halafu Reuben.

**Jeremiah Higwo**: Mimi naitwa Jeremiah Hingo, nilikuwa nataka kuzungumza kwa sauti ya upole ili nipate kusikika vizuri. Kwa kweli hoja yangu ya kwanza kuchangia hii Katiba ni kuhusu hali yangu mimi mwenyewe ya kiraia vile nitakavyo ishi katika dunia hii ama katika country hii ya Kenya. Kuna mamlaka ambayo yamepewa mtu kama D.O kama chief ambaye ana haki ya kunishika kokote ama kuniamuru vyovyote vile. Mimi, mtu kama raia ambaye sina chochote hali yangu ni ya unyonge, ni ya kutembea tembea, mtu yule akinionea kwenye vichaka ama kwenya kichochoro nichukue hatua gani ama nitamshtaki mahali gan? Ama mtu kama huyo nitamchukulia hatua gani ama nitamshtaki popote pahali gani? Na ninaomba kama ingewezekana saa hii mkatujibu sote raia ambao tuko hapa.

Pili, kuhusiana na hii hali ambayo tunaendelea nayo hapo kwetu ni kuhusiana na hizi clashes ambazo zinaendelea. Ukweli ni kwamba, mimi baba yangu ni mzee Maboki amenizaa Tana River district kando ya mto kidogo hapa, amenizaa pale, alikua akilima lima pale. Na ule mmea ulikuwa hauondoki kwenda pahali pengine, ule mmea ulikuwa anakaa pale pale. lakini kuna mfugo mwingine unatoka kule unakuja kuharibu ule mmea, sasa hapa ndio mahali panaleta fujo, kwa hivyo haki ni kwamba chui na mbuzi kuwaweka mahali moja haitawezekana kulingana na Katiba. Ni kwamba mfugo ukae kando na mmea ukae kando, kwa sababu mmea hauli mbuzi, mbuzi ndiye anakula mmea. Kwa hivyo kulingana na hoja hiyo nimemaliza. Hapo ndipo mwisho wangu.

**Com. Yano:** Asante sana, asante sana Bwana Higwo. Reuben Soso.

**Reuben Soso:** Kwa majina naitwa Reuben Soso na mimi nimetoka katika jamii ya wawindaji halali, yaani jamii ya Wada. Na mimi ni mchungaji wa kanisa na natoka (inaudible). Kitu kile ningezungumza kuhusu Katiba ni kuhusu jamii ya Wada. Katiba ya sasa ningetaka iweze kuangalia makundi yale madogo ikiwa moja ni jamii ya Wada. Kama ingewezeka na wapatiwe settlement scheme itakayofanya wote wakae mahali pamoja ili wapate development mahali pale.

Jambo lingine ambalo ningetaka kuzungumzia Katiba iangalie ni usalama. Kama mzee wangu aliyetangulia alivyosema security. Miji na misuko suko sisi nasi tunavyo tafuta mzee wa homegaurd, mkianza kufuata fuata mambo yote yanakuwa hayana maana. Kwa hivyo, Katiba ya sasa ningetaka ione ya kwamba jamii hii nayo inaangaliwa kiusalama.

Jambo la tatu, ningetaka kuzungumza kuhusu elimu. Jamii ya Wada Katiba ya sasa ihakikishe ya kwamba wanapata elimu, yale makabila madogo, kwa sababu huu ujambazi unao endelea barabarani ni ukosefu wa elimu na watu wananyanganya. Na ningetaka kusema ya kwamba elimu iwe ya bure kisha iwe ya lazima, watu wasome.

Na jambo la mwisho ambalo ningezungumza ni kwamba Katiba ya sasa iweze kuona ya kwamba kila mmoja, yale makabila madogo nayo yameingizwa katika kushiriki kwa kazi za kiserikali. Kwa sababu kumekuwa na ufisadi mwingi. Waajiriwe nao wapate kazi hasa kabila la Wada, wapate kazi nao wapate kula national cake. Nafikiri hayo ndiyo maoni yangu, Mungu awabariki.

**Com. Yano:** Asante sana Bwana Soso. Mwenye anafuata ni Zila Dulu, halafu baada yake ni Abdalla Giyo.

**Zila Dulu**: Kwa majina naitwa Zila Dulu. Maoni yangu ambayo nilikuwa nataka kuchangia katika Katiba hii tunayo rekebisha, ni kuhusu urithi wa wanawake. Wanawake kwa jumla tunanyanyaswa kivyovyote. Katika hali ya kuolewa, kielimu na urithi, unakuta mwanaume ndiye anapatiwa elimu kwa nguvu msichana anawachwa. Ikizidi unaambiwa wewe utaenda kujenga boma ya watu, kwa hivyo mzee hatakubali kuharibu pesa zake kwa sababu unaenda kukula mali yake kwa boma ingine. Na tukikuta mwanamke tayari ameachwa, hajui aende wapi, kwa sababu kwa wazazi hana urithi, hana kibali cha kiwanja chochote cha kujenga, hana mahali anaweza kufanya kazi, inabidi mwanamke ana randa randa anakuwa malaya, ambalo jina hilo tayari limetuharibu wanawake. Na ni kwa sababu ya kukosa urithi katika familia.

Pili, tukiangalia habari ya ardh: Ardhi ama ukosefu wa makazi ni bora kuwe na majimbo, ndipo tutaweza kutawala sehemu yetu. Ikiwa muoroma ni mtu wa Pwani atapata sehemu yake ya kufuga mfugo wake. Maanake hata mimi naweza nikasema pia mimi ni mfugaji maanake kwa nyumba yangu kuna panya, nitaambiwa ni mfugaji wa panya. Na nikikosa mahindi je, panya ataishi. Hata wewe ambaye unasema wewe ni mfugaji lazima ukule sima, je, ukinikataza nisilime, umekula nini? Pesa zako nitakazo nunua nyama yako ama soko lako la nyama ukinikataza nisilime pesa hiyo nitaipata wapi nikununulie nyama yako. Tumekosa maendeleo.

Tatu, nimeomba Rais apunguziwe majukumu. Rais amepewa mamlaka ya kila kitu, mamlaka tunajua sheria ndiyo iko juu, mamlaka yako chini, lakini sasa hivi tunaona mamlaka ndiyo yako juu, sheria iko chini. Ni kumaanisha Katiba iko chini ya sheria. Rais apunguziwe majukumu. Rais naye awe anaweza kuwa kama binadamu yeyote ijapo atakua ni kiongozi, na sheria iwe inamsimazi wa ile sheria kikamilivu, hasionee upande huu wala upande ule, lakini tunaona Rais ndiye anaweza kuamuru sheria ambapo haiwezekani. Ni kama vile sisi tunavyo chagua mbunge, mbunge tukimpeleka kule, tulimchagua sisi na Rais

amewekwa pia kutulinda sisi na kama hatumtaki, pia tuwe tunaruhusiwa kutoa maoni kuwa hatumtaki. Na tusiweze pia kuchaguliliwa mambo mengi zaidi juu. Pia sisi tupewe mamlaka ya kujiamulia wenyewe, sisi tulioko chini. Kwa hayo machache nimesema ni asante.

**Com. Yano:** Asante sana. Abdalla Giyo, kama hayuko, Mohamud Jago, Nasir Guyo, Mohammed Farah.

**Mohammed Farah:** Kwa majina naitwa Mohammed Farah, kutoka kwa ukoo wa wafugaji. Ya kwanza naongea kuhusu mbunge. Mbunge wananchi ndio wanaowaandika kazi, tunataka Katiba ya sasa, mbunge wananchi wawe na uwezo wa kumfuta kazi pia, kama wao ndio waliomuandika. Kwa sababu tukisha muandika kazi hatumuoni tena mpaka miaka mitato. Tutakuwa tunachelewa sana. Tunataka awe na ofisi katika tarafa yake hata kama siku moja kwa mwezi tumuone, lakini kama hatumuoni tuwe na uwezo wa kumfuta.

Pili, naongea kuhusu kitambulisho hapa Garsen division. Tuko na shida sana, haya mambo ya vetting ya metukosesha vitambulisho za watoto. Sababu unaweza kuja ukaambiwa leta screening card, pengine huna screening card, utatoa wapi? Unaweza kuona mama amezaa watoto, nne na hana kitambulisho. Wengine mpaka sisi tuliambiwa tuende mahakamani tukahapishwe ndio wapate kitambulisho.

Tatu, ugawaji wa ardhi: ugawaji wa ardhi mpaka wahusishwe wananchi wote na sio kabila fulani peke yake, hata Tana River tuhusishwe. Wananchi ndio wanaweza amua, bila wananchi hakuna kitu.

Nne, ni sisi kabila tunayoitwa Wardehi nafikiri tunayo mambo mengi hapa. Sababu tunanyanyaswa kusema kweli. Hakuna committee katika hii disrict, na kama hakuna committee hakuna kitu hapa tunaweza kujua kitika hii district yetu ama division yetu. Kila kitu tunaona baada ya kutendeka. Serikali kama haiwezi kutuelimisha tuwe na committee. Makabila ambayo tunaishi hapa pamoja wakulima sio peke yao ndio wakulima. Sisi ni wakulima na ni wafugaji, wao pia, wawe wakulima na wafugaji sio ati wakuwe wakulima peke yake, sababu wanadai kuwa watu wamejaa. Watu wamejaa kweli, watu wamezaana waangalie census ya themanini na tisa wakenya walikuwa wangapi? na tisini na nane watu walikuwa wangapi? Hawa ambao wanazaliwa watachinjwa? kusemekana kwamba tutakaa pale pale. mifugo inaongezeka watu wanaongezeka na ardhi ni hiyo hiyo. Kwa hivyo lazima maji ya mto Tana tutumie sio ati itumike kwa mchanga peke yake, Wafugaji pia wana haki ya kutumia, wana haki --- (interjection)

**Com. Yano**: Bwana Farah umemaliza?

**Farah:** kidogo, tuna haki ya kutumia maji ya mto Tana, kwa hivyo, Katiba hiyo tuangalie sisi Wardehi, tuwe na haki kama Wakenya wengine.

Asante sana.

**Com. Yano**: Asante sana Bwana Farah, Reverend Harrison Muramba, halafu afuatiwe na Daniel Boro.

**Reverend Harrison Muramba:** Jina langu ni Reverend Harrion Muramba, Pastor wa Methodist church. Ninazungumza juu ya wanyama hasa sehemu hizi za hapa tulipo. Wanyama wa mwituni na wanyama wa mtoni. Tunaona kwamba watu wakati mwingi wanakufa ama wanauwawa na wanyama, lakini serikali haichukui hatua ya haraka. Wakati mwingine mtu anaweza kuumwa na mnyama lakini anaangaika kwa sababu hana pesa za kuenda hospitali, na serikali iko badala ya kuwa angechukuliwa kupelekwa hospitali akapata matibabu ya kutosha ili arudi, aweze kupewa zile pesa za kumsaidia, lakini hana lolote ambalo atafanyiwa. Na anaporudi nyumbani serikali haiangalii chochote juu ya huyo mtu, kwa hivyo, kama tulivyo sikia ni kwamba serikali inadhamini mnyama kuliko mwanadamu. Na hiyo tafadhali Katiba ingebadilika hapo, kwamba mwanadamu ni muhimu kuliko mnyama. Kwa hivyo iangalie hapo. Wanyama wa porini na wanyama wa mtoni wawe, kutakuwa na policies ambazo zinapasa mwanadamu awe na umuhimu zaidi ya mnyama.

Mali asili: Mapato ya mtu wa Pwani ni duni sana. Mapato ya huko Pwani ni duni, ni kitu ambacho hata akidhaminika katika Kenya nzima. Mtu wa Pwani ameachwa nyuma, nyuma, nyuma kabisa na serikali. Kwa sababu, Katiba yenyewe hairuhusu kwamba wewe ukiwa sehemu hii yale mapato yako nayo ni yapate nafasi katika nchi. Tunaona hapa tuna maembe. Si ndivyo hivyo? Tuna maembe lakini hatuna chochote, hatuna world market. Tuna maembe, tuna nazi, hizi zote imetupwa, korosho, si mtamba wa korosho umemalizwa kabisa na watu wa bara? Mtamba wa korosho watu wa serikali waliletwa hapa kwa sababu ni watu wao, hata hawaangalii habari za accounts zinawekwa namna gani kwa sababu ni watu wao. Kwamba wanawekwa pale na hawana views, yeye wanamaliza pesa, mwisho ule mtambo unafungwa na ndipo sasa sisi watu wa Pwani tunakuwa masikini kila wakati kwa sababu serikali haituangalii sawa sawa. Kwa hivyo tuna mapato kama tungepewa uwezo kama wale watu wanauza coffee, tea, pyrethrum kule watu wanaendelea kufanya mashamba yao vizuri na wanapata pesa. Lakini sisi tunawachwa hivi hivi, kama watu ambao hawana baba. Kusema ukweli watu wa Pwani ni wajibu wetu. Ile Katiba mpya lazima ifikirie kila province kuwe kuna kitu ambacho kina outside market. Hiyo itatusaidia sisi wanyonge ambao hatuna lolote huku sehemu za Pwani tuweze kuwa nasi tunaweza hata kutoka nje tukajivunia. Mtu anaweza kununua gari hata kama ana shamba lake ndogo, anaweza kununua gari. Lakini hata baiskeli inatushinda kwa sababu hatuna chochote ambacho tunaweza kuuza katika sehemu zetu.

**Com. Yano**: reverend nimekupatia dakika moja umalizie.

**Rev. Harrison**: Factories zimemalizwa kwa sababu ya ufisadi. Ni wajibu wa serikali kufikiria juu ya factories, kwamba watu wanaoandikwa kazi wawe na ujuzi wa ile kazi ambayo wameandikiwa. Sio kwamba ni mtoto wangu ndiyo nimpatie ile kazi ili aweze kufaidika.

Elimu. Kila mwanachi anao wajibu wa kujiendeleza kielimu. Tunaona kwamba watu wengi kutoka sehemu za juu ndio ambao wanaingia university, hata mtu wa hapa Pwani akiwa anakiwango kile cha kuingia katika medicine, hawezi kupata kwa sababu pale lecturerers si watu wa Pwani. Kama mtu anataka udaktari, unaambiwa hiyo uwezi kupata, na pia umeshinda kila somo, science unayo kila kitu unacho lakini hupati nafasi kwa sababu wewe ni mnyonge, kule hakuna mtu wako wa kukusaidia. Hata wale lecturers wale wa university kule ambao ni watu wa Pwani hawana say, kwa sababu wale watu wa Pwani hawana watu wa kuwasimamia katika zile departments kule. Kwa hivyo tuone kwamba Katiba inabadilika, kila mtu aweze kupata nafasi, ya kuweza kupata nafasi ya elimu.

**Com. Yano:** Asante sana Bwana Muramba. Tupe memoranada ili tukaweze kuiosoma, Salim Boro.

**Salim Boro:** Kwa jina naitwa Daniel Boro ni mfugaji. Pendekezo langu ni juu ya ardhi. Ningependa kutoa maoni yangu juu ya ugawanyaji wa ardhi hasa hapa Tana River. Wakaaji wa Tana River asilimia themanini na tano ni wafugaji na wana ng'ombe wengi sana. Na wakati serikali inaangalia au inafanya mpango wa kugawanya ardhi ni lazima waangalie masilahi ya hiyo mifugo ambao kiasi chao ni million tano. Pendekezo langu tena hapo hapo ndani. Wakati ardhi inagawanya hasa Tana River ardhi igawanywe kulingana na sub-location hadi location.

Pendekezo langu la pili, ni juu ya soko la mifugo. Serikali tunapendekeza Katiba hii mpya itafutie mifugo soko sawa wanavyo tafutia kahawa, majani, pareto na maua.

Pendekezo langu la tutu, ni juu ya project mbovu ambayo iko katika wilaya ya Tana River kama vile TARDA, Bura Scheme na Hola Scheme ambazo zimekuja bila mpangilio katika ardhi ya Tana River, zimeharibu mazingara, zimefukuza wenyewe na saa hii hakuna faida imefilisika. Napendekeza hizo ardhi zirudishiwe wenyewe, wenyewe waweze kuendelea kuthibiti hiyo ardhi. Kwa hayo machache nasema, asante.

**Com. Yano**: Asante sana Bwana Salim, mwenye anayefuata ni Abdi Nasir Gota, yuko? Abdi Nasir Gota. Councillor K. Ammed, Councillor tafadhali tunakungoja. Wewe endelea.

**Abdillahi Goja Azizi**: Mimi naitwa Abdillahi Goja Azizi. Yangu ambayo nitaongea ni kuhusu sisi watu wafugaji. Serikali ya Kenya hasa hapa Tana River wakikuja hapa Tana River hapa kwetu wakija kwa operation hakuna maneno ambayo wao wakingia yale ambayo wanaongea wanatuambia sisi ni ma-shifta, na sisi sio ma-shifta. Ma-shifta hawana number na wakiingia area hii yetu hakuna maneno wanaongea wanasena ni hawa, hawa na kutupiga ovyo ovyo.

Cha pili, kuhusu upande wa shule, kuna sehemu ambayo shule ziko na zimejegwa na serikali lakini hawana walimu. Walimu wanakula mshahara na watoto wamekosa masomo, kama sheria ya Garana college.

Cha tat, ni kama sehemu za --- naongea kuhusu serikali za GSU ya upande wa Garana college, ambao wanauwa watu wetu na marisasi kama wanyama. Na tukiwafuata kudai sisi wenyewe ni watu wa kuingizwa ndani. Sheria kama hiyo kama iko Kenya hatutaki, yale mimi naongea ni hayo tu, mimi naitwa Abdillahi Goja Azizi.

**Com. Yano:** Asante sana Abdillahi Azizi, mwenye anafuata ni Fatuma, yuko hapo? Fatuma K Mohammed, Nelie Kayumbe, halafu afuatwe na Yusuf Juma.

**Nelie Kayumbe Daudi**: Kwanza namsalimia, habari zenu? Hii Katiba kweli mumeifurahia, mbona mmekasirika kasirika? Mimi naitwa Nelie Kayumbe Daudi, mkaaji wa Garsen lakini kijiji cha baba yangu na mama yangu ni kule Gambo Viwaanda ndio kijiji chao. Lakini ninavyo omba je, wanawake, mwanamke akipata bwana, akiolewa na bwana ambaye hakumuoa na ndoa, akizaa naye watoto wale watoto hawana haki, je, akiwachana naye, akimtupia watoto ye je, anajua wale watoto atawafanya nini? Na amemharibia shule, amemharibia maendeleo yake. Mimi naomba Katiba iombe hiyo neno sana, kwa kuwa sisi wanawake tunaumia vibaya sana. Na mwanaume akipata kazi ataishi na wewe vizuri, akipata kazi akutambue tene wewe ni mwanamke nyumbani, naomba Katiba.

Na la tatu, naomba hivi, je, ikiwa mimi huyu bwana amenioa, nimeishi na yeye, ameniwacha, mbona watoto wangu wana hangaika? Wakipita barabarani wanaambiwa aah! yule wamezaliwa na mwanamke ambaye hata bwanake amemuacha, sasa wanawake wanahangaika. Naomba Katiba.

La nne, naomba hivi, mtoto wako na mtoto wangu wakikosana tukae chini tuongee, siyo unakuja na pange kunimaliza. Siyo kisasi ambacho kwetu asili tumefundishwa, naomba Katiba.

La tano, naomba hivi, ikiwa mimi na wewe tumekosana tukae chini tuite wazee, tuongee, siyo kuwa wewe unakuja na panga unataka kuniua unanipeleka polisi, iko faida gani? Naomba Katiba.

La sita, hii dakika ya sasa, sisi hii Tana River yetu. Mimi nimezaliwa hapa, nimekua hapa, najua kabila nyingi Waoroma, Wasanye, Mpokomo, sote ni kitu kimoja, kwa nini hatuelewani siku hizi? Ni kitu kinatukera mpaka tunaanza kumalizana? Kuna nini ndani yetu? Wazee wakae chini kila kabila nne hizi, tatu, kabila nne hizi, zikae chini ziongee, tunamalizana faida tutapata wapi? idap Katiba.

(Laughter.)

La sita naomba, saa hii mimi nikiwa mgonjwa, nikitembea naenda kutafuta gari ije inibebe pengine mama yangu ni mgonjwa, mtoto wangu ni mgonjwa anataka kufa. Siwezi kuondoka saa hii nifike pale feri, wako watu watakuja kunichoma. Zamani tulikuwa tunaogopa wanyama, lakini siku hizi hatuogopi wanyama ni kitu gani sisi kinachotukera, naomba Katiba, sina mengi.

(Laughter and background noise)

**Com. Yano :** Asante sana, tumeshukuru, mwenye anayefuata ni Yusuf Juma, kama hayuko Ali Bure halafu afuatwe na Peter Gilo. Ali Bure.

**Ali Bure :** Asalaam Aleykum. Mimi kwa jina naitwa Ali Bure. Kwa jina naitwa Ali Bure. Nina mengi na nina maoni ya wengine, yangu na ya wengine.

**Com. Yano**: Una tu na dakika tano.

**Ali Bure :** Tafadhali naomba nafasi. Yangu ni kwamba ninazungumza juu ya kitambulisho. Kitambulisho sisi tukiwa wafugaji hasa jamii ya Waredei, Waoroma au wale wengine wote, tuna shida sana. Kitambulisho tukiwa tunaomba kwanza tunaambiwa tuna matatizo mengi. Kwanza tunaambiwa tutoe screening card ambao kwanza ilienda kwa season tu na hatukuona office yake tena. Kitambulisho kikitolewa, tunaambiwa tutoe birth certificate ambao kwamba ilikuwa hakuna Tana River. Na wafugaji hasa katika asili mia 99 ya wafugaji ni watu wasiosoma, hawakusoma na bado hawasomi hata sasa.

Ya pili, Land Ajudication, katika land ya Tana River. Tana River, ardhi ya Tana River karibu three quarters of the land is already taken by private developers and companies and ranches. Some of the ranchers I can mention now are these: Gora National Park, ambao kwamba imechukuliwa it covers a lot of acres. ADC, Galana Game, Mchelelo National Reserve, Kitangale Ranch, Wildwater Ranch, Tanza, Burawa, hiyo ardhi yote imechukuliwa. Are you getting my point?

**(Speaker)** explain pole pole, haya majina hawa hawayajui

**Ali Bure:** Ardhi ya Tana River, three quarters imechukuliwa na watu wanasema ardhi igawanywe. Naona hapo hakuna nafasi ya kugawanywa. Tunaomba serikali au Kamishena wa land hiyo ardhi iregeshwe, Gora National Park, Galana game, ADC, Mchelelo National Reserve, Kitangale ranch, Wildwater ranch, TARDA ambayo kwamba ni kampuni ya wakulima, kuna, Gulawa salt ambayo kwamba imechukuliwa ardhi nyingi. Kuna LFD ambayo ime-cover sehemu nyingi, iko sehemu nyingi ya LFD hapa Tana River. Kipini ambayo kwamba kuna mashamba imechukuliwa na watu fulani fulani. Hizo ardhi ziregeshwe ndio ardhi ya Tana River igawanywe.

Pia job equalization: Nafikiri nafasi inayobaki ni a quarter of the land, imebaki. Hiyo haitatosha watu mpaka hiyo ardhi ziregeshwe nafikiri hakuna ugawaji wa ardhi.

La pil, wafugaji hatuna elimu, 99% of the people are illiterate. Kwa hivyo mpaka tuelimike nafikiri hatutakubali ugawaji

wowote.

Yangu ya tatu sas, job equalization: Sisi tukiwa wafugaji we are less representated, watu wetu sio wasomi, kwa hivyo nafasi nyingi hawakupata mbeleni. Na sasa wale walioko walibaki alisoma wamekuwa left over. Kenya imeenda kwa jamaa those with tall relatives and those with money, so hatuna maoni. We are not represented in the DDC meetings, tunataka recognition tuwe recognized. Some of these communities are able, the Wardehi community without code number, we have no problem we want recognision of the Wardehi community, Waoroma and infact wale waliosoma waalimu, juzi kulikuwa na fujo nyingi, waalimu waligoma, hatuna walimu katika jamii ya wafungaji. Nafikiri jamii ya wafugaji ni watu, almost 75% of the people in Tana River are the pastoralists, and we do not have even 30 teachers in Tana River, so I beg this, tunataka hata wale waliofika darasa la nane wapatiwe nafasi katika college, ili wajitolee, wasomeshe wengine ili watoke wapate basic education---(interjection)

**Com. Yano:** huko na dakika moja, jaribu kumaliza

**Ali Bure:** Niongezee tafadhali, niongezee, Elim: Ninaomba serikali itoe nomadic schools, ambao kwamba ili wale watu walioandikishwa waweze kusomesha wengine, iwe introduced nomadic schools.

Ya pili, kazi: Kazi nilizungumza, kazi sisi hatuna nafasi ambavyo hatupati kazi, hata wale waliosoma hawana kazi. Kwa hivyo tunaomba wale waliosoma, those with D minus, standard 8 wapewe nafasi katika colleges. Ili hata kama hawataajiriwa wafundishe voluntarily.

Land managemen: Ardhi ya Tana River, veterinary service imeondolewa. Veterinary service imendolewa, wakulima, wafugaji. Wakulima wanapewa huduma nyingi sana, veterinary service ilipo ondolewa ng'ombe zinakufa ovyo, hazina dawa, kwa hivyo, veterinary service ziregeshwe na katika (inuadible) ng'ombe zinatoka sehemu mbali mbali sana kama North Eastern zinakuja kupita hapa. Veterinary servant ambaye yuko ofisini anapewa tu mshahara na anatoa tu permit, ng'ombe zipite kila mahali zilete ugonjwa mwingi. Kwa hivyo tunaomba veterinary service ziregeshwe na management ya ng'ombe kupita (inaudible) ipewe kwa wenyeji, wafugaji wawe wanapewa nafasi ya kwamba watu wanaweza wakapita mahali.

**Com. Yano:** Asante sana Bwana Ali utatupatia --- hold on.

**Ali Bure**: Ya pili inawahusu nyinyi Commissioners. Moja yangu inahusu Commissioners, I will blust you. One, Commissioners function ya commission inasema hivi Cap3A part (III) inasema hivi, clearly reported that a diserving and review of social culture, obstacles that from all variant organs of discrimination and recommen, improvement to secure equal rights for all. Nafikiri hayo yote inahusu nyinyi na ambao kwamba mge-mobilise watu, from grassroot to interior watu wawe wanahakikisha kwamba culture, some of the history, the community Wardehi community or the Gala community. Kwa vile hawakusoma the above

history imekuwa imesahauliwa na hata haijulikani, kwa hivyo mgetembea kwa ndani muwe mnajua hiyo habari. The community ya Wardehi is just suffering due to this baseless history, that makes way to the --- (interjection)

**Com. Yano:** umechuka dakika kumi tafadhali wachia wenzako.

**Ali Bure:** Kwa hivyo hayo yote yachukuliwe kwa maanani (interjection inaudible) ni maoni ya wengi.

**Com. Yano:** kuna wale wenzenu walikuwa wameenda kuswali, tafadhali nitawaita make pamoja, Peter Gilo

**Peter Gilo:** Nashukuru kwa kunipatia nafasi hii, kwa jina naitwa Peter Gilo. Nilikuwa napendekeza kwamba ikiwezekana, introduction ya Katiba izingatie sana kuhusu mambo ya ufisadi, haki za watoto na umasikini, kwa sababu ufisadi umerudisha sana nchi yetu.

Na kipengele kingine ambacho ningependelea kizingatiwe ni kwamba Judiciary, ikiwezekana iwe independent, iwe Rais hana uwezo wa Judiciary kutoka Attorney General mpaka Magistrate yule wa chini kabisa, na wapewe security ya kutosha, ili wasiwezwe kutafutwa kwa njia yoyote.

Pendekezo lingine ni kuhusu mamlaka ya Rais. Ningependekeza kwamba ikiwezekana na kama haitawezekana basi Rais awe na Tume ambayo inaweza kumu-advise mambo ya kiusalama, Mambo ya kuamua kuhusu vita, emergencies. Hasiwe na uwezo yeye peke yake wa kuweza kuamua jambo hilo.

Jambo lingine ni kuhusu polisi: Tungependelea iwapo polisi wanakuja kukamata mtu, kuwe kuna offical document ambayo inatoka katika police station ikiwa ime-sign-niwa na OCS ama yule mkubwa wa kituo kile na mtu yule asivalishwe bangili ama achukuliwe kama ambaye amevuja sheria mpaka atakapopitishwa. Isipokuwa tu kwa watu ambao wanafanya makosa makubwa kama umilikaji wa silaha kinyume cha sheria, hawa wanaweza wakachuliwa zile hatua ambazo zinatakikana.

Jambo lingine ni citizenship, uraia: Ningependekeza ikiwezakana mtoto anapozaliwa kutoka zero mpaka miaka mitano. Huyo mtoto awe anaweza akawa na identity card. Isipokuwa anapofikisha miaka kumi na mi-nane identity card ile iweze kuwa na picha yake kwa sababu ameshakua mtu mzima, na pia ikiwezekana itakapofika wakati huo apate pia passport, iwe ni automatic. Kwamba yeye ni mkenya na awe anaweza kupata passport automatically ikiwa na 18 years. Kwa sababu naona wazungu wanakuja hapa bila shida lakini sisi tukitaka kuenda nje tunapata shida nyingi sana.

Parliamen:. Ningependekeza ikiwezekana katika Bunge la sasa kuwe na ile inaitwa life Parliament, ndio tujue wale wabunge tunaowatuma huko wanaongea nini. Wameongea ama wanalala, sababu wanalipwa pesa nyingi sana.

Kitu kingine ni mambo ya ardh: Tungependekeza ardhi zote ambazo ziko na dispute ikiwa ni serikali, ikiwa ni NGOs, ikiwa ni mashirika ambayo ni ya serikali. Hizo kesi ikiwa haziko kotini, zitupiliwe mbali, na pia zile ranch ambazo ni za wananchi na zimefifia na wako na madeni kwa serikali, yatupiliwe mbali na wananchi ikiwezekana waweze kumiliki ardhi hizo. Kwa hivyo kwa hayo machache. Asanteni.

**Com. Yano:** Asante sana kwa wale wenzetu walikua wanaswali, Mohamud Ahmed Gabo, halafu Abaloni Racha Abaloni afuate, na pia Abaloba Barisa Abaloba ajitayarishe.

**Mahamud Ahmed Gabo**: Kwa jina naitwa Mahamud Ahmed Gabo. Jambo langu la kwanza ambalo ninaliongea hapa, ni kwamba kabila la Wardehi tunataka lipate recognition and given a code number.

Jambo la pili ni kuhusu passport. Sisi waislamu, kwa upande wa passport sisi tunakua discriminated, maanake tunakua screened, kuwa jina lako tu likisomwa jina ni la muislamu unakua huwezi ukapewa passport, kwa sababu unakua screened ili ujulikane wewe ni mkenya alisi ama la.

Jambo lingine ambalo hapo tunataka waislamu wapewe usawa na wale wengine ili waweze kupata passport. Jambo lingine ni kwamba katika koti ya waislamu Kadhi's Court uwa haina High Court, tuseme ni katika District level ama ni magistrate tu anakua kama magistrate. Kisha tunahitaji pia hiyo koti ya waislamu iwe na High Court. Kadhi's court iwe na high court. Jambo lingine ni kwamba, pia tunahitaji kuwa na Court of Appeal katika Kadhi's Court, isiwe mtu hawezi kuwa na appeal katika koti la Kadhi. Tunaitaji kuwe na Court of Appeal katika Kadhi's Court.

Jambo lingine ni kwamba, kuna sehemu ya ardhi ambayo katika Tana River imekuwa grabbed, yaani tumepokonywa na watu matajiri, ama wakubwa katika vyeo vya serikali. Hio ardhi tunataka irudishwe kwa mikono ya wananchi, ili wananchi wafaidike na iyo ardhi. Ardhi kama hiyo ni sehemu kama Galana ambayo ilikuwa ni sehemu ya malisho kwa wafungaji na imechukuliwa na ADC ambayo ni kampuni ama ni shirika la serikali. Tunataka hiyo Galana ranch irudi kwa mikono ya wenyeji ili wafaidike nayo na wawe wanaweza kuitumia iyo ardhi kwa malisho. Tunasema ardhi igawanywe wakati ardhi yetu yote imeporwa. Ardhi nyingine iliyoko katika mikono ya watu wapepari ambao wamechukua, ni kama ardhi ya Kurawa Holding Ground.

**Com. Yano**: Tafadhali harakisha

**Mahamud Gabo:** Kurawa Holding Ground imechukuliwa na hivi iko katika mikono ya watu binafsi. TARDA ambayo ni kampuni ama ni shirika ambalo limefifia, tunataka ifufuliwe na watu wapewe lease ya kutumia iyo ardhi, ili wapate kulima

wenyewe na sio shirika la TARDA liweko, tunataka irudi kwa wenyeji na wenyeji wapate kulima hiyo ardhi.

Jambo lingine ni kwamba MP anapochaguliwa na kwenda bunge ikiwa kuna hoja ambazo ziko bungeni na wenyewe huku hawajui kwamba hoja hizo zinapasishwa katika Bunge kwa sababu zao, na wao tunataka huyo mbunge aje kwao, aje kuchukua maoni aone hilo jambo ambalo linatakikana lipitishwe bungeni kama sheria linawafaa hma haliwafai. Kabla halijakua sheria na kupitishwa bungeni kule.

Jambo lingine, ni kwamba hali ya maisha ya watu hawa wafugaji ambao wako katika sehemu hii, wana hama hama. Hilo jambo la kuhama hama tunataka litiwe katika sheria na liwe jambo ambalo linakubaliwa. Kwa sababu sehemu ambazo kuta-fit ama mambo fulani yamefanywa katika hali ya maisha ya ufugaji kama ranches. Kwa vile ng'ombe zao zinakua restricted hazitembei kwenda kulishwa, wametuishia hizo ranches zote zimefifia. Lakini ile life style, maisha ya uhamiaji, wale wanaotumia mpaka sasa, hayawali ama ng'ombe zao bado zingali ziko na zinatumika ama wenyewe wanapata faida kutokana nao, kwa hivyo hii maisha ya kuhama hama katika Katiba hii tunataka ichukuliwe kama maisha.

**Com. Yano:** Yule mwingine ni Abaloni Racha Abaloni

**Abaloni Racha Abaloni**: Asante Kamishena. Makamishena's mimi maoni yangu. Jina langu ni Abaloni Racha Abaloni. Unanipatia dakika tano najaribu kufupisha.

Economy: Maisha ya mwanadamu yeyote inaambatana na uchumi. Kama mwanadamu hana uchumi, yeye ni masikini hakuna maisha. Katiba iliyoko saa hii Makamishena's imeonea sana wafugaji katika hii nchi. Katiba iliyoko saa hii imependele sana wakulima. Kila mimea inatoka katika ardhi ya Kenya iko na board yake, Pyrethrum Board of Kenya, Coffee Board of Kenya, kila mimea iko na board, lakini hakuna board hata moja ya mifugo. Ile iliyoko ni ya KMC na yenyewe imeuwawa. Kwa hivyo Makameshina's kuinua hali ya wafugaji katika Tana River na Kenya nzima kwa jumla, Katiba hii ya sasa mpya tunataka hivi; Wizara ya mifugo itungwe peke yake isichanganywe na wizara ya kilimo, na Minister incharge wa hiyo Ministry pamoja na Parmanent Secretary incharge wa hiyo Ministry atoke katika jamii ya wafugaji, ndio tutasaidika.

Makamishena's kuhusu security, wilaya hii imeharibiwa jina, inaitwa operation area. Operation area tafsiri yake ni unyanyasaji. Wakati mambo yanaharibika askari wakija katika operation area wamepata advantage wanfanya kila aina ya uchafu. Mtoto anapigwa, mbuzi yetu inachinjwa kwa nguvu, ng'ombe inachinjwa kwa nguvu, wasichana wetu wananajisiwa kwa sababu ya operation area. Kwa hivyo, hili neno operation area ijapo liko liondolewe na imeitwa operation area Tana River kwa sababu wafugaji wanaishi hapa, kama wafugaji hawako hapa Tana River haingekua operation area. In Nairobi saa hii sio operation area lakini watu huko hawalali, polisi wanauwawa, matajiri wanauwawa, nchi inaibiwa usiku na mchana lakini Nairobi haitwi operation area. Tana River ambayo inatokea such cases kila baada ya mwezi mmoja, miezi mbili wanadamu wanakufa inaitwa operation area. Hilo neno operation area tunataka Katiba mpya iangalie.

Kuhusu local government: Local government, tunataka central government iwapatie uhuru waendeshe mambo yao, isingiliwe na serikali, na chairmen na mayor katika hii Katiba ya sasa tunataka wachaguliwe na wananchi direct. Na madiwani walioko saa hii na wale ambao watakuja baadaye, wasilipwe na ushuru kutoka kwa wananchi, walipwe na central government direct, au wawe chini ya Parliamentary Service Commission. Ule ushuru unapatikana kwa wananchi na ufanyie huduma wananchi wa Tana River.

(Clappings)

Jambo lingine Kamishena's, watu wote ambao wanapigiwa kura kuanzia President, Mjumbe na Diwani, tunapata taabu kupiga kura sisi watu wa Kenya. Tukipeleka mtu kama Councillor au mtu kama mjumbe huyu mtu hatumuoni tena, mpaka baada ya miaka mitano, kwa hivyo, Katiba hii mpya ya sasa, itupatie sisi uhuru wapiga kura, kama mjumbe hatahudumia wananchi wale waliomchagua asilimia sitini na tano wapiga kura katika hio area wakisema No, by-election iitishwe twende kwa fresh elections.

Kingine, wajumbe wa Bunge, wanajipandishia mishahara ki holela holela hatuelewi ni uwezo gani, ni sheria aina gani sisi hatuelewi. Mjumbe saa hii anakula zaidi ya shilingi laki sita na bado kuna Kamishena wanazunguka wanachukua maoni wanataka huu mshahara usukumwe mpaka ufike million moja, sasa basi, kama wafanyi kazi wale wa kawaida, wa chini anapata mishahara - juzi katika labour day, mfanyi kazi wa mwisho unasikia anakula elfu mbili mia tano. Mtu moja, mwanadamu moja anakula zaidi ya laki sita na bado wanataka hii mishahara isukumwe mpaka ifike million moja. Hatuelewi sisi hapa mashinani kwa ground, mwananchi wa kawaida, uwezo aina gani wako nao wajumbe kujipandishia mishahara ki holela holela mpaka inafika mwanadamu moja anakula one million shilling. Sisi hatuelewi, tunataka Katiba ya sasa iangalie hayo maneno. Ma-bwana Kamishena's leo ni Friday katika Katiba hii sisi tulikuja tukaandikisha majina hapa tumekwenda msikitini tumekuja saa hii kutoa maoni. Siku ya Ijumaa ni siku takatifu kwa waislamu, kwa hivyo kutoka sasa, kutoka saa hii, na muandike maoni yetu hapa leo saa hii, Katiba hii mpya, area yote ambayo imekuwa dominated na waislamu, siku ya Friday mkutano wowote usifanyike. Ile ni siku muhimu sana katika calendar ya waislamu, waislamu wapate nafasi ya kupumzika siku hiyo.

Kingine, kuna kitu kinazungumziwa. Kinazungumziwa mahali kwingi na sasa imekuwa ni lazima na hakuna budi lazima sisi kama wazazi tuzungumze, kuhusu kutahiri wasichana. Mambo ya kutahiri wasichana ni makosa, hata kwa dini yetu ni makosa, na hakuna dini inaunga mkono. Kwa hivyo tunasema saa hii, iwekwe katika Katiba ifanywe mkazo ile jamii ambayo ni lazima wasichana watahiri, Katiba ya sasa iangalie kwamba wasichana wapewe uhuru, vile Mungu ameumba kwa vile hakuna matatizo kwa dini wawe vile vile.

Kuhusu ardhi, nyamazeni, kuhusu ardhi, sisi wafugaji wa wilaya hii, tumeeleweka vibaya. Tunaambiwa kwamba sisi tunapinga

ardhi ati kwa sababu ng'ombe zetu hazina malisho. Wakaaji wa wilaya hii ambao ni wafugaji hawapingi mambo ya kugawanya ardhi, lakini tunataka civic education kubwa vile mlivyo tufanyia sisi kabla ya nyinyi hamkuja. Kuwe na shirika maalum, serikali iunde shirika maalum ambao inapatia elimu raia vile mlikua mkitupatia elimu mbeleni kabla hamjakuja. Watu waelimishwe faida na hatari za ugawaji wa ardhi au umilikaji wa ardhi katika wilaya hii, kwa sababu, nasema hivyo kwa sababu watu wengi hawaelewi faida ya land adjudication ndani ya hii wilaya mpaka saa hii. Kwa hivyo, kujua ile faida na asara, kuwe na civil education proper, thorough kila kijiji kama huyu bwana co-odinator alikua akitufanyia mbeleni kabla hamjakuja, wafugaji na watu wengine ambao wanaishi katika wilaya hii, wafundishwe faida na hasara za land adjudication.

Kingine bwana Kamishena's. kuhusu elimu, wafugaji wana shida kubwa sana kuhusu elimu. Tafadhali tunaomba katika hii Katiba mambo ya elimu ile area ambayo ni ya wafugaji kuwe na mobile schools. Wakati mvua inanyeshwa watu wana hama shule ifuate watu. Walimu wafuate watu, mobile education.

(Clappings.)

Wale waalimu ambao wanafundisha area kama hasa Warenda, Wayu, Chefiri na Angofa, kuwe na mobile schools, inawezekana Wamaasai wanafanya msicheke. Watu mvua ikinyesha wafugaji wakihama shule ifuate wafugaji, mobile classes, na area ya wafugaji tunaomba Katiba ya sasa, katika area ya wafugaji ambayo iko mbali na town kuwe na Nomadic Primary Schools.
Asanteni.

**Com. Yano:** Asante sana bwana Abaloni. Mwenye anayefuata ni Abaluma Barisa, yuko? Tunaendelea Hussein Fayu, Hussein Fayu alafu Mohammed Genyi.

**Abdi Hussein Yusuf Fayu**: Kwa jina naitwa Abdi Hussein Yusuf Fayu. La kwanza kusema ni juu ya ardhi. Ardhi tunataka ifanywe, serikali irudishe ardhi kwa mikono ya wananchi kwanza, kisha ardhi watu wanasema wafugaji na wakulima. Hapa Tana River panaishi kabila saba, kabila saba, na kila kabila ni wafugaji na ni wakulima, kwa sababu wapokomo wako nazo ng' ombe, mbuzi na kondoo. Baadhi yao ni wakulima, Marakoti ni hivyo hivyo, Moyaya hivyo hivyo, Bajuni hivyo hivyo, Wardehi na Oroma ni hali kadhalika ambapo ni wafugaji vile watu wanaelewa, lakini wote ni wakulima na wafugaji. Hapo basi wakulima ni wote tena Wardehi wanalima, Wapokomo pia ni wakulima, Wamarakoti pia ni wakulima, kila mmoja ambaye ni mkaaji wa hapa Tana River ni mkulima. Kwa hivyo hakuna tofauti mtu kusema kwamba wakulima na wafugaji, mpaka wataje jina kabila fulani waseme, wakisema kabila fulani, ndio sasa watu wataelewa kwamba kabila fulani ndio wafugaji ama wakulima. Kwa hivyo ardhi kugawanywa hivi hivi kuna ma-hectares ya range mengi, watu wamechukua ardhi. Kwanza waregeshe hiyo, kama Gritu range**,** kama LMD, Kurawa, kuma nyingi wakiregesha hapo ndiyo pengine tufikirie lakini mpaka watu waelewe kugawa ardhi ni nini, ama mpaka watoto wasome waelewe ni nini, hakuna cha kugawa ardhi, yaani maoni yangu mimi mpaka miaka hamsini ijayo, hakuna cha kugawa ardhi.

**Com. Yano:** Tafadhali tusikie.

**Abdi Hussein:** Tunaingia kitambulisho, Kitambulisho kusema ukweli watu wa kuhama hama ndio wako na shida, hasa Wardehi wako na shida sana. kwa sababu kila wakati watoto wanatafuta kitambulisho, wanaambiwa leta card ya screening ambapo sisi hatujui imetoka wapi, Somali screening. Na kuna wengine walichukua form kutoka 1998 upto now wako nazo, form na hawajapewa kitambulisho. Na kila kitu kikitengenezwa kinapelekwa Nairobi, kinarudishwa tena, hapo wafanya makosa. Wale makarani wanaruka majina ya babu ama baba, kisha baadaye inaregeshwa inasemekana kwamba kitambulisho chako kimekosekana kitu fulani. Kwa hivyo kwa miaka nne wengine wako na form, hawana kitambulisho, wanahangaika, na wengine wanaambiwa walete birth certificate ya babu.

**Com. Yano**: Hussein dakika moja.

**Abdi Hussein:** ngoja dadangu bado. Haya, education: Nataka education ifanywe kilazima, kwa sababu hapa kijijini ukienda, vijana wanaranda randa, wengine hawana baba, sasa kama serikali ingesaidia ingeleta elimu ya bure, kila mtoto angeenda kusoma. Sasa tunaomba serikali ilete elimu ya bure kama zamani na watoto wawe ni lazima waende shule.

La nne, naongea juu ya KPR, KPR ni askari lakini watu hawawatambui. KPR tangu ilipoletwa, habari ya wagaidi imepungua na KPR saa yote wao wako kijijini. Ni watu ambao sasa wanalinda kijiji, hao watu wanastahili walipwe pesa na bunduki zao zidhibitishwe na risasi wapewe nyingi, kwa hivyo serikali iangalie KPR wapewe mishahara na wapewe ofisi zao za binafsi. Wakati wakikuja ama ukipeleka malalamishi yako uende kwa ofisi sio kuja na kuhangaika huku na huko, kwa hivyo serikali iangalie hapo KPR wasaidiwe kwa pesa na hiyo mishahara yao. Asante.

**Com. Yano**: Councillor Hassan Omar Gurutumu, karibu.

**Councillor Hassan Omar**: Madam Kamishena, nashukuru serikali kwa kubaliana kwamba --- Jina langu naitwa Hassan Omar Gurutumu na pia mimi ni Councillor wa hapa Garsen na pia ni sub-branch KANUchairman wa Garsen. Nimeshukuru serikali kwa kukubaliana ya kwamba ibadilishwe ile Katiba tuliowachiwa na wakoloni. Ya kwamba sisi wenyewe ndio kama wananchi wa Kenya tuunde Katiba yetu kama tumejitawala na serikali na uhuru wetu wakenya. Kama hii ni ya kupendekeza Katiba mpya na kutoa maoni, cha kwanza hosptali ndiyo maisha ya binadamu ya kwanza. Nimependekeza juu ya hospitali, medical officer, ama ma-officer wowote ambao ni watumishi wa umma, anafanya kazi ya hospitali na ako na clinic yake, aondoe hiyo clinic yake, kwa sababu wanaiba dawa za serikali za kuuza kwa clinic zao binafsi. Kwa wakati huu hakuna mwananchi ambaye atawaipita huduma kutoka kwa hospitali, wa division ama district, kwa sababu yule mu-officer ana hospitali yake na hakuna controller, yeye mwenyewe ndiye controller na mwenye biashara ni yeye. Ningependekeza kwenye Katiba mpya wasikubaliwe wafanyi kazi wa serikali kufanya clinic zao binafsi, katika area yenye wanafanyia kazi.

Ya pili, watu wanalia na wanapendekeza kugawanywa kwa ardhi ama kusema ya kwamba baadhi ya wakaaji wa Tana River watolewe kwa area ya mto iwekwe nje. Hiyo nafikiri huyo mtu hakupendekeza haki kwa sababu mto wa Tana River hakuna mwenyewe ambaye yuko na Title Deed. Amepewa na Mwenyezi Mungu, kwa sababu niwa ya kila mtu, ya Kenya sio watu wa Tana River. Kwa sababa nimesema hivyo kutoka North Eastern ama Tana River wako na wafugaji, kwa jumla wakenya hakuna wakenya wowote ambao wako Kenya hii hawaishi gigiri ya huo mto wa Tana River, wanalima na wanafuga mifugo yao ya kila aina, kama ngamia, ng'ombe na mbuzi na kondoo, hata kuku. Na saa hii mkichunguza gigiri ya huo mto, ng'ambo ya pili na ngambo hii huwezi kupata watu ambao wanajidai wako na shamba, hakuna mtu ako na shamba ya acre mbili ama acre tatu ambayo anavuna na anapanda. Mbali tu anataka mzozo wa kutaka kupinga mfugaji aondekewa hiyo area na sijui atapelekwa wapi. Mahali palitajwa kusemekana hapo ndio panafaa papelekwe mfugaji, hata wanyama huwezi kulishwa kwa sababu ya jua na ukame, nani ataisha mahali saw?. Kwa nini mamba na kiboko na nyati hawapendi hapo pahali? Binadamu wataishi kivipi? Hii haileti uhusiano kati ya watu, wataleta mzozo kama na wale wakaaji wa Tana River lazima kila mmoja ambaye ako na akili na hekima wakubaliane kuishi na mwenzake. Tangu ukoloni ng'ombe wako, mbuzi wako, shamba iko, wazee wako, ng'ombe kama zinaingia kwa mashamba wazee ndio wanasuluhisha, wanatatua kwa wakati huu ndio utapatanisha.

Ya tatu, habari ya kitambulisho. Madam Kamishena, tunajua kutoka ukoloni uondoke hapa, Kenya iko na Katiba moja lakini kwa nini serikali yetu ya Kenya imekubali iwekwe na Katiba ya mtu binafsi, ambaye anasikilizwa na baadhi ya wananchi na kusemekana screening, screening ni kitu cha Wasomali. Hiyo screening ni ya mtu binafsi, hata katika Katiba ya Kenya ambayo ilituachia ukoloni, Madam Kamishena kitu kama hicho wasikubaliane katika Katiba mpya, mtu aunde sheria yake mbali ibaki ni Katiba ya Kenya. Na tunaomba ikiwezekana hiyo screenig (inaudible) hata msingojee mda wa kurekebisha Katiba, iondelewe mapema hiyo, kwa sababu hii ni sheria imewekwa na mtu binafsi.

**Com. Yano:** Maliza, maliza tafadhali Councillor.

**Cllr. Hassan Omar:** Tafadhali, kodogo nisamehe, naomba nisamehe, kodogo. Watu wanaongea habari ya mbunge na madiwani na mapato. Madiwani ni serikali ya pili, ni local government, lakini madiwani mshahara ambao wanalipwa, ofisi zao hata hawalipi wale wafanyi kazi wa kujenga na hali ni serikali ya pili. Baadala ya hizo pesa wabunge ambao wanalipwa ipunguzwe ilipwe madiwani, sasa ndio wanatetea wabunge wapatiwe one million kwa mwezi mmoja na hao ndio wanakaa na shilingi elfu tatu kwa benki kwa mwezi. Na hiyo ni ajabu kwa watu ambaye wa (inaudible) na hana mamlaka katika ward yao. Wapate uwezo katika ward zao madiwani.

Madam Kamishena wa Kenya wengine, wamekubaliwa kupewa na (Inaudible). Tana River mkitoka Pwani kutoka Kipini kwenda Kora mwisho wa Tana River hata ndege itachoka, kwa nini serikali ilikataa kugawanya ikuwe district mbili ibaki Warendai na Waoroma. Hii serikali yetu sasa ndio imetuumiza kama sisi watu wa Tana River.

**Com. Yano:** Asante sana, Bwana Councillor nafikiria umeshanena mengi.

**Cllr. Hassan Omar:** Kidogo imebakia, agenda moja ndio nimalizie. Wafugaji, mifugo ya Tana River haina huduma kutoka kwa veterinary. Wakati huu ukienda hapo Garsen ofisi ya veterinary, kuna officer mmoja na hakuna dawa aina yoyote ambayo ni ya kutibu ng'ombe. Na huku tunajiita hivi na serikali iko na Katiba, iko na wizara fulani za mifugo na hawashughuliki na ng' ombe kama wanakufa ama maradhi gani yamezipata. Nataka wale ambao hawatumikii mifugo katika wizara ya mifugo tunataka watolewe. Na serikali iwapatie uwezo mali, fedha ya kutoshana kutoa huduma kwetu sisi. Hapo ndio nimemalizia mimi.

**Com. Yano:** Asante sana Councillor Hassan mwenye anayefuata Councillor Said Sadiki, yuko? Said Sadiki endelea.

**Cllr. Said Sadiki**: Madam Kamishena mimi naitwa Said Sadiki, Zera Location. Nimeondoka hapa mengi bwana Karasinga ameyaongea na ma-councillors wengine wameyaongea. Mimi sina maneno zaidi, mbali nadokeza kwako Kamishena mambo ya mipaka, hii ambayo tumepewa na wakoloni. Upande wetu wa pili ambako kunaitwa sehemu ambayo inaitwa Barathiro, huko sasa mambo hayo nimeona mimi mwenyewe ya naingiliwa zaidi sana, sana, sana, watu wengine ambao sehemu yao ni ingine ya Ijara wanaingia huko, wanachimba visima, wanajenga mashule, nakimbia naenda kwa DC sipati lolote, nakuja kwa DO sipati lolote, kwa hivyo Kamishena mimi ninaomba mipaka iwe ile ile ya wakiloni maana serikali hii tumepewa na wakoloni.

(Laughter)

Na hayo mambo chini yake kuna mawaziri fulani ambao wanakaa kwa ofisi ya mzee ndio ambao wanafanya mambo hayo.

**Com. Yano:** Tafadhalini tumpatie huyu mwenzetu mda aongee, kama unataka kuondoka, ondoka pole pole wachakupiga kelele.

**Cllr. Said Sadiki**: Sisi watu wa Tana River ni watu wa amani. Mgeni pia tukimuambia karibu anataka kutuondoa kabisa kwa sahani ale yeye. Lakini sisi ni watu wakustahimili. Lakini leo Kamishena wamekuja hapa ninakueleza hiyo shauri ya watu wengine kuchukua sehemu ya watu wengine, mambo kama hayo myapeleke yabadilishwe ili tuwe na idadi ile ile ya zamani ya wakoloni ndio tumeamini, maana wakoloni wametuachia serikali hii tuendelee sawa sawa.

Na swali lingine naomba, kama inawezekana kutoka leo Madam Kamishena, uandike hapo ukifika Nairobi iwe agenda ya kwanza. Sisi watu wa wilaya ya Tana River serikali imetusahau na sasa tunataka barabara. Jana nilitoka Hola saa kumi na moja kufika hapa pamoja na bwana DO mimi nimekua mgonjwa hivi najaribu kuzungumza siwezi. Kwa hivyo Madam Kamishena hiyo barabara itengenezwe mara moja iwezekanavyo, kwa sababu na sisi pia ni watu wa Kenya tunachangia kila

kitu na kutoka Kokani mpaka Hola sio mbali, kwa hivyo ninaomba barabara itengenezwe mara moja. Madam Kamishena mimi nina mengi lakini nilienda kuswali nimerudi saa hii. Hapa tulipokaa sisi kama jua limekuchwa huwezi kuona huko wala huku ni giza, Madam Kamishena naomba mengi kina Bwana Karasinga wameyazungumza lakini naomba taa. Tana River maji yetu yamekauka ya mtoni kwa sababu ya Kindaruma kuchukua maji yetu na kuyapeleka huku na huko lakini taa hatuna, kwa hivyo Madam Kamishena ninaomba serikali itupatie taa wilaya ya Tana River hata kule Mnazini nami pia nipate taa. Maana usiku ukija madam Kamishena nitakukaribisha wewe kama mgeni mheshimiwa.

Mimi naomba wanaume wasiwapige akina mama, lakini akina mama pia noa wasiwapige waume, tunataka amani wakati huu ambao tunajenga serikali mpya ni sawa au si sawa?

**Audience:** Sawa.

**Cllr. Said Sadiki**: Kina mama pia watuheshimu, ni sawa?

**Audience:** Sawa.

**Cllr. Said Sadiki:** Pia naomba madam Kamishena vijana wapewe nafasi na wao, ambayo kwa vikundi vyao vipatiwe pesa. Madam Kamishena wilaya ya Tana River hatupati mikopo hata ile midogo midogo ya vioski, kwa hivyo ninaomba tupatiwe mikopo kama mimi nina duka lakini sipatiwi mkopo na nyumba yangu inapata dhamani yake, million mbili dhamani ya ile nyumba maana nimejenga na block. Wakati wa mzee Kenyatta mwaka wa sabini na nne na mimi ni Councillor kutoka Kenyatta mpaka leo.

**Com. Yano**: Asante sana Councillor Said Sadiki, ulituahidi sisi ya kuwa hukutaka kuongea mengi lakini inaonekana wewe ni mwana siasa. Kuna tangazo tafadhali tulieni.

**Omar:** Wananchi wa Garsen ningependa tukae na wageni wetu mpaka mwisho. Tuko na matangazo ambayo yanawahusu nyinyi muhimu sana. Kuhusu mipango baada ya kumaliza mkutano. Kwa hivyo ukiondoka si vizuri, tumeanza vizuri tumalize vizuri. Tukae chini mpaka tuwasikilize wale watu wawili, watatu ambao wamebaki ndio tufunge mkutano, tafadhali msiende tuko na matangazo muhimu baada ya mkutano. Asanteni.

**Com. Yano:** kuna Bwana Sheikh Giresi Bakero.

**Sheikh Bakero**: Nimefanya take over. Mimi kwa jina ni Sheikh Giresi Bakero chairman wa CIPK Tana River. Maoni yangu katika Katiba nifanye haraka haraka kwa sababu ya madika. Ya kwanza kama ninavyo jua kwamba Katiba ya Kenya haina ma kitangulizi, hii napendekeza iwe na kitangulizi chenye kufaamika kabisa.

Ya pili, naomba Katiba ya Kenya ama napendekeza iandikwe kwa lugha tatu, ili wananchi wote wajisomee wenyewe, kwa lugha ya Kizungu na Kiswahili na Kiarabu ikiwezekana. Hizo lugha tatu ndizo lugha zinazotumika katika Kenya.

Pia napendekeza katika Katiba hii mpya inaandikwa, power ya Rais ama uwezo wa Rais upunguzwe kwa asilimia hamsini. Iwe Rais atakua chini ya sheria, akifanya kosa lolote aweze kupelekwa kotini.

Pia ninapendekeza Kadhi's Court. Viongozi wa makadhi wasichaguliwe na serikali mbali wachaguliwe na viongozi wa dini, committee wenyewe wa dini wakae chini kuchagua makadhi, yule ambaye anajua uislamu sawa sawa, siyo serikali ichague Kadhi.

Na pia tunapendekeza tuwe na High Court ya waislamu, sio hatimaye Kadhi anahukumu baadaye file inatolewa kwake inaenda kwa High Court ambayo haikumu Kiislamu vile inatakiwa.

Pia napendekeza Rais katika uwezo wake hasiwe na uwezo wa kumchagua yule mbunge ambaye amesimama kwa election akaanguka, wananchi wenyewe hawamtaki, amchague mbunge maalumu kisha ampatie wadhifa wakati wananchi wenyewe hawamtaki, achague yule mtu ambaye ana bidii, mtu ambaye ana julikana na hajasimama kwa mambo ya siasa.

Pia, ninapendekeza makamu wa Rais katika hii Katiba mpya ikiwa Rais ni mkristo, makamu wa Rais awe muislamu. Ikiwa Rais ni muislamu makamu wake awe mkristo.

Pia, ninapendekeza serikali ya jimbo kwa sababu huduma na maendeleo zitakuja karibu na wananchi. Ninapendekeza kama nilivyo omba hapa mbele yangu, siku hii ambayo ni ya Friday huwa ni siku bora takatifu kwa waislamu, hivyo hivyo tunaheshimu siku ya juma pili kwa wenzetu pia, siku hizi mbili zisiwe na agenda yoyote ya mkutano kwa wananchi.

Yangu ya mwisho kabisa, ninapendekeza ya kuwa wale waliochagua wabunge, ikiwa mbunge ameonekana kwamba ni mtu hatekelezi ile jukumu yake aliyopewa, wananchi wawe wanaheshimiwa, ile people political power, sauti yao iheshimiwe, wawe na uwezo wa kuweza kumuondoa kwa Bunge kabla ya hiyo miaka mitano ingine. Asante sana.

**Com. Yano:** Asante sana.

**Konde Hashako:** Asante sana Bwana Kamishena's. Jina langu naitwa Konde Hashako. Mambo ambayo nataka kuyazungumzia ni protection of fundamental rights na freedom of individuals. Hii ni haki ya kikatiba ambayo ingefaa ipewe nguvu zaidi. Kwa mfano, minority communities kama wafugaji kama Waoroma hivi na Wada, Wardehi and the rest wanapata shida sana. Particularly sisi watu wa Tana River hii sheria ya mtu kuwa arrested na anawekwa remand over 24 hours for ordinary offenses or for over 14 days for capital offense, kama vile Katiba inavyo zungumzia haifanyi kazi huku kwetu, kabisa.

Mtu anashikwa pengine for ordinary offenses anawekwa for almost 3 months at remand bila kufikishwa mahakamani kwa sababu hii area yetu inaitwa operation area sijui under presidential decree and I don't know what. Kwa hivyo iondolewe kabisa, na hii issue ya protection of fundamental rights isiwe suspended.
Freedom of fundamental rights isiwe suspended hata kama nchi iko kwa vita, pengine mara nyingine serikali inakua na uwezo wa decree property za wananchi, kwa sababu (inaudible) whatsoever hata kama serikali imefanya kitu cha aina gani isichukuliwe mali ya wananchi ati kwa masilahi ya state.

Jambo lingine nataka kuzungumzia ni system of governance na land issues. Waoroma as a minority community have preferred federal system in 1962 in lancaster house conference on the Constitution through their legislator (inaudible) Tana River. They had proposed the federal system to protect their land from being taken over by the bigger communities. Therefore, immediately after independence Constitution imekua changed in 1964 na ikafanywa unitary system, ambayo ime-supress the rights of minority in Kenya. Kwa hivyo tunataka hiyo majimbo irudi so that the minority in Kenyan society haki yao, kwa mfano, Tana River (inaudible) for each individuals or persons of Kenya, have acquired thousands of acres of each plot in Tana, even before it has been announced an adjudication area, that is very wrong, it is (inaudible) of the highest order.

Issue ingine ambayo nataka kuizungumzia --- (interjection)

**Com. Yano:** You have only a minute.

**Konde Hashako**: Please. Citizenship of the minority particularly the Oroma, we are facing a very big problem in the acquisition of ID cards, Passports, Birth Certificates a lot of people (inaudible) just because and we don't know whether they are wrong, because of our case of being Muslims. Because over one million fall in North Eastern thus are accused of terrorism. Western propaganda. So tunataka haki iangaliwe.

The other issue is on local government: At least the Councillor should have education level of standard 8 and above, so that ataweza kujisaidia katika kazi yake. And at least, we should also have a Constitutional Court so that the rule of law should be taken care of as the watchdog of the public. Constitutional Court as the watchdog of the public, because we can today have a very nice Constitution but the government in power will never take that into considertion. A Constituional Court has to be given priority. The issue in the Kadhi's Court should be given a and also the Court of Appeal.

Land adjudication should not take place until pastoral land issues are addressed seriously in the new Constitution, because the present Constitution from the colonial has been enacted to favour the interest of farmers and has nothing to do with the interest of pastoralists. Therefore, there should no land adjudication particularly in Tana River District until pastoral land issue have been seriously addressed in the new Constitution.

**Com. Yano:** Thank you very much councillor, now I am going to hand over to my fellow colleague Commissioner so that he can wind-up.

**Com. Kangu**: Watu wa Garsen tunataka kuwarudishia shukrani kwa maneno ambayo mumetueleza. Tumekaa tumesikiza, mumezungumza mambo mengi, mengine na uchungu sana, ndiposa nimesema nizungumze machache kabla hatujamaliza. Tukisema tunataka kutengeneza Katiba sababu ni kwamba tunatafuta kila mtu apate nafasi ya kuendelesha maisha yake ya kupata cha kukula na kitu chochote anachotaka ndio aendeleshe maisha yake. Na ikawa, mara nyingi uwa maisha imefika kiwango cha wale wanaojiweza na wengine wanawachwa nyuma ndio binadamu wanasema hapana tutafute njia ya kuwafikisha hata wale hawajiwezi wapate nafasi ya kundelesha maisha yao. Ndio nikisia mkizungumza kuna wale wanasema tunataka mfumo wa Majimbo sababu tunaona pengine yale makabila makubwa yametuwacha sisi nyuma. Na mimi naona hiyo ni sawa sawa lazima tuende pamoja. Lakini baada ya nyinyi kusema hivyo, mkirudi sasa nyumbani Pwani mimi nasikia inakua tena wapokomo, waoroma, wardehi, sasa mimi nashindwa kama mnalia kwa nchi nzima tumewachwa nyuma tuko wadogo na hapa ndani nanyi mnataka kuacha wengine nyuma, ni sawa sawa kweli? Si hio itakua makosa. So ikiwa tutatengeneza Katiba ya kuendelea sawa sawa lazima tutafute tutafanya namna gani mahali tumepata tumekaa na wenzetu, tutafute mbinu ya kuishi, kila mtu apate nafasi yake bila kukanyagana miguu na kuumiza mwingine, si hiyo ndiyo itakua sawa sawa? So, mjaribu kufikiria kuzungumza ni namna gani tutafanya kama sisi ni watu wa Tana River tukubaliane tutakaa namna gani. Mama alikuwa anazungumza hapa akisema, hata wale wanalima kuna wakati wanataka nyama ya kukula ugali nayo, si ni kweli? Na wale wanyama saa ingine wanataka ugali, so we depend on each other, na nafikiria pengine haya mazungumzo ya kutengeneza Katiba inasaidia watu kuanza kujifunza kukubaliana kuishi na wenzao. Inasaidia kwa sababu sasa mnazungumza kila mtu anasikia uchungu wa mwenzake na nafikiria pengine mtafuatilia sasa hata kama sisi hatujafanya Katiba wenyewe mnasema sisi ni watu wa hapa tutafanya namna ngani, tuishi pamoja kwa usalama. Yule wa ng’ombe asipeleke kwa mimea ya mwenzake ikule na wa mimea tutapata, ndio nao hao waweke ng’ombe lazima wapate maji. Pengine tungekuwa tunasema okay kama watakaa huko tutafanya namna gani tupate serikali iwachimbie maji huko ya kunywesha ng’ombe zao, si hiyo itakua sawa sawa. Lakini tukisema tu, hapana leta nao lazima ng’ombe ikunywe maji unapata tunaanza kufurungana, si ni kweli? So I hope mtaelewana tuona namna gani.

Na wamama wamezungumza nikasikia nao wanazungumzia mambo sana ya wanaume kuacha wamama na watoto, I the hope, men walisikia wataangalie hayo maneno, sawa sawa? So tunawarudishia shukrani, mumeeleza maneno, tutatengeneza, sheria anasema tukimaliza ripoti itarudi kwenu, mtasoma muone namna gani, tena ndio watu waendelee kujadiliana ndio waone tunatengeneza Katiba ya aina gani. Asanteni sana.

**Com. Yano**: Asante sana Bwana Kangu na wakati huu tutapatia Maranga pia asemezane na nyinyi.

**Com. Maranga**: Mimi kwa niaba ya mimi mwenyewe pamoja na Tume ya Kurekebisha Katiba nawarudishieni asante. Yale maoni ambayo mumetoa ni ya muhimu, nimesikia huu mto wa Tana River unaanzia huko Mt. Kenya, kwa hivyo hakuna njia

mnaweza mkasema watu wa Mt. Kenya hamuwezi mkawa na husiano na wao, kwa sababu wakifunga hiyo maji itakua taabu kwenu hapa, ama namna gani? Kwa hivyo, ni muhimu sana wanakenya wote huo mto wa Tana River unaunganisha watu wa Central Province, unaunganisha watu Garissa, North Eastern, vile vile nyinyi hapa inaunganisha watu wa pastoralists na wale ambao ni wakulima, ama namna gani? Kwa hivyo mimi nawaombeeni heri sana, maoni yenu yamekua sawa kabisa, nawashukuru na Mungu awasaidie sana na mzidi kutuombea sisi kama Tume ili tuweze kukamilisha hii kazi, kwa sababu itakua ngumu sana na tunaona kweli kuna maneno mazito sana.

Asanteni. Thank you.

**Com. Yano:** Asanteni sana, tumeshukuru na tumefurahi kuwa nanyi, mumetoa maoni, maoni mazuri kabisa na kazi yetu kama wana Tume ni kuchukua hayo maoni yenu ili tukayafanyie kazi ikifika wakati wa kuchangia maneno ya Katiba katika National Constitutional Conference najua mtakua mumekubaliana wenyewe kwa wenyewe, ni nani watakuja kuendesha haya maneno yenu. Tumefurahi sana, infact I think this is one of the largest crowd we have worked with.

Thank you very much, and before we close may the district co-ordinator will close for us.

**Omar:** Basi wananchi watukufu ningependa kuchukua nafasi hii kwa niaba ya watu wa Garsen kurudisha asante kwa Makamishena wa Tume ya mageuzi ya Katiba kwa uvumilivu wao na kuchukua maoni yetu na nina hakika sauti zenu zimesikika kwa hivyo yangu nikutangaza ya kwamba ninaelewa kwa sababu mimi naishi sehemu hii kwamba watu wamesafiri kutoka mbali, kutoka Chara, kutoka Mnazini, Wema, kutoka Asa na wamekuja kutoa maoni yao. Na kwa sababu hiyo tumeandaa chakula kwa wale wote ambao wamehudhuria mkutano. Nimeambiwa kuna chakula cha kutosha nyinyi nyote na kubaki, kwa hivyo ni ulaji ambao utamua kama kitaisha ama kitabaki. Chakula hicho kiko kule primary school, Garsen primary school na chief wa hapa ama Assistant wake atakaa na nyinyi ili mle kwa makini na hasa wale watu wa mbali wapate kitu kabla ya kurudi nyumbani. Na wageni wetu pamoja na viongozi, Councillors na wale machief wengine pamoja na watu ambao wametoka Mombasa kina Karasinga, kina Katuda, hao tungependa tukae na Makamishena's ili wazidi kubadilishana mawazo wakati wa mankuli. Mankuli yao tumeandaa huko YWCA, tutaenda huko kwa ajili ya chakula. Kwa hivyo, kuna watu ambao wametoka mbali na wamefika hapa hawakuweza kutoa maoni, lakini si kupenda kwetu ni kwa sababu ya wakati na watu ambao wamewakilisha maoni tayari ni wengi ya kutosha. Nadhani hayo maoni yenu ambayo mko nayo ni kama yale ambayo Kamishena's tayari wamesikiza, kwa hivyo msisikie vibaya mkatoka hapa, mkasema hamkusikizwa. Kwa hivyo, yule mzee ambaye amekuja kulalamika sana nimemuomba msamaha kwamba wakati umeenda sana na wageni wetu wanaenda mbali, kwa hivyo nina hakika maoni yake yamewakilishwa, asisikie vibaya, akasema pengine hakusikizwa.

Ningependa sasa kusema Bura Constituency haijafanywa, kwa hivyo itafanywa na itatangazwa, tutawaelezea watu wa Bura, wakilishi bungeni wa Bura bado hatujafanya. Na sasa ningependa kumualika Sheikh Bakero ili aje hapa afunge kikao chetu cha leo kwa kumuweka Mwenyezi Mungu mikononi mwa kila mmoja ambaye yuko hapa. Asanteni sana na Mwenyezi mungu

awabariki.

**Sheikh Bakero:** Bismillahi Ralman Rahim, ee Mola tunakushukuru kwa kutuwezesha kukaa kwa makini na hekima. Ee Mola tunakuomba utuwekee fanaka katika haya yote tulioshauriana hapa ili yaweze kuchukuliwa kwa ubusara na hekima. Ya Allah, tunakuomba haya tuliojaribu kuyazungumza hapa yawe ni yenye manufaa kwetu sisi na kwa watoto watakao kuja baada yetu. Ya Allah tunaomba haya yawe na manufaa kwetu sisi na kwa Kenya nzima, iweze kuleta manufaa kubwa. Ya Allah tunakuomba utupe tangamano nzuri na kuweza kuishi pamoja. Uweze kuwahifadhi hawa wenye kuzunguka Tume ya Katiba wakitafuta haki kutoka kwa wananchi. Haki kama hiyo Ya Allah tunaomba kwamba wewe ndio mwenye kuweza kufunua wazi uweze kutuonyesha haki yetu na iweze kututawala yenyewe. Ya Allah tunakuomba haya yanayo andikwa sasa, yawe ni yenye haki na usawa kwa kila mmoja wetu. Tunaomba na tunamaliza maombi yetu kwa kumtaja mtume Mohammed Salaha.

Amen.

Meeting ended at 4.30 p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**